**22 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 22 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. AZIZA S. ALLY K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 133

**Kuongeza Posho kwa Askari na Wasimamizi wa Uchaguzi**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza posho kwa Askari na Maafisa Wasimamizi wa Uchaguzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wa Ngazi ya Jimbo na Kata hulipwa posho za kujikimu wanapokuwa wanatekeleza majukumu ya uchaguzi kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma kuhusiana na posho za Serikali. Kwa sasa Serikali imefanya maboresho kwa kuongeza viwango vya posho hizo kupitia Waraka wa Utumishi wa Umma Na.1 uliotolewa tarehe 24 Mei, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Watendaji na Walinzi wa Vituo vya Kupigia Kura, utaratibu wa uboreshaji wa viwango vyao vya posho utazingatiwa wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Bajeti ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa katika maelezo yake amesema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura utaenda sambamba na uboreshaji wa posho kwa mwaka 2025; ukizingatia mwaka huu tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utakuwa uchaguzi wa kwanza kwa awamu ya sita: Je, hawaoni kuna haja ya kuanza kulipa posho hiyo mwaka huu ili iweze kuleta motisha katika chaguzi hizo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Zanzibar Maafisa Usimamizi wa Uchaguzi na Askari huwa wanasimamia chaguzi mbili tofauti, chaguzi ya kumchagua Rais wa Tanzania, na wa Bunge la Muungano na chaguzi wa kumchagua Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na Madiwani Zanzibar, je, hawaoni kuna umuhimu wa kulipa posho mbili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa

Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni sahihi kwa mujibu wa jibu langu la msingi kama alisikiliza vizuri Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2022 mwezi Mei, tayari umeshaanza kutumika. Kwa hiyo, zingatio hilo lipo pia la kuweza kulipa posho kama jinsi ambavyo ametamani kuona kwamba zinalipwa.

Mheshimiwa Spika, pili, maboresho yatafanyika wakati Tume itakapokuwa imekaa na kuanza kufanya tathmini ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa bajeti ya uchaguzi ya mwaka huu ambapo mazingatio hayo yote yatakuwa ndani ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, swali la lake la pili anauliza kuhusu upande wa Zanzibar katika chaguzi kwamba ziko mbili; zile za Rais, na pia za Wabunge na Wawakilishi. Suala hili tunalichukua kama Serikali na tutazingatia kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Ukamilishaji wa Kituo cha Afya Kata ya Mbebe**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kata ya Mbebe kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi sambamba na kujenga vituo vipya.

Mheshimiwa Spika, Boma la Kituo cha Afya Kata ya Mbebe limejengwa kwenye Zahanati ya Mbebe ambapo eneo lina ukubwa wa ekari tatu. Eneo hilo halitoshi kwa ujenzi wa kituo cha afya. Hivyo, Halmashauri inapaswa kutafuta eneo litakalowezesha ujenzi wa kituo cha afya wakati Serikali ikiendela kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tuko katika hatua za mwisho za kupata eneo jipya katika Kitongoji cha Ipanga, naomba kupata *commitment* ya Serikali endapo *process* hizo zitakamilika. Je, Serikali itakamilisha huo mchakato haraka kwa sababu wananchi wa Mbebe wanapata changamoto sana hasa kwenye masuala ya afya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, tunacho Kituo cha Afya katika Kata ya Isansa lakini kwa muda mrefu sana hakina wodi za kulaza wagonjwa hususan wodi ya akina mama. Naomba kujua lini Serikali itatupatia wodi za akina mama katika Kituo cha Afya cha Kata ya Isansa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Mbebe kwa kuanza kutafuta eneo lingine ambalo litatosheleza ujenzi wa kituo cha afya. Nimhakikishie Mheshimiwa Juliana Shonza kwamba Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itatafuta fedha na kupeleka kwenye Kata ya Mbebe kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi kwenye ujenzi wa hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na upungufu wa majengo katika Kituo cha Afya cha Isansa, naomba nimhakikishie kwamba Serikali ilishafanya tathmini kwa vituo vyote vya afya vyenye majengo pungufu ya yale yanayohitajika kwa ajili ya kutoa huduma za afya. Hivyo, tutahakikisha pia tunapeleka fedha katika Kituo cha Afya Isansa kujenga hilo jengo la wazazi na majengo mengine ili tuweze kutoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kukamilisha Kituo cha Afya cha Ngimu katika Jimbo la Singida Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa na tayari tumeshakiingiza kituo hicho kwenye orodha ya vituo ambavyo vinatafutiwa fedha kwenye mwaka ujao wa fedha ili kiweze kujengewa majengo yanayopungua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; wananchi wa Kitongoji cha Iringong'wen Wilayani Longido wanatembea zaidi ya kilometa 35 kutafuta huduma za afya. Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za wanachi katika kumalizia zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumkumbusha na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Longido kwa ajili ya kuanza kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ili kuunga mkono juhudi za wananchi katika ukamilishaji wa zahanati hiyo.

Pale kama mapato ya ndani hayatatosheleza, Mkurugenzi alete taarifa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili Serikali iweze kuunga mkono umaliziaji wa zahanati hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kendege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, yapo mapendekezo ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo yote Tanzania. Kwa sisi wananchi wa Kalambo, pendekezo ni katika ujenzi wa Kituo cha Afya Katete. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na ujenzi wa vituo vya afya hivi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kwa kuthamini afya za wananchi, ilishaweka mpango mkakati wa kutambua maeneo ya kimkakati wa ujenzi wa vituo vya afya ikiwemo vituo vya afya katika Jimbo la Kalambo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kata hiyo ambayo ameitaja alishaiwasilisha kama ni eneo la kimkakati na Serikali inatafuta fedha ili tuweze kwenda kujenga kituo hicho cha afya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, je, lini Serikali itaanza kuwaunga mkono wananchi wa Kata ya Msia katika ujenzi wa kituo chao cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi katika ujenzi wa vituo vya afya kwa kutoa fedha kutoka Serikali Kuu, pia kutoa fedha kutoka mapato ya ndani. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumkumbusha na kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Vwawa, Mbozi kwa ajili ya kuanza kutenga fedha

za mapato ya ndani wakati Serikali Kuu ikitafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; naomba kujua Kituo cha Afya cha Ndola ni lini kitakamilika ili wananchi waweze kupata huduma iliyokusudiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue swali la Mheshimiwa Mbunge nikafuatilie kujua hicho Kituo cha Afya cha Ndola kimekwama katika hatua gani na nini kimekwamisha ili tuhakikishe tunakwamua mkwamo huo na kituo hicho tukikamilishe kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, sasa aulize swali lake.

Na. 135

**Hitaji la Waganga na Wauguzi kwenye Zahanati Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza Waganga na Wauguzi katika Zahanati za Buhulyu, Luhumbo, Mambali, Ikindwa, Lukuyi, Mbutu na Karitu – Bukene?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika vituo vya huduma za afya. Hivyo, Serikali imeendelea kuajiri

wataalamu wa kada mbalimbali za afya ambapo katika kipindi cha miaka mitatu Serikali imeajiri jumla ya watumishi 18,418 na kuwapangia vituo kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 jumla ya wataalamu 73 waliajiriwa na kupangwa kwenye vituo vya kutolea huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti na kuajiri wataalamu wa kada mbalimbali za afya ili kupunguza pengo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameidhinisha ajira mpya 46,000 zikiwemo ajira za kada ya Afya. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa *commitment* hapa kwamba katika hizi ajira mpya 46,000 ambazo ndani yake kuna ajira za kada ya afya, itapeleka angalau mganga mmoja na nesi mmoja kwenye Zahanati za Buhulyu, Luhumbo, Mambali, Ikindwa, Lukuyi, Mbutu na Karitu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwajali wananchi, tayari Mheshimiwa Rais, ametoa kibali cha ajira za watumishi wa sekta ya afya na pia watumishi wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatoa *commitment* siku ya leo kwamba kwenye zahanati hizi ambazo zina mtumishi mmoja mmoja, tutahakikisha kwenye ajira hizi ambazo zinafuata tunapeleka watumishi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ina upungufu mkubwa sana wa watumishi wa kada ya Afya kwenye vituo vya afya kumi na Hospitali ya Wilaya na zahanati kumi ambazo hazina watumishi. Ni lini mtapeleka watumishi kwenye Halmashauri hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishafanya tathmini ya maeneo ya halmashauri kote nchini yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi na katika kile kibali cha ajira kinapotokea maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi wa watumishi yanapewa kipaumbele cha kupelekewa watumishi wengi zaidi kuliko maeneo yale ambayo yana upungufu mdogo zaidi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba Halmashauri ya Tanganyika na halmashauri nyingine zote zenye maeneo ambayo yana upungufu mkubwa zaidi wa watumishi yatapewa kipaumbele zaidi wakati wa ajira hizi ili watumishi waweze kupelekwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wauguzi na waganga katika Zahanati ya Makuburi na Mavurunza katika Halmashauri ya Ubungo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge Mariam kwamba tunatambua kwamba vituo hivyo vinahudumia wananchi wengi sana na vinahitaji kuongezewa watumishi. Tayari Serikali imeshatambua pengo la watumishi katika vituo hivyo na katika ajira hizi tutapeleka watumishi. Pia tutaendelea kupeleka watumishi kwa awamu kadri ya vibali vya ajira vinavyojitokeza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga inahudumia wagonjwa mpaka kutoka Halmashauri ya Mlimba, je, Serikali iko tayari kutuangalia kwa macho mawili na kutuongezea watumishi katika Hospitali ya Mji wa Mafinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari kuiangalia Hospitali ya Mji wa Mafinga kwa jicho la tatu na kupeleka watumishi zaidi ili wananchi wetu waweze kuhudumiwa vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 136

**Mji wa Kibaha Kupewa Hadhi ya Manispaa**

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaupatia Mji wa Kibaha hadhi ya Manispaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, halmashauri huanzishwa au kupandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipokea wasilisho la Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa mara ya kwanza mwaka 2016 na kuchambua kwa kuzingatia vigezo ambapo haikukidhi vigezo. Maelekezo yalitolewa kwa ajili ya maboresho. Uchambuzi wa awamu ya pili ulifanyika mwezi Mei, 2023 ambapo timu maalumu ilifika uwandani mwezi Septemba, 2023 ili kubaini hali halisi wakati wa zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, ombi hili kwa sasa lipo katika hatua za mwisho za uhakiki wa vigezo na mrejesho utatolewa kabla ya mwezi Juni, 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, ila kwa niaba ya Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, je, Serikali haioni haja sasa kufanya kwa haraka kwa sababu Mkoa wa Pwani umeanza mwaka 1972 na hauna hata halmashauri moja yenye hadhi, lakini pia Halmashauri ya Kibaha Mjini ina wakazi zaidi ya 200,000; lini kilio hiki kitazingatiwa kwa haraka? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inatekeleza suala hili kwa haraka zaidi, lakini kigezo kikubwa ni namna ambavyo halmashauri yenyewe inakidhi vigezo vya msingi vilivyowekwa ikiwemo idadi

ya wananchi ambao hawapungui 300,000 lakini na vigezo vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari timu yetu imeshafika uwandani kuona vigezo vingine na mwezi Juni mwaka huu tutaleta majibu ya hatua ambayo inafuata. Ahsante.

**SPIKA:** Mhe. Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, Muleba ni moja ya miji yenye hadhi ya miji midogo tangu mwaka 2008. Ni lini itapata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishafanya tathmini kwenye Mamlaka za Miji Midogo kote nchini. Zipo mamlaka ambazo zinakidhi vigezo vya kupanda kuwa Halmashauri za Miji, lakini zipo mamlaka nyingi ambazo pia bado hazijakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kuwa Hamashauri za Miji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kikoyo kwamba Halmashauri ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Muleba ni moja ya mamlaka ambazo zinafanyiwa tathmini ya vigezo na mara tutakapokuwa tumefanya tathmini na pale Serikali itakapokuwa ipo tayari kwa ajili ya kuanza kupandisha hadhi Mamlaka za Miji kuwa Halmashauri za Miji tutakwenda kufanya hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, Mlandizi ni Mamlaka ya Mji Mdogo tangu mwaka 2004 na Serikali inafahamu kuwa tunaenda kuujenga Mji wa Kwala, je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi kufanya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini kuwa Mji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mji wa Mlandizi unaendelea kukua kwa kasi kubwa, lakini ujenzi wa Mji wa Kwala utaongeza kasi ya ukuaji wa Mamlaka ya Mji wa Mlandizi pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalitambua hilo, na tayari imeshafanya hatua kadhaa kuelekea kuona vigezo kama vinafikia hatua inayotakiwa ili iweze kupandishwa hadhi ya kuwa Halmashauri au Manispaa, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Upungufu wa Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hesabu**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, kuna upungufu wa walimu kiasi gani kwa shule za msingi na sekondari kwa masomo ya sayansi na hesabu nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa upungufu wa walimu wa masomo ya Hisabati na Sayansi katika shule za sekondari nchini. Kwa sasa mahitaji ya walimu wa sayansi na

hisabati ni walimu 71,027, waliopo ni walimu 31,417, na upungufu ni walimu 39,610, sawa na 55.8%.

Mheshimiwa Spika, kufuatia upungufu huo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kila mwaka kuajiri walimu wa masomo mbalimbali wakiwemo wa masomo ya sayansi na hisabati. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023 Serikali iliajiri walimu wa masomo ya sayansi na hisabati 10,853. Aidha, katika mwaka 2023/2024 Serikali inategemea kuajiri walimu 12,000 wakiwemo wa masomo ya hisabati na sayansi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ina upungufu wa walimu wa sayansi na hesabu wapatao 83,000 lakini pia ina walimu wa sayansi na hesabu ambao wanajitolea 44 ambao ni takribani 53% ambao wamehakikiwa. Kwa sababu Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 na ukichukua *sample* ya Tarime Mji ina maana Tanzania nzima wana *average* zaidi ya walimu hao wanaojitolea ni zaidi ya 50%, sasa kwa nini Serikali katika hizo ajira 12,000 isitenge 50% kwa ajili ya walimu hao wanaojitolea ili kuendelea kutoa motisha zaidi kwa walimu wengi kuweza kujitolea na kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi na hesabu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Shule ya Msingi Magufuli yenye wanafunzi wenye uhitaji maalum iliyopo Halmashauri ya Mji wa Tarime ambayo ni kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa akili, ulemavu wa kuona na kusikia, ina upungufu wa walimu 13 ambao ni takribani 53%. Kwa nini Serikali isitoe kipaumbele kwa shule zote maalumu nchini kwa kuwa wote tunatambua ugumu uliopo wa kufundisha wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na akili? Serikali iweze kutoa kipaumbele na kupeleka walimu toshelezi katika shule hizi *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la walimu wanaojitolea kupewa kipaumbele

katika ajira zilizotangazwa za walimu, maoni haya ya Mheshimiwa Mbunge tunayachukua na tutaona namna ya kuyachakata tulishirikiana na wenzetu wa Utumishi ili tuweze kuona ni namna gani nzuri tunazingatia miongozo na taratibu za kiutumishi katika kuajiri walimu hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili ambalo amezungumzia uhitaji wa kuajiri walimu wenye uhitaji maalumu, kwa mujibu wa taratibu katika kila ajira zinazokuwa zimetangazwa za walimu angalau asilimia tatu, ni lazima wawe ni walimu wanaofundisha wanafunzi wenye uhitaji maalumu. Mwaka 2023 Mei, ajira za mwisho za walimu tayari waliajiriwa walimu kwa 2.7% kwa sababu kwa kawaida wanaojitokeza huwa hata asilimia tatu hawafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watakaojitokeza, walimu watakaoomba nafasi hizo ambao wanakidhi vigezo vya kuwa walimu kwa ajili ya wanafunzi wenye uhitaji maalumu kwa mujibu wa taratibu watachukuliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo kubwa la walimu, takwimu zilizopo, walimu wa sayansi ni walimu wa somo la *physics*. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuhakikisha inaajiri walimu wa somo hilo ukizingatia tunaenda kwenye mafunzo ya amali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na walimu na hasa wanaofundisha masomo ya sayansi na kwa kila ajira zinapotangazwa, Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba inaajiri walimu wa sayansi. Kama tunavyofahamu, tayari zimetangazwa ajira za walimu 12,000. Kwa hiyo, Serikali itazingatia katika kuajiri walimu hao 12,000 wapatikane walimu wa sayansi na hasa wa somo la fizikia kama aliyotaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Simiyu kuna upungufu wa walimu zaidi ya 6,000 katika shule za sekondari na za msingi: Je, ni lini Serikali italeta walimu wa kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kutetea wananchi wake na kutetea na wanafunzi waliopo katika eneo lake la utawala. Aidha, Serikali tayari imeshatangaza ajira 12,000 kwa sababu inatambua upungufu wa walimu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika ajira hizi za walimu 12,000 jimbo lake la lenyewe litatizamwa kwa kipaumbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu walimu ama watumishi wanaojitolea Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora walishatoa kauli humu ndani kwamba kuna mpango maalum Serikali inatayarisha kwa ajili ya jambo hili. Kwa hiyo, nafikiri Ofisi ya Rais, TAMISEMI muwasiliane na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili mjue huu mpango umefikia wapi? Kwa sababu hawa watu wanaojitolea kule, lazima wapewe kipaumbele kwenye hoja ya ajira. Nadhani lilishazungumzwa humu ndani, kwa hiyo ofisi hizi mbili zishirikiane ili ule mpango maalumu sasa ufikie mahali ambapo hakutakuwa na maswali kuhusu watu wanaojitoea huko mashuleni na maeneo mengine pia.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 138

**Utaratibu wa Urasimishaji na Umilikishaji wa Ardhi kwa Wanawake Nchini**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO K.n.y. MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi kuweka utaratibu rahisi wa urasimishaji na umilikishaji ardhi hususani kwa Wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kuboresha usalama wa miliki za ardhi kupitia mradi wa *(LTIP)* kwa mkopo wa fedha kutoka Benki ya Dunia ambayo unafanyika katika mamlaka za upangaji 58 nchini. Kupitia mradi huo, haki za wanawake zimezingatiwa ipasavyo katika utoaji wa elimu na uhamasishaji umiliki wa ardhi kwa wanawake na umiliki wa pamoja baina ya mume na mke.

Mheshimiwa Spika, kupitia utaratibu huo, vikosi kazi vimeundwa kwa ajili ya kushughulikia uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa makundi maalum ya wanawake, wazee na walemavu katika suala la urasimishaji makazi pamoja na umiliki wa pamoja wa ardhi. Aidha, elimu inatolewa kupitia vyama vya hiari vya kijamii, mashirika yasiyo ya Kiserikali; *CSO's* na *NGO's* ambapo mikutano ya elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa miradi imefanyika katika ngazi za Mitaa, Kata na Wilaya. Jumla ya wananchi 3,249 wamehudhuria mikutano hiyo wakiwemo wanaume 1,518 na wanawake 1,731.

Mheshimiwa Spika, mradi pia umewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi nchini kutoka 25% hadi 41%. Vilevile idadi ya hatimiliki za pamoja *(joint titles)* kati ya wanandoa zimeongezeka na kufika 10% ya hati zinazotolewa.

**SPIKA:** Mhe. Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na majibu na mradi huu wa *LTIP* kufanya kazi nzuri, ningependa kujua je, Serikali haioni umuhimu wa kuyafanyia kazi au kuifanyia kazi ile Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Kukabiliana na Migogoro ya Ardhi iliyofanyika mwaka 2020 ili sasa iweze kufanyiwa kazi, na wanawake wengi zaidi waweze kumiliki ardhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba haya tunayoyatekeleza sasa yameweza vilevile kuunganisha mambo mbalimbali ikiwemo hiyo taarifa iliyotolewa ya mwaka 2020 ambayo imetupa dira ya kuendelea kuhamasisha akina mama kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwa sasa wameongezeka kutoka 25% mpaka 41% ambalo ni ongezeko kubwa ambalo linaonesha wazi kabisa mwamko wa akina mama umeongezeka kwa asilimia kubwa sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na mpango huo mzuri wa urasimishaji na umiliki wa ardhi hizo, je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa nyumba zote za tope kwenye ardhi hizo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ntara, hebu rudia swali lako.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango wa urasimishaji na umiliki wa ardhi hizo, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba nyumba zote za tope zinaondoka kwenye ardhi hizo kabla hata hawajafanya huo urasimishaji?

**SPIKA:** Nipo natafakari kama... Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ujenzi wa nyumba hizi unategemea hali halisi ya wananchi wa eneo lile. Katika namna yoyote ile, kuondoa nyumba za tope maana yake ni kuongeza uhamasishaji kwa jamii kuitumia mifumo mbalimbali ya kujipatia fedha zinazoweza zikawahamisha kutoka kwenye nyumba za tope kwenda kwenye nyumba za kisasa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge muwe sehemu ya wahamasishaji ili maeneo ambayo nyumba za tope zipo, basi tushirikiane katika kuwahamasisha wananchi wa eneo lile kutumia uchumi walionao katika maeneo hayo kuboresha makazi yao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba sasa aulize swali lake.

Na. 139

**Miradi ya Maji katika Jimbo la Kibamba**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza: -

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya kutokamilika kwa Miradi ya Maji katika Jimbo la Kibamba?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa miradi mitatu ya usambazaji wa maji kutokea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi Bagamoyo *(2B-2F)*, Mshikamano na Kitopeni ambapo miradi hiyo inanufaisha wakazi wapatao 210,876 wa Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa usambazaji maji Kusini mwa Dar es Salaam (Bangulo) ambapo utekelezaji wake umefikia 25% na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024. Mradi huo ukikamilika utanufaisha wakazi wapatao 271,863 wa Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa miradi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Jimbo la Kibamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri na tuendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kututekelezea miradi hiyo mitatu katika kipindi chake cha miaka mitatu. Pamoja na majibu hayo, naomba niulize maswali ya mawili (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa miradi iliyotamkwa kwenye majibu ya msingi ni ukamilishaji wa matanki au vihifadhia maji, lakini ili mradi ukamilike ni lazima usambazaji wa mabomba kwenda kwa wananchi ukamilike ili thamani ya fedha itimie. Sasa yapo maeneo kama CCM ya zamani Mpijimagohe, Torino kwa Mvungi, kwa Mzee Kadope na maeneo ya kwa Yusuph Michungwani.

Ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya muda mrefu kupeleka mabomba hapa katika maeneo hayo?

(b) Mheshimiwa Spika, Mtaa wa Msumi hasa Msumi *Center* na Darajani ni muda mrefu hawajawahi kuyaona maji safi na salama, lakini tayari Serikali imefanya utafiti wake na kutekeleza mradi au ina nia ya kutekeleza mradi wa shilingi bilioni 13.9. Je, ni lini sasa Serikali inatoa *commitment* kwa wananchi wa Kibamba ya kuanza kutekeleza mradi huo ambao mmeshaufanyia tathmini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia miradi hii kwa niaba ya wananchi wake wa Jimbo la Kibamba na kwa kweli anaendelea kufanya kazi nzuri. Sasa kupitia mradi wa kuboresha huduma za maji katika Mkoa wa Dar es Salaam, Serikali imepenga kiasi cha shilingi bilioni 33 ambapo ndani ya fedha hizo kuna shilingi bilioni 13.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi katika maeneo ya Msakuzi, Makobe, Msumi A, B, C, Tegeta, Mpindi na Magohe. Maeneo yote hayo yatakuwa ndani ya mradi huo wa kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika pamoja na maeneo ya Tegeta, utaweza kunufaisha wakazi takribani 166,548. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira katika bajeti hii itakapopitishwa, basi mradi huo utaanza mara moja. Katika maeneo ya usambazaji wa mabomba, yote hayo yapo ndani ya mradi huu wa kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge waliosimama mwanzo nilishawaona, kwa hiyo, nilishawaandika hapa, mnaosimama mara ya pili samahani sitawaita ila wale ambao mnapata nafasi, nenda moja kwa moja kwenye swali na Mheshimiwa Naibu Waziri moja kwa moja kwenye jibu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge inakuwa nimeshawataja tayari. Mheshimiwa Deodatus Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nini kauli ya Serikali kuhusiana na Mradi wa Maji Igongwi wa kupeleka maji kwenye kata tatu ambao umekamilika lakini bado maji hayawafikii walengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mradi huu umeshakamilika, lakini ni katika hatua ya kwanza. Hatua ya pili ni kuhakikisha sasa maji yanawafikia wananchi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge atupe nafasi kusudi mkandarasi aendelee na hatua ya mwisho ili wananchi wapate maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, wananchi waishio katika Visiwa vya Besi na Tefu hawana maji safi na salama kwa maana ya maji ya bomba. Ni lini Serikali itawapelekea maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Base ni moja ya visiwa vidogo vidogo ambavyo viko katika Ziwa Victoria, lakini Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria walifanya tathmini na kugundua kwamba hakuna maji ardhini. Tunachokifanya kwa sasa kupitia Mamlaka ya Maji Mwanza, *MWAWASA* wanaenda kuanzisha mradi mdogo ili waweze kuchakata maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika kisiwa hicho ambacho zaidi kinakaliwa na wavuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Serikali kuhakikisha katika mwaka huu wa fedha 2024 tutaanza mradi huo na hatimaye wananchi wa kisiwa hicho watapata maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, lini Serikali itatatua changamoto ya maji iliyopo ndani ya Wilaya ya Makete kule Mfumbi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Njombe, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kikao chako hiki cha Bunge, kwa sababu ni eneo *specific* ambalo amelitaja, tuweze kuonana ili niweze kujua na kuona kama limetengwa. Kama halijatengwa, basi tuone Serikali tunafanya nini ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wananufaika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Wabunge wanakuwa wametajwa, huna haja ya kuwataja tena. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 140

**Uhitaji wa Maji katika Mji Mdogo wa Gairo**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Mradi wa Maji ya Mserereko katika Milima ya Nongwe kwa wananchi wa Gairo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa miradi ya maji miwili ya Gairo na Njungwa kwa kutumia vyanzo vya Mserereko vinavyopatikana kwenye Safu za Milima ya Nongwe na Mamiwa Wilayani Gairo. Kazi zinazotekelezwa kupitia miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa ukarabati wa madakio matano *(intakes)*, ujenzi wa matanki matano yenye jumla ya ujazo wa lita 2,300,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 90 na ujenzi wa vituo 58 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani wa asilimia nane na inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 87,134 waishio kwenye Kata nane za Rubeho, Msingisi, Gairo, Ukwamani, Magoweko, Chakwale, Kibedya pamoja na Mandege.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuendelea kuboresha hali ya huduma ya maji Wilayani Gairo, Serikali ina mpango wa kujenga miradi mitatu ya Nongwe, Lukinga na mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji Gairo Mjini kwa kutumia chanzo cha mto Chagongwe kinachopatikana kwenye Milima ya Nongwe katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri kuwa wananchi wa Gairo watapata maji Desemba, 2024. Hata hivyo nina maswali mawili. Manispaa ya Morogoro mpaka wapate maji safi na salama ya kutosha, wanategemea Bwawa la Mindu. Bwawa hili limechukua muda mrefu. Je, ni lini Bwawa hili litaanza ukarabati wake, kwani limechukua miaka mingi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wananchi wanaozunguka Bwawa la Mindu wameshafanyiwa tathmini kusudi waondoke, na ni muda wa miezi minane hawafanyi kazi yoyote. Je, ni lini watapata fedha zao za fidia ili waweze kupisha bwawa hili? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi huu wa uboreshaji wa bwawa hili tunatarajia kuingia mkataba na mkandarasi ifikapo Septemba, 2024. Vilevile, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.37 kwa ajili ya kuwalipa wananchi wanaozunguka katika lile bwawa ili waweze kupisha mradi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari hizo fedha zipo kwa ajili ya mchakato, kwa ajili ya malipo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba wananchi wake wa eneo hilo tayari watakuwa wamenufaika na mradi huo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Kisondela katika Wilaya ya Rungwe hawana maji safi na salama. Ni lini Serikali italeta na ukizingatia kata hii Mheshimiwa Spika ni mdau mkubwa wa maendeleo na ni mlezi wa kata hiyo? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kata hiyo wewe ndiye mlezi, basi Serikali inalichukua. Vilevile tunatambua mchango wa Mheshimiwa Mbunge kwa kuisemea kata hiyo kwa umuhimu huo, naomba tutoke hapa tuonane ili tuweze kulichambua na kuona limekwama wapi ili tuweze kuwasiliana na *RUWASA* walioko katika eneo husika tuone kama iko kwenye mpango ili tuweze kutekeleza kwa haraka. Kama haiko kwenye mpango, basi Serikali ina njia nyingi za kutafuta vyanzo vya fedha ili kuhakikisha tunatekeleza miradi hiyo ya maji na wananchi waweze kunufaika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Magoto na Mradi wa Maji Itiryo ni mradi wa mserereko, wakati wa mvua maji yanakuwa machafu. Ni lini Serikali itapeleka pale chujio au kuweka dawa ili maji yawe safi na salama kwa wananchi wangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, samahani sijalisikia vizuri swali lake.

**SPIKA:** Ametaja vijiji hapo, labda kama hujavisikia hivyo vijiji. Amesema huo mradi wa mserereko ni lini utafika huko? Unataka majina ya vile vijiji, si ndiyo? Mheshimiwa Waitara rejea majina ya vijiji.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji katika Kata ya Nyakonga, Magoto na Mradi wa Maji Itiryo ni mradi wa mserereko, lakini hauna chujio wala dawa. Kwa hiyo, wakati wa mvua, maji ni machafu. Ni lini watapeleka chujio katika maeneo hayo ili maji yawe safi na salama kwa wananchi wangu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba inafikisha maji safi na salama. Kwa hiyo, kwa sababu ya changamoto hiyo, Serikali inalichukulia hatua moja kwa moja na tutakwenda kuona kwamba eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliongelea lina changamoto ipi ili wataalamu wetu waweze kuchukua hatua stahiki, ahsante, *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa miradi mingi ya maji inayoendelea ukiwemo Mradi wa Maji Ukara unasuasua kwa sababu ya wakandarasi kutolipwa

pesa zao, ni lini sasa Serikali itakwamua miradi hii ili iweze kuleta tija kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imetenga kiasi cha shilingi bilioni 60, pia fedha ambazo zinatokana na mfuko wetu wa maji shilingi bilioni 18, vilevile *RUWASA* kuna fedha ambazo wamepata shilingi bilioni 30. Kwa hiyo, niamini kabisa kwamba wakandarasi ambao hawajalipwa na wale ambao tayari wameshawasilisha hati za madai, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan lengo lake ni kuwalipa wakamilishe miradi kwa wakati na Watanzania wapate maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa kutoa maji kwenye Kijiji cha Turuki kuyapeleka Liwale Mjini ni lini utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mradi wa kuyatoa maji Kijiji cha Turuki...

**SPIKA:** Mheshimiwa umeshasikika, kwani nani amesema urejee?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, anasema hajasikia.

**SPIKA:** Mheshimiwa, umeshasikika. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilipokee kwa ajili ya hatua stahiki. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 141

**Ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Bonde la Mto Kilombero**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji katika Bonde la Mto Kilombero?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2016 Serikali ilifanya upembuzi yakinifu wa awali *(prefeasibility)* wa miradi ya umwagiliaji katika bonde la Kilombero lenye ukubwa wa hekta 53,344 ambapo skimu za Kisegese, Udagaji, Mgungwe na Mpanga - Ngalamila zilihusishwa katika kazi hiyo. Upembuzi yakinifu wa awali ulibaini kuwa kuendelezwa kwa skimu hizo kutanufaisha kaya 15,102 na kutoa ajira 69,476.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina *(feasibility study and detailed design)* wa miradi ya umwagiliaji katika Bonde la Mto Kilombero kupitia Mshauri Elekezi ambaye yupo eneo la kazi. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, bonde hilo litaingizwa katika mpango wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Njagi ni skimu ambayo haijakamilika na wananchi wameanza kunufaika nayo. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kuhifadhia maji?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Mlimba tumelazimika kuishi kwa matumaini, je, sisi wananchi wa Kata ya Utengule, Chisano, Ching'anda, Mgeta, Mchombe na Idete, tungependa kujua ni lini mradi huu utaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mradi wa Skimu ya Njagi umeshaanza na kinachosubiriwa ni bwawa na liko katika awamu inayofuatia, kwa hiyo, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, mradi huo upo katika mpango wa ujenzi wa bwawa katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo, ninaamini utatekelezeka katika kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa eneo la Kata za Utengule, Chisano, Ching'anda, Mgeta, Mchombe na Idete na zenyewe kwa sababu Mshauri Elekezi yuko *site* na tumekubaliana kwamba katika *next financial year* tunaliingiza katika mpango wa bajeti, maana yake tutaanza utekelezaji katika mwaka wa fedha unaokuja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini utakuwa tayari kutembelea Halmashauri ya Mji wa Ifakara kujionea maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nipo tayari muda wowote. Tukiomba ruhusa tu kwa Mheshimiwa Spika, hata *weekend* tutakwenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Magessa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, je, katika utekelezaji wa bajeti mwaka huu wa fedha, ni lini Serikali itaanza mchakato wa miradi ya umwagiliaji katika maeneo yaliyo pembezoni mwa Ziwa Victoria Jimboni Busanda ukizingatia imebaki miezi miwili kwenye hii bajeti? Nashukuru sana,

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Miradi mingi ambayo ipo katika mwaka wa fedha wa bajeti uliopo sasa hivi, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kuitangaza kila wakati na ninaamini kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha tutakuwa tumeshatangaza na kupata mkandarasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

Na. 142

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji – Arumeru Mashariki**

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Skimu za Umwagiliaji katika Tarafa za King'ori na Mbuguni pamoja na eneo la Kusini mwa Tarafa ya Poli – Arumeru Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Tarafa za King'ori, Mbuguni na Poli zina skimu 13 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 18,032 na zinanufaisha wakulima 13,546. Skimu hizo ni Kisimiri Juu, Kisimiri Chini, Ukombozi, Olkung'wado, Ngabobo, Mwakeny, Kyamakata,

Momela, Nasula, Mapama, Domikwa, Kammama na Valeska. Aidha, mazao makuu yanayolimwa katika skimu hii ni nyanya, mahindi, maharage na mbogamboga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika Skimu za Kisimiri Juu na Kisimiri Chini zenye ukubwa wa hekta 802. Vilevile, skimu za Kyamakata, Ukombozi, Ngabobo, Mapama, Momela, Mwakeny, Olkung'wado, Kimosonu, Eyani, Maktemu na Oldonyo Wass zipo kwenye mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujua gharama halisi za ujenzi. Baada ya usanifu kukamilika, skimu hizi zitaingizwa kwenye mpango wa ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Ni lini utakuwa tayari kutembelea Jimbo la Arumeru Mashariki kukagua skimu za umwagiliaji alizotaja Mheshimiwa Mbunge hapa?

Swali la pili, katika mwaka wa fedha uliopita Wizara ya Kilimo, Mradi wa Umwagiliaji wa Ngipa, Engusero-Kiteto ulipitishwa, ni lini sasa mtaanza kujenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kutembelea hizo skimu, katika moja ya *weekend* tuombe ruhusa tu kwa Mheshimiwa Spika kama nilivyoahidi kwa Mheshimiwa Abubakari Asenga, tukafanye kazi. Nguvu tunayo na uwezo wa kufanya hiyo kazi tunao, Mheshimiwa Dkt. Samia ametuamini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Skimu ya Ngipa ambayo ilikuwepo katika mwaka wa fedha uliopita, nina uhakika Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iko katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi ili iweze kufanyiwa kazi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 143

**Kuongeza Uzalishaji Zao la Pareto**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa zao la pareto nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza uzalishaji wa zao la pareto. Mikakati hiyo ni pamoja na utafiti na uzalishaji wa mbegu bora, elimu ya kilimo bora na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kuongeza thamani na mashamba makubwa ya kilimo cha pareto.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mikakati hiyo, uzalishaji wa pareto umeongezeka kutoka tani 3,150 mwaka 2022/2023 hadi tani 4,238 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 121% ya lengo la kuzalisha tani 3,500. Aidha, kilo 5,130 za mbegu bora za pareto zimesambazwa katika msimu wa 2023/2024 kwa wakulima 10,260 wa pareto katika mikoa sita inayolima zao hilo ambayo ni Mbeya, Iringa, Songwe, Njombe, Manyara na Arusha sambamba na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima 2,530.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kuchakata maua ya pareto vimeongezeka kutoka viwanda viwili vilivyokuwepo mwaka 2020/2021 hadi viwanda vinane mwaka 2022/2023 vinavyowezesha uongezaji wa thamani na kupanua wigo wa masoko ya pareto na bidhaa zake. Vilevile Serikali imeanza kushirikiana na Kampuni ya Pareto Tanzania *(PCT)* kuanzisha shamba la ekari 300 katika Wilaya ya Makete kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kuanzisha mashamba makubwa, na mpango huo utaendelea katika maeneo mengine ya uzalishaji wa pareto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Pia, nawapongeza kwa jitihada za kuongeza zao la pareto, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali sasa ina mpango gani wa kujitengenezea viuatilifu vyake kwa kutumia pareto ambayo haina madhara kwa binadamu, rafiki kwa mazingira na pia haijengi usugu kwa wadudu na kupunguza au kuacha kabisa uingizaji wa viuatilifu nchini vinavyotengenezwa kwa kemikali *(synthetic)* yenye madhara makubwa kwa mazingira na pia kwa afya ya watumiaji?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali sasa ina mpango gani kuwasaidia wakulima wa pareto Mkoani Manyara hususani Wilaya ya Mbulu na Babati kuwapa pembejeo na pia kuwasaidia vikaushio vya maua ya pareto? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali katika utengenezaji wa viuatilifu upo katika hatua mbili, hatua ya kwanza tunahamasisha wawekezaji wa viwanda kwa maana ya sekta binafsi kuingia ili waweze kuzalisha viuatilifu na ndiyo maana unaona hata sasa hivi viwanda vimetoka viwili vimefika vinane.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ya Serikali ni kwamba sisi Serikali tukishirikiana na sekta binafsi kwa maana ya *PPP* tutafanya shughuli hiyo ili tuweze kuzalisha viuatilifu vinavyotokana na mazao ya pareto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwasaidia wananchi wa maeneo ya Mbulu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, hiyo ni sehemu ya mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunatoa pembejeo pamoja na vikaushio kwa wakulima. Kwa hiyo, kila mwaka wa bajeti mipango hii tunaendelea kuiweka. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 144

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi Kata za Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi katika Kata za Berege na Ng'hambi Mpwapwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Berege imetenga eneo lenye ukubwa wa meta za mraba 1011.5 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata. Ujenzi wa kituo hicho umeshaingizwa kwenye mpango wa ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Kata 647 vitakavyojengwa nchi nzima kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kata ya Ng'hambi bado haijatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kata ya Ng'hambi na kata nyingine zisizokuwa na Vituo vya Polisi vya Kata, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, utaratibu wa kuwa na Polisi Kata kila kata umesaidia kupunguza uhalifu katika maeneo mengi. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuongeza idadi ya Polisi Kata angalau kufikia wawili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni nini mkakati wa Serikali kuwapatia vitendea kazi Polisi Kata, kwa mfano pikipiki, ili ziwasaidie katika kutekeleza majukumu yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Malima, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali imeendelea kuajiri Askari wa Jeshi la Polisi, na jinsi bajeti itakavyoruhusu. basi tutaendelea kuajiri askari wa kutosha na hatimaye kuwafikisha walau wapatikane wawili kwenye kila kata kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mahitaji ya pikipiki kwa nchi nzima kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ni pikipiki 4,434 na kwa awamu ya kwanza tayari Serikali imeshasambaza pikipiki 105 kwa maana ya pikipiki 95 upande wa Tanzania Bara na pikipiki 10 kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi bajeti itakavyoruhusu, tutaendelea kununua pikipiki kwa awamu ili kuhakikisha zinafika kwenye kata zetu, ili kuimarisha ulinzi na usalama wa wananchi wetu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, sasa aulize swali lake.

Na. 145

**Kudhibiti Makosa ya Kimtandao Nchini**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED K.n.y. MHE. MAULID SALEH ALI** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kudhibiti mfumo wa makosa ya kimtandao *(cyber crime)* ili yasitokee nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, uhalifu wa makosa ya mtandaoni unasimamiwa na Sheria Na. 14 ya Mwaka 2015 na ndiyo Sheria inayodhibiti makosa haya. Sheria inaelekeza matumizi sahihi ya mtandao na imeainisha adhabu kwa makosa ya matumizi mabaya ya mtandao. Serikali katika kuimarisha udhibiti wa makosa ya mtandaoni imeanzisha mkakati wa Taifa wa udhibiti wa usalama mtandaoni wa kuanzia mwaka 2022 – 2027.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu utawatumia wataalam mbalimbali katika kuratibu ugunduzi, kuzuia, kukataza, kufanya uchunguzi wa majibu na kuandaa mashitaka ya uhalifu. Pia, kuimarisha mazingira ya matumizi ya mtandao na kuboresha sheria iliyopo, kulinda huduma muhimu za habari, kuendeleza ujuzi kwa wafanyakazi na usalama mtandaoni, kutoa elimu kwa wadau na kuweka ushirikiano wa Serikali, wafanyabiashara na watu binafsi ili kudhibiti matukio ya uhalifu mtandaoni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina ushauri mdogo tu kwa Serikali. Kwa vile haya makosa ya uhalifu mitandaoni yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku, ninaishauri Serikali ijaribu kukiwezesha Kitengo hiki cha *Cyber,* ili kiwe na mfumo mzuri wa kufanya kazi zake kwa wepesi pamoja na kujaribu kurekebisha baadhi ya sheria ambazo zimekuwa kikwazo katika utendaji wao wa kazi za kila siku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona umepewa ushauri hapo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri na tutaufanyia kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, sasa aulize swali lake.

Na. 146

**Ujenzi wa Barabara ya Kyaka – Katoro – Ibwera hadi Kyetema, Nkenge**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kyaka Katoro – Ibwera hadi Kyetema Nkenge kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Kyaka – Katoro – Ibwera hadi Kyetema yenye urefu wa kilometa 60.7 pamoja na daraja la Kalebe kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa taratibu za kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 10 za barabara hiyo kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi wa daraja la Kalebe zinaendelea na inategemewa zabuni za kazi zitakuwa zimetangazwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2024. Kwa sehemu iliyobaki Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa *commitment* ya Serikali katika barabara hiyo na ni kweli, imeshakabidhiwa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, naomba kujua ujenzi wa barabara katika Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Misenyi,

Barabara ya Katuma – Bukwali ambayo nimekuwa nikiomba iongezewe bajeti kwa ajili ya kuikamilisha kwa kiwango cha lami, je, ni lini hiyo bajeti itaongezwa ili iweze kukamilika?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, naishukuru Serikali kwamba barabara ya Mutukula kwenda Minziro, mpaka sasa hivi kilometa sita tayari, je, ni lini sasa kile kipande cha kilometa saba kwa wale wananchi kitakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Barabara ya Katoma - Bukwali yenye urefu wa kama kilometa 38, tulikuwa tunaijenga kwa awamu na karibu kilometa nane zimekamilika. Hata hivyo, tulichokifanya Serikali ni kumpata Mhandisi Mshauri ili aweze kusanifu barabara yote na tuweze kuijenga yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mutukula – Minziro, na kwa bahati nzuri hizi barabara zote nimezitembelea, imeshafunguliwa yote kwa maana ya kuifungua ambayo ilikuwa haipo, na sasa tunatengeneza tuta. Tunapoongea sasa, tayari mkandarasi wa kuendelea kutengeneza tuta ameshapatikana ili barabara ipitike mwaka wote ikiwa ni pamoja na kujenga madaraja ambayo yako katika barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaongeza pesa kwa Barabara za Nata – Sanzate na Busekela – Mugango hadi Musoma Mjini kwa sababu ni barabara zilizokaa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Sanzate – Nata yenye urefu wa kilometa 40, mkandarasi yuko *site* anaendelea kujenga, labda tu ni kasi iongezeke. Pia barabara ya Musoma – Busekela yenye urefu wa kilometa 40 inatangazwa mwaka huu ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 147

**Kufuta Ada Vyuo vya Ufundi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta ada za Vyuo vya Ufundi hususani *VETA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa vijana wengi wa Kitanzania katika maeneo yao kwa lengo la kuwawezesha kupata ujuzi utakaowawezesha au kuwasaidia kujiajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha hilo, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanaotamani kupata mafunzo haya, wanayapata kwa gharama nafuu. Kwa sasa mwanafunzi wa bweni analipa ada ya shilingi 120,000 badala ya gharama halisi ya shilingi 860,000 wakati mwanafunzi wa kutwa analipa ada ya shilingi 60,000 badala ya shilingi 300,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupunguza gharama za upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kadiri uchumi wa nchi na mapato ya Serikali yatakavyoendelea kuimarika. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Kwa kuwa mafunzo ya *VETA* yamekuwa ni mkombozi kwa vijana waliokosa kuendelea na masomo ya juu na kwa wale wasikuwa na ajira, kwa nini, Serikali isiondoe mzigo huu wa ada kwa hawa wanyonge?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, wenye nia ya kupata mafunzo haya wanapata mafunzo haya bila kubugudhiwa licha ya kuwa wamekosa ada?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza kwa pamoja ya Mheshimiwa Mchungahela kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi ni kwamba, tumeweza kutoa ruzuku kwenye mafunzo haya na kupunguza ada kwa kiasi kikubwa, lakini kwa vile Mheshimiwa Mbunge anatoa ushauri kwamba tuendelee kupunguza, basi kwanza nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ukipitia rejea ya Bodi ya Mikopo ambayo mwanzoni ilikuwa inatoa tu kwa elimu ya juu, lakini kwa sasa tumeanza kushuka kwenda kwenye elimu ya kati, kwa hiyo, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata elimu kwa utaratibu wowote ule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaangalia ushauri wake wa kwamba, je, ifutwe au tuipeleke kwenye ule utaratibu wa Bodi ya Mikopo na hawa wanafunzi wasiojiweza kwenye maeneo haya

ya ufundi stadi, ili waweze kupata mikopo na waweze kuendelea na elimu yao. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Naleta matangazo niliyonayo hapa mbele.

Kwanza ni tangazo la wageni na tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika, wapo wageni watano ambao ni wageni wangu na hawa ni Wabunge kutoka Bunge la Malawi, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa tutaanza na Mheshimiwa Patrick Siabonga Bandawe, huyu ndiye kiongozi wa msafara. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Chimwemwe Chipungu ambaye ni Mjumbe; yupo Mheshimiwa Karim Iliyas Younos Abdul – Mjumbe; Mheshimiwa Chatima Raymond Sikelela - Mjumbe; pia wameongozana na Bi. Isabel Tambala ambaye ni Afisa Dawati Msaidizi wa *CPA*, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa pamoja na kwamba Malawi ni majirani zetu, lakini ni wachache sana wanaozungumza Kiswahili. Walivyokuwa wanapunga mikono nimeamini kwamba wameelewa. Kwa hiyo, hawahitaji niwatambulishe kwa Kiingereza. Karibuni sana Bungeni na tunafurahi sana kuwapokea hapa, naamini tutapata nafasi ya kujifunza kutoka kwa kila mmoja wenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni sita wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na hawa ni viongozi wakuu kutoka Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Tutaanza na Dkt. Tausi Kida ambaye ni Katibu Mkuu, yupo Ndugu Lawrance Mafuru ambaye ni Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, tunaye Ndugu Charles Itembe ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA*, pia yupo Ndugu Giliead Terl, Mkurugenzi Mtendaji. *(Makofi)*

Vilevile wameongozana na Ndugu Nehemia Mchechu ambaye ni Msajili wa Hazina, Dkt. Majaliwa Marwa yeye ni *UNFPA Assistant Representative,* yupo Ndugu Samweli Kilua - *Country Director Gatsby Africa* wameongozana pia na Ndugu Evance Siangicha - *UN Resident Office on behalf of the UN Resident Coordinator,* karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 12 kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar na hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, yupo Mheshimiwa Mwanaisha Hamis Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Dkt. Sudi Nahoda Hassan ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati; Mheshimiwa Asha Abdallah Mussa, Mjumbe na Mheshimiwa Mohamed Mgaza Jecha, Mjumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja nao ni Mheshimiwa Profesa Omar Fakih Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Rukia Omar Ramadhan, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Masoud Makame, Mjumbe; Mheshimiwa Yusuph Hassan Iddi, Mjumbe; Ndugu Asha Said Mohamed, Katibu wa Kamati; Ndugu Husna Rajab Othman, Katibu wa Kamati; na Ndugu Shaib Fadhil Shaib, Katibu Kamati, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria na hawa ni Mheshimiwa Dauglas Foo, Balozi wa Singapore nchini Tanzania mwenye makazi yake Singapore. *(Makofi)*

Sasa sijajua ni maelezo hapa ndiyo yamechanganya mambo ama vipi, lakini huyu ni Balozi wa Singapore nchini Tanzania, lakini hapa imeandikwa makazi yake tena Singapore? Huyu ni Balozi wa Singapore hapa nchini, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia, yupo Ndugu Suleiman Magoma, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ndugu Tham Wen Long, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Singapore; Ndugu Abdulrahman Mshamu, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Huduma za Sheria kwa Umma; na Ndugu Lucy Dinganyeck, Wakili wa Serikali Idara ya Haki za Binadamu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali ambao ni wageni wenu na wengine wamekuja kwa ajili ya mafunzo.

Tutaanza na mgeni wa Mheshimiwa David Kihenzile ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi, ni *Project Officer-Nourish Africa* kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Masache Kasaka, Mwenyekiti wa Wazee kutoka Wilaya ya Chunya, karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni viongozi wa taasisi ya *Youth Success Foundation* kutoka Dar es Salaam, karibuni sana.

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni rafiki zake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni Makatibu Kata na Waenezi kutoka Geita Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Eric Shigongo ambao ni ndugu zake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho na hawa ni Wanakwaya wa *MACC* wa Kanisa la Anglikana kutoka Musoma, Mkoa wa Mara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wanafunzi 100 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Bihawana ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi 32 wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Ndugu Masanja Bundala Antony, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Umoja wa Vijana 65 wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Tawi la SUA, Mkoa wa Morogoro na mwisho ni wanafunzi 30 wa Chuo cha Takwimu kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao, lakini lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu inawaalika katika Maadhimisho ya Sherehe ya Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho hayo yatafanyika tarehe 26 Aprili, 2024 Siku ya Ijumaa katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa kuhudhuria maadhimisho haya, lakini pia shughuli za michezo zitafanyika huko na huenda nanyi mkashiriki baadhi ya michezo. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu inawakaribisha sana kwenye maadhimisho haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo aje awasilishe hotuba yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni

na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo imechambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kumbukumbu sahihi za Bunge lako Tukufu, naomba hotuba yangu yote ya bajeti iliyowasilishwa Mezani itumike kama kumbukumbu *(Hansard)* za Bunge.

Mheshimiwa Spika, tumeaswa kuwa kila tunapopata fursa hatuna budi kumshukuru Mungu na kuwashukuru watu wote ambao wameleta tofauti katika maisha yetu. Ninamshukuru Mungu kwa wingi wa rehema, baraka na fadhili zake kwangu iliyoniwezesha kuwasilisha hotuba hii ya kwanza ya ofisi yangu na kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utulivu na hekima za uongozi ambazo Mwenyezi Mungu amemjalia pamoja na juhudi zake za dhati alizoziweka katika kuendeleza nchi yetu ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa muktadha wa majukumu ya ofisi yangu, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha Diplomasia ya Uchumi iliyochochea kuongezeka kwa ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi mbalimbali rafiki, kuboresha mazingira ya uwekezaji, na kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahali salama katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na jitihada zake kubwa anazozifanya katika kujenga Zanzibar yenye maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanazofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza nchi yetu vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kuwasilisha bajeti zao na kupata ridhaa ya Bunge lako Tukufu…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kelele zimekuwa nyingi sana. Tupunguze sauti kidogo.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi mahiri na imara wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, kwa ushirikiano, maelekezo, maono na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024 na Mapendekezo ya Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliopata heshima ya kuteuliwa na kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali katika Serikali na katika Bunge letu Tukufu. Hawa ni Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Zainab Athman Katimba kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kutoa pole kwako, kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa msiba uliolipata Bunge letu Tukufu kufuatia kufariki kwa Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Tunamwombea Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie nafasi hii kwa niaba ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zake kutoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko na majanga mengine ya asili yaliyojitokeza katika msimu huu wa mvua katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ukiwemo wewe Mheshimiwa Spika kule Mbeya Mjini na tumekuona ukihudumia wananchi wetu. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nifanye Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina liliidhinishiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi trilioni 1.07. Maduhuli hayo yanatokana na gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi ya taasisi zinazochangia, mrejesho wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania, rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2024 ofisi ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 459.44 sawa na 43% ya lengo la mwaka. Matarajio ni kwamba sehemu kubwa ya makusanyo itapatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 mafungu matatu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Msajili wa Hazina na Tume ya Mipango yaliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 126.19

kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2024 mafungu haya matatu yamepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 68.08 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo sawa na 54% ya kiasi kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nifanye mapitio ya baadhi ya *program,* miradi na kazi ambazo zilitekelezwa katika mwaka 2023/2024. Kwa kuzingatia kuwa muda wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 unakamilika mwakani, Serikali ilianza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Maandalizi ya Dira hii yanaendelea vizuri na rasimu ya kwanza ya Dira mpya inatarajiwa kupatikana ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) maarufu kama *Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*. Mpango huu unalenga kuondoa vikwazo vya kufanya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, mpango huu unatekelezwa na Wizara zote za kisekta na Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi ukiratibiwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Kitengo cha Maboresho na Mazingira ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, mpango unahusisha mapitio ya sheria, kanuni na taratibu kuondoa mwingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi za umma, ujenzi wa mifumo ya kielektroniki na kuimarisha uwezo wa idara za viwanda biashara na uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022 Serikali iliajiri mtaalamu mwelekezi kufanya tathmini ya utekelezaji wa MKUMBI ili kubaini hatua iliyofikiwa na changamoto zilizojitokeza katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Taarifa ya tathmini hiyo imehuishwa mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, taarifa ya tathmini hiyo imebaini mafanikio yafuatayo katika uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji nchini: -

(i) Tozo, ada na faini 374 zilizobainika kukwaza uanzishaji wa biashara na uwekezaji zilifutwa zikihusisha taasisi mbalimbali zikiwemo: *TBS, TMDA*, Bodi ya Sukari Tanzania, *OSHA*, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Jeshi la Zimamoto;

(ii) Kuunganisha mamlaka za urekebu ambazo majukumu yake yalionekana kuingiliana. Kwa mfano, majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* yalihamishiwa katika Taasisi ya Viwango (*TBS*). Aidha, majukumu ya kutoa vibali vya kusafirisha kemikali yalihamishwa kwenda Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na hivyo kuondoa mwingiliano uliokuwepo miongoni mwa Taasisi hii na *TMDA* pamoja na *TANROADS*.

Vilevile, Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* Sura ya 415 ilirekebishwa ili kuondoa haki pekee ya uondoaji na usafirishaji wa mizigo na shehena kwa njia ya maji. *TASAC* sasa inahusika na bidhaa nne peke yake ambazo ni makinikia, wanyama hai, kemikali zinazotumika migodini pamoja na nyaraka za Serikali;

(iii) Ujenzi wa mifumo ya elektroniki 42 kupitia Wizara na taasisi mbalimbali ambao umeboreshwa utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara; na

(iv) Kupungua kwa idadi ya siku za kupata huduma kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla. Kwa mfano, muda wa kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Mpaka wa Tunduma umepungua kutoka siku saba hadi siku tatu; muda wa kupata usajili wa sehemu za kazi umepungua kutoka siku 14 hadi siku moja; na muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi umepungua kutoka siku 14 hadi siku tatu na siku saba.

Mheshimiwa Spika, majukumu mengine yanayotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mipango katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:-

(i) Kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025 ambao utawasilishwa hapa Bungeni pamoja na Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ifikapo mnano 13 Juni, 2024;

(ii) Katika kuweka mfumo imara wa kusimamia uwekezaji wa sekta ya umma, Serikali iliandaa Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma. Muswada umeshasomwa Mara ya Kwanza na taratibu za Kusomwa kwa Mara ya Pili zinaendelea kukamilishwa;

(iii) Kufanya tathmini ya utendaji wa Mashirika ya Umma;

(iv) Kuanzisha Mfumo wa Elektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji *(Tanzania Electronic Investment Window)*; na

(v) Kuhamasisha uwekezaji ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia falsafa ya kuifungua nchi inayolenga kuimarisha na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, Serikali imeendelea kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji nchini kutoka ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuongeza wigo wa shughuli za kiuchumi nchini kupitia uwekezaji mpya na kulinda uwekezaji uliopo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie baadhi ya mafanikio katika sekta ya uwekezaji. Mafanikio haya hupimwa kwa kuzingatia vigezo vikubwa vitatu: -

(i) Idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa;

(ii) Kiwango cha ajira kinachozalishwa; na

(iii) Kiwango cha mtaji kinachoingia nchini ikiwemo mtaji kutoka nje *(Foreign Direct Investment - FDI)*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kilisajili jumla ya miradi mipya 509 sawa na ongezeko la 112% ikilinganishwa na miradi 240 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Miradi hiyo inatarajiwa kuwekeza jumla ya dola za Kimarekani bilioni 4.5 na kutengeneza ajira 229,282.

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi ambayo ni ya Watanzania ni 196 sawa na 38.5%, wageni 214 sawa na 42% na miradi ya ubia kati ya Watanzania na wageni 99 sawa na 19.5%.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 katika kipindi cha miaka minne (mwaka 2020 mpaka 2023) *TIC* ilisajili miradi 1,282 iliyotarajiwa kuajiri jumla ya watu 248,309 na kuingiza mtaji wa jumla ya dola za Kimarekani bilioni 15.1.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita jumla ya miradi 1,004 imesajiliwa katika sekta mbalimbali. Sekta tano zinazoongoza katika kusajili miradi ni uzalishaji viwandani 45%, usafiri na usafirishaji 18%, utalii asilimia tisa, kilimo asilimia tisa na huduma asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, idadi ya miradi kiwango cha mtaji na ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji katika kituo cha *TIC* imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, idadi ya miradi iliongezeka kutoka miradi 207 mwaka 2000 hadi kufikia miradi 526 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha mitaji inayotokana na miradi ya uwekezaji kilipanda kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.09 mwaka 2020 hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni 5.7 mwaka 2023. Aidha, idadi ya ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka ajira 17,385 mwaka 2020 hadi ajira 137,010 mwaka 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihitimishe eneo hili kwa kutoa taarifa kuwa Serikali inaendelea na majadiliano ya kimkataba na kampuni zinazotarajia kuwekeza katika Mradi wa Gesi Asilia *(Liquefied Natural Gas - LNG)*. Mradi huu utahusisha ubadilishaji wa gesi asilia kutoka hali ya hewa na kuwa kimiminika.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha gesi kilichogundulika baharini ni futi za ujazo trilioni 45.13 katika vitalu Na. 1, Na. 2, na Na. 4. Aidha, gesi iliyothibitishwa kuvunwa kwa ajili ya mradi huu ni kiasi cha futi za ujazo trilioni 25. Thamani ya uwekezaji inayotarajiwa

kufanyika katika mradi huu ni dola za Kimarekani bilioni 42, sawa shilingi trilioni 109.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuchochea kasi ya ukuaji uchumi, kuongeza ajira nchini, kuingiza mtaji mkubwa kutoka nje *(FDI),* kuchochea ujenzi wa viwanda vinavyotumia gesi asilia kama malighafi na kupanua shughuli za kiuchumi na kijamii nchini, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuona kwamba majadiliano yanakamilika mapema iwezekanavyo ili utekelezaji wa mradi huu muhimu uanze.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Taasisi zake kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ni kuleta mapinduzi ya uchumi kwa maendeleo ya watu. Moja ya nyenzo muhimu ya kuleta mapinduzi ya uchumi iliyoainishwa katika Ilani hiyo ni kuwa na mipango endelevu ya maendeleo, kuchochea uwekezaji, kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini na kuimarisha uendeshaji wa Mashirika ya Umma ili yachangie kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo haya, lengo kuu litakaloongoza Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/2025 ni kuratibu mipango thabiti inayolenga kuleta maendeleo endelevu na jumuishi kwa wananchi, kuvutia uwekezaji wenye tija kwa Taifa, uboreshaji wa mazingira ya biashara na uendeshaji wenye tija wa Mashirika, na Taasisi za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufikia lengo hili, programu, miradi na kazi zitakazotekelezwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji zimezingatia vipaumbele kumi vifuatavyo: -

(i) Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2025;

(ii) Kukamilisha uandaaji wa sera mpya ya uwekezaji na mkakati wake wa utekelezaji;

(iii) Kukamilisha kuunganisha Taasisi za Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)* na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje *(EPZA)* na kuanzisha taasisi mpya ya kusimamia masuala ya uwekezaji wa sekta binafsi;

(iv) Kukamilisha Mwongozo wa Ujenzi na Uendeshaji wa Kongani za Viwanda nchini;

(v) Kufanya tathmini kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi *(Special Economic Zones)*;

(vi) Kufanya mapitio ya sheria zinazohusu masuala ya madini, ardhi, kilimo, utalii na biashara kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika maeneo hayo;

(vii) Kukamilisha kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake;

(viii) Kuanza utekelezaji wa Mradi wa Kielelezo wa Kanda Maalum wa Kiuchumi Bagamoyo *(Bagamoyo Special Economic Zone)* kwa kuzingatia mpango kabambe wa mwaka 2024;

(ix) Kuanzisha mashindano ya jinsi Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinavyovutia uwekezaji na kuweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara; na

(x) Kuhuisha mpango wa maboresho ya mazingira ya biashara na uwekezaji utakaoainisha changamoto mpya ya uwekezaji na biashara nchini na namna ya kuzishughulikia changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele na kazi ambazo nimeziainisha katika hotuba yangu, naliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 121,329,199,000, ikiwemo shilingi 100,246,191,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 21,083,008,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2024/2025 kwa mgawanyo ufuatao kwa kila fungu: -

(i) Fungu 11 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tunaomba kuidhinishiwa shilingi 30,030,502,000;

(ii) Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, tunaomba kuidhinishiwa shilingi 45,077,067,000;

(iii) Fungu 06 - Tume ya Mipango, tunaomba kuidhinishiwa shilingi 46,221,630,000; na

Mheshimiwa Spika, jumla kuu kama nilivyosema tunaomba kuidhinishiwa shilingi 121,329,199,000.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu. Hawa ni pamoja na Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Ndugu Lawrence Nyasebwa Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina; Ndugu Charles Jackson Itembe, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka na Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje *(EPZA);* na Ndugu Gilead John Teri, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Nchini *(TIC)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru *Management* na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda kuwashukuru sana viongozi wa sekta binafsi kwa kusimamia vyema sekta binafsi ambayo ndiyo *engine* ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na kwa ushirikiano wao wa karibu na Serikali katika kukamilisha uwekezaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwataje angalau wachache kuwakilisha wenzao. Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini *(TPSF),* Umoja wa Ulaya *(European Union),* Benki ya Dunia, *UNIDO, Trade Mark Africa, UNDP, UNFPA* na wadau wengine wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa pekee kabisa, nawashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia

kwa juhudi na maarifa ili kuhakikisha kuwa Jimbo letu la Ubungo linaendelea kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Ubungo na Mkoa wa Dar es Salaam kwa malezi na ushirikiano tulionao katika kutekeleza Ilani ya CCM na baadhi yao leo wapo hapa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hii ni bajeti ya kwanza ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia mpango na bajeti niliyoiwasilisha. Viongozi na watumishi wote wa ofisi hii na taasisi tunazozisimamia tumejipanga vyema katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango endelevu ya maendeleo ya nchi yetu kuhakikisha kuwa fursa za uwekezaji zinaendelea kupanuka na kuwanufaisha Watanzania wote katika kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanaendeshwa kwa ufanisi na tija na kwamba yanachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, matokeo muhimu tarajiwa ya utekelezaji wa mpango na bajeti hii ni kukamilika kwa Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo, kupanuka kwa fursa za uwekezaji nchini na kuimarika kwa utendaji na tija ya mashirika ya umma katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa dhima tuliyoweka kama Taifa kupitia mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026 na kwa uimara wa Chama Cha Mapinduzi katika kuiongoza nchi yetu na kwa unyenyekevu, ushupavu, uzalendo, weledi na uchapakazi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa mapenzi mema ambayo Mungu anayo juu ya Taifa letu la Tanzania na kwa kuwa nia tunayo na uwezo tunao na kupitia Bunge hili mahiri na imara sana, chini ya uongozi wako makini kabisa; tunayo imani kubwa kuwa, kwa ushirikiano wa Bunge lako Tukufu tunaenda kuleta mapinduzi ya uchumi kupitia mipango thabiti na endelevu na kuendelea kupanua na kuimarika kwa fursa za uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, ninapomalizia, naomba tena Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na

Matumizi ya shilingi 121,329,199,000 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENIMAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI TA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka 2023/24 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (Fungu 11); Ofisi ya Msajili wa Hazina (Fungu 07); na Tume ya Mipango (Fungu 66) kwa Mwaka 2024/25.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema iliyoniwezesha kuwasilisha Hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (OR-MU). Aidha, ninamshukuru Mungu kwa kulijalia Taifa letu amani, utulivu na mshikamano na kwa kutuwezesha kukutana katika mkutano huu wa 15 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa kupitia Bajeti zinazowasilishwa katika Bunge hili la Bajeti.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, waheshimiwa wabunge na wananchi wote kwa ujumla kwa msiba uliolipata Bunge kufuatia kufariki kwa ***Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil***, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Tunamuombea Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina! Aidha, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Mipango na

Uwekezaji na taasisi za umma inazozisimamia kutoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na mafuriko yaliyojitokeza katika msimu huu wa mvua katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**4.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa, ninapenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, pamoja na juhudi za dhati alizoziweka katika kuiendeleza nchi yetu ili tuweze kufikia malengo tuliojiwekea. Kipekee, na kwa muktadha wa majukumu ya Ofisi yangu, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha diplomasia ya uchumi iliyochochea kuongezeka kwa mashirikiano baina ya nchi yetu na nchi mbalimbali rafiki, kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuitangaza nchi yetu kuwa kivutio na mahala salama katika uwekezaji. Aidha, ninamshukuru **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na jitihada zake kubwa katika kuendelea kuijenga Zanzibar yenye maendeleo makubwa.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwapongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kazi kubwa wanazofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuendesha nchi yetu vyema.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi mahiri na imara wa Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama**, Mbunge wa Jimbo la Madaba na Makamu wake **Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo**, Mbunge wa Jimbo la Nkenge, kwa ushirikiano, maelekezo, maoni na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/25.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza waheshimiwa wabunge waliopata heshima ya kuteuliwa na kuchaguliwa kushika nafasi mbalimbali katika Serikali na Bunge letu tukufu. Hawa ni:

**Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), **Mheshimiwa Zainabu Athuman Katimba (Mb)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa **(OR-TAMISEMI)** na **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama**, Mbunge wa Jimbo la Madaba, na **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika**, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji, kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yetu na kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii. Hawa ni pamoja na Dkt. Tausi Mbaga Kida (Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji), Ndugu Lawrence Nyasebwa Mafuru (Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango), Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu (Msajili wa Hazina), Ndugu Charles Jackson Itembe (Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje), na Ndugu Gilead John Teri (Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania). Aidha, ninawashukuru Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa umuhimu wa pekee kabisa, ninawashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Ubungo kwa kuendelea kunipa ushirikiano na imani wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Ninaahidi kuendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuhakikisha jimbo letu linaendelea kupata maendeleo.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na utangulizi nilioutoa hapo juu, Hotuba yangu ina sehemu kuu tatu: Majikumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Taarifa ya Utekelezaji wa kazi zilizofanyika kwa Mwaka 2023/24; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25.

## 2. MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali namba 407 (A na B) la tarehe 22 Juni, 2023. Ofisi hii ina jukumu la msingi la kuandaa na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati inayohusu mipango ya maendeleo ya Taifa, uwekezaji, kusimamia utendaji wa mashirika ya umma, na kuratibu utekelezaji wa mikakati ya kuboresha mazingira ya biashara nchini.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, Majukumu mahususi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni haya yafuatayo:-

(i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera kuhusu Mipango na Uwekezaji nchini;

(ii) Kuratibu na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi;

(iii) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara;

(iv) Kuratibu taasisi za kitaifa na kimataifa zinazohusika na uwekezaji; na

(v) Kuzisimamia taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambazo ni Tume ya Mipango, Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH), Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA) na Kituo cha Uwezekezaji Tanzania (TIC).

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Machi 2024, Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji ina jumla ya watumishi 80 katika taaluma na kada mbalimbali waliogawanywa kufanya kazi katika idara nne na vitengo saba.

## 3. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

### 3.1. MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI HADI MACHI, 2024 (FUNGU 11, FUNGU 07 NA FUNGU 66)

#### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa kukusanya maduhuli yenye jumla

ya **shilingi trilioni 1.07.** Maduhuli hayo yanatokana na gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya taasisi zinazochangia, mrejesho wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS), rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **shilingi bilioni 459.44** sawa na **asilimia 74.11** ya lengo la kukusanya **shilingi bilioni 619.96** kwa kipindi kinachorejewa zilikusanywa, sawa na **asilimia 42.96** ya lengo la mwaka. Matarajio ni kuwa sehemu kubwa ya makusanyo itapatikana katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2023/24.

### 3.1.2 Bajeti iliyoidhinishwa

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mafungu matatu (3) ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yaliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 126.19** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi bilioni 15.61** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na **shilingi bilioni 79.90** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi bilioni 30.69** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 3.1.2 Matumizi

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, mafungu matatu (3) ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji yamepokea na kutumia jumla ya **shilingi bilioni 68.08** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 53.95** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kati ya kiasi kilichopokelewa, **shilingi bilioni 8.48** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi** bilioni **41.83** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi bilioni 17.76** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## 3.2. MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2023/24

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa mafungu matatu (3) ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni kama ifuatavyo: -

**i) Kuandaa Dira 2050 na Mpango Mkakati wa Muda Mrefu**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ajenda ya Maendeleo ya Taifa imefafanuliwa na inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo utekelezaji wake utafika ukomo Juni, 2026. Kwa msingi huo, Serikali imeanza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ambayo inatarajiwa kutoa mwongozo na mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka 25.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024 shughuli zifuatazo zimefanyika katika maandalizi ya Dira:

(i) Kuundwa kwa Kamati Kuu ya Kitaifa ya Dira pamoja na Timu Kuu ya Kitaalam ya Dira yenye wajumbe 23 katika fani, uzoefu na ujuzi mbalimbali kutoka Serikalini, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia (AZAKI), Taasisi za Elimu na Tafiti;

(ii) Kufanyika kwa Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 tarehe 9 Desemba, 2023 ambapo mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika mkutano huo nyenzo na mbinu za ushirikishaji wadau na ukusanyaji wa maoni zilizinduliwa na kukabidhiwa kwa Timu Kuu ya Wataalam wa Dira 2050;

(iii) Kufanyika kwa kikao cha kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Dira 2050 chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambacho kilitoa mwongozo mahsusi kuhusu mwelekeo wa maandalizi ya Dira 2050;

(iv) Kufanyika kwa semina elekezi na mafunzo mbalimbali kwa Timu Kuu ya Kitaalam ya Dira 2050, viongozi mbalimbali wa Serikali na Mameneja Takwimu wa Mikoa yote 31 na Makarani 132 wa Dira 2050 katika Mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar;

(v) Kuandaliwa na kuidhinishwa kwa miongozo ya usimamizi na uratibu wa maandalizi ya Dira ikiwemo Mwongozo wa Usimamizi wa Maandalizi ya Dira 2050 na Mwongozo wa Ushirikishwaji Wadau katika Maandalizi ya Dira 2050;

(vi) Kuanza kwa ukusanyaji wa maoni kuhusu Dira 2050 kupitia makundi mbalimbali yakiwemo: (i) Taasisi za kidini - Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza la Kikristo Tanzania (CCT), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA); (ii) Asasi za Kiraia (AZAKI) zinazoratibiwa na Foundation for Civil Society (FCS); (iii) Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); (iv) Kongamano la mwaka la Jukwaa la Wahariri Tanzania (Tanzania Editors Forum-TEF); na (v) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF); na

(vii) Kufanyika kwa semina ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurungenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu zoezi la ukusanyaji wa maoni ya wananchi na wadau kuhusu Dira 2050.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wananchi na wadau ambapo hadi kufikia tarehe 16 Aprili, 2024 jumla ya watu **623,914** wametoa maoni kupitia simu za mkononi, **7,067** wametoa maoni kupitia tovuti na 590 katika ngazi ya kaya kupitia mahojiano ya ana kwa ana yanayofanywa na makarani wa Dira 2050 katika mikoa yote nchini na hivyo kufanya jumla ya washiriki **631,571** wametoa maoni.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya wananchi 631,571 waliotoa maoni kupitia simu za mikononi na tovuti, asilimia 70 ni wanaume na asilimia 30 ni wanawake. Aidha, asilimia 80 ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35. Tunawapongeza na kuwashukuru sana vijana wengi kujitokeza kutoa maoni yao kuhusu mustakabali wa nchi yao katika miaka 25 au zaidi ijayo.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuhamasisha wapiga kura wetu na wananchi wote kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi kushiriki kutoa maoni kwa wajumbe wa Timu ya Dira watakaopita katika maeneo yao. Aidha, maoni yanaweza kutolewa kupitia njia ya simu za mkononi kwa kupiga ***152*00#** au kupitia tovuti *www.dira2050portal.planning.go.tz.*

### ii) Tathmini ya Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya awali ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inaonesha kuwa, pamoja na changamoto zilizojitokeza, mafanikio makubwa yamepatikana katika utekelezaji wa dira hiyo, katika nyanja za uchumi, huduma za jamii, nishati, ujenzi wa miundombinu, n.k. Taarifa kamili ya matokeo ya tathmini ya Dira 2025 inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji *www.planninginvestment.go.tz.*

### iii) Kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea na uratibu wa maandalizi ya mipango ya maendeleo ikiwa ni takwa la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 63(3)(c), Sheria ya Tume ya Mipango ya mwaka 2023 Kifungu cha 6(2)(b) na Sheria ya Bajeti, Sura 439 Kifungu cha 11 vinavyoitaka Serikali kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kila mwaka. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 umejikita katika kuendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambao unachochea mageuzi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu kupitia viwanda.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taarifa kamili ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 itatolewa wakati wa kusoma bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa tarehe 13 Juni 2024.

### iv) Uendelezaji wa kada za Wanamipango

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Mipango imekasimiwa jukumu la kuendeleza kada za wanamipango pamoja na kuratibu makongamano ya wadau mbalimbali kwa ajili ya kujadili masuala ya mipango ya maendeleo. Mwelekeo ni kulea na kuendeleza kada ya wanamipango na kuwa na usajili rasmi wa wanamipango. Katika kutekeleza jukumu hilo, mwaka 2023/24, Tume iliandaa kongamano la wanamipango nchini lililofanyika Jijini Arusha ambalo lilikuwa na kauli mbiu "*Fikra za pamoja na*

*utekelezaji, ulioratibiwa kwa ustawi jumuishi*". Jumla ya wanamipango 747 kutoka katika Wizara, Idara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa walishiriki.

**v) Kuandaa Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea na maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma. Lengo la Muswada huo ni kuweka mfumo wa kisheria na muundo wa kitaasisi utakaochagiza mashirika na taaisisi za umma kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi. Aidha, sheria hii itaanzisha chombo cha usimamizi wa mashirika ya umma na kuanzisha mfuko wa taifa wa uwekezaji kwa lengo la kuwa na chanzo endelevu cha mitaji kwa ajili ya uwekezaji wa umma.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2024, Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2023 umekamilika na kusomwa kwa mara ya kwanza kwenye Mkutano wa 14 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada huo uliwasilishwa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) Januari, 2024 kwa ajili ya kuchambuliwa pamoja na kukusanya maoni ya wadau. Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuchambua Muswada na kuratibu maoni ya wadau. Kwa sasa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inafanyia kazi maoni ya Kamati na wadau yaliyowasilishwa na kuboresha Muswada ili uweze kuwasilishwa kwa mara ya pili katika Bunge lako tukufu mapema iwezekanavyo.

**vi) Kusimamia Maboresho ya Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2020 iliielekeza Serikali, pamoja na mambo mengine, **"*kuimarisha mashirika ya umma ili yaweze kuendelea kutoa michango katika maendeleo ya Taifa*"**. Aidha, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kupitia hotuba yake Bungeni ya tarehe 22 Aprili 2022 alielekeza, pamoja na mambo mengine, ***"kufanya mapitio na uchambuzi wa kina wa uendeshaji wa Mashirika ya Umma, tukiwa na lengo la kuyafanya yaweze kujiendesha kwa faida"***. Vile vile, kupitia falsafa ya 4R, pamoja na hatua zingine, Mheshimiwa Rais alitangaza kufanya mageuzi makubwa katika uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maagizo hayo, mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, ilipanga kufanya tathmini ya utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma ili kubainisha changamoto za kiutendaji na kupendekeza hatua za kuchukua katika kuongeza tija katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Hadi Machi 2024, tathmini ya kina kuhusu utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma 248 imefanyika. Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hiyo, Serikali imefanya maamuzi ya kuunganisha Taasisi na Mashirika ya Umma 14; na kufuta Taasisi na Mashirika ya Umma matatu (3). Aidha, katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Maelekezo ya Chama Tawala CCM, Serikali kupitia, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeandaa Mwongozo wa Masuala ya Kuzingatia katika Kuunganisha au Kufuta Taasisi za Umma ambao umesambazwa katika Wizara zinazohusika kwa ajili ya utekelezaji. Vilevile, Wizara za Kisekta ambazo Taasisi zinazounganishwa au kufutwa zipo chini yake zimeunda Kamati za Wataalam ambazo zinaendelea na utekelezaji wa zoezi la kuunganisha au kufuta Taasisi husika.

### vii) Usimamizi wa utendaji wa mashirika ya Umma

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** **katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuzisimamia kwa karibu Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisi y Msajili wa Hazina imehuisha Mwongozo wa kuandaa Miongozo ya Uendeshaji washughuli za Bodi za Taasisi *(Board Charter Guideline)* pamoja na mwongozo wa tathmini ya Utendaji wa Bodi*(Board Evaluation Guide),* imeandaa Mwongozo wa Utawala Bora *(Corporate Govarnance Guideline)* na Mwongozo wa majukumu ya Bodi za Taasisi, Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali. Aidha, imefanya tathmini ya utendajikazi wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika 63 kati

ya lengo la mashirika 70 kwa mwaka 2023/24. Kati ya tathmini hizo 18 zimefanywa kwa mfumo wa kidigitali ikiwa ni mwanzo wa kufanya tathmni hizo kwa mfumo wa kieleketroniki ambao unatumiwa na nchi nyingi zilizoendelea duniani. Matokeo ya miongozo na tathmini hizi yanalenga kuongeza ufanisi wa utoaji huduma zenye ubora, tija na kwa wakati kwa walengwa na kuongeza utendaji na uwajibikaji wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma.

**32.** Vilevile, Ofisi ya Msajli wa Hazina imefanya mapitio ya kiolezo (template) cha Mikataba ya Utendaji Kazi ikiwa ni pamoja na kuboresha Viashiria vya Upimaji, kutoa mafunzo kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu kiolezo hicho. Viashiria vipya vya upimaji vimeandaliwa kwa kuzingatia sekta na vimetenganisha mashirika ya kibiashara na yale yasiyo ya biashara.

**viii) Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Shughuli za Taasisi na Mashirika ya Umma – *Dashboard***

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Serikali inajenga mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Mfumo huo utaimarisha usimamizi kwa kubainisha vigezo vya kupima utendaji hususan kigezo cha utendaji wa kifedha na vigezo vingine kama utawala bora, huduma kwa wateja na usimamizi wa rasilimali watu.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo huo utatumika kutoa taarifa mbalimbali ikiwemo mapato, muundo na utendaji wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya Umma, Tathmini ya utendaji kwenye Taasisi, mikataba ya utendaji kazi ambayo imekuwa ikiingiwa kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Bodi za Wakurugenzi. Hadi kufikia Machi, 2024 ujenzi wa Mfumo huo umefikia asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika katika Mwaka 2024/25.

**ix) Kuandaa Mwongozo wa Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi Kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma yapatayo 248 na hivyo kama

mwekezaji mwingine yoyote, Serikali inatarajia kupata rejesho la uwekezaji wake katika Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa njia ya gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya taasisi zinazochangia, rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo ikiwemo mapato yatokanayo na mrejesho wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS). Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuchangia kiasi kidogo cha mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali ukilinganisha na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali.

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Msajli wa Hazina imeandaa Mwongozo wa Ukusanyaji wa Mapato Yasiyo ya Kodi wa Mwaka 2023. Mwongozo huo unaweka utaratibu wa ulipaji wa gawio na uchangiaji wa michango kwa kuzingatia vigezo vya uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutoka Taasisi na Mashirika ya Umma.

**x) Kuratibu Uwezeshaji na Kujenga Uwezo kwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika ya Umma**

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kunakuwa na utendaji wenye ufanisi, tija na utawala bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma, kuna umuhimu mkubwa wa kuwawezesha na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika ya Umma, sambamba na kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanakuwa na Bodi hai za Wakurugenzi muda wote.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Msajili wa Hazina iliratibu Kikao Kazi cha Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kilichozinduliwa na Mheshimiwa Rais na kufanyika tarehe 19 hadi 21 Agosti, 2023 Jijini Arusha. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Chuo cha Uongozi iliratibu mafunzo kwa Wajumbe 136 wa Bodi za wakurugenzi kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma 14 pamoja na Kikao Kazi kati ya Msajili wa Hazina na Wakurugenzi wa Bodi Wanaoiwakilisha Serikali kwenye kampuni zinazomilikiwa

kwa hisa chache (Minority Interest) kilichofanyika tarehe 12 hadi 15 Machi, 2024 katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere – Kibaha mkoani Pwani.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kwamba Taasisi na Mashirika ya Umma yanakuwa na Bodi hai za Wakurugenzi, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeanzisha moduli ya *Board Management* kwenye mfumo wa *Office of the Treasury Registrar Management Information System* (OTRMIS) ambao unatumika kuhifadhi taarifa za Bodi za Wakurugenzi katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, mfumo huo unatoa taarifa kwa mamlaka za uteuzi kuhusu Bodi zilizo hai, zinazokaribia kumaliza muda wake na zisizotimiza akidi ya Wajumbe. Uwepo wa Mfumo huo umeleta mafanikio makubwa ya kupunguza idadi ya Mashirika ya Umma yasiyokuwa na Bodi hai za Wakurugenzi kutoka Mashirika 52 Novemba, 2022 hadi Mashirika saba (7) Machi, 2024.

**xi) Kuandaa Sera Mpya ya Uwekezaji na Mkakati wake**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji ya mwaka 1996 na kuandaa rasimu ya sera mpya ya Taifa ya uwekezaji ambayo imezingatia mazingira ya sasa ya uwekezaji na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 na mabadiliko mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi na kiteknolojia.

**xii) Kuhamasisha Uwekezaji Ndani na kutoka Nje ya Nchi**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ilipanga kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Machi, 2024, Ofisi pamoja na taasisi zake za TIC na EPZA imeshiriki makongamano ya uwekezaji nane (8) yaliyofanyika nje ya nchi wakati wa ziara za viongozi wakuu kwenye nchi za Morocco, Qatar, India, Italia, Zambia, Indonesia, Saudi Arabia na Norway. Vilevile, Ofisi imeratibu ziara maalum za kunadi fursa za uwekezaji na biashara katika nchi za China, Ivory Coast na Uholanzi. Aidha, Ofisi imeratibu na kushiriki mikutano na makongamano ya ndani ya nchi yaliyofanyika katika mikoa 17 na maandalizi kwa mikoa

mingine yanaendelea. Jitihada hizo zimeimarisha hamasa ya kuwekeza nchini kama ilivyoainishwa hapo juu.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya kulinda na kukuza Uwekezaji (*Bilateral Investment Treaties*-BITs) inayohusisha nchi za Canada, India, Indonesia, Iran, Korea, Qatar na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Aidha, Ofisi imefanya mapitio na uchambuzi wa Mikataba yote ya Kimataifa ya kulinda na kukuza Uwekezaji (BITs) iliyosainiwa na nchi ili kufahamu hali ya utekelezaji na kupendekeza Mkataba Kifani (Model BIT) wa nchi utakaotoa mwongozo wa majadiliano.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) iliendesha kampeni ya kitaifa yenye lengo kuu la kuhamasisha uwekezaji wa ndani iliyobebwa na kauli mbiu "***2024 isipite bila kutekeleza mradi wako***". Kampeni hii ni endelevu na ina malengo yafuatayo: kubadili fikra na mtizamo wa kwamba TIC ni mahsusi kwa wawekezaji wa kutoka nje ya nchi na siyo kwa watanzania; kutoa elimu ya uwekezaji hususan taratibu za kusajili miradi ya uwekezaji; na kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayomilikiwa na Watanzania kwa lengo la kuwashirikisha kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Awamu ya kwanza ya kampeni hiyo imehusisha mikoa 13 ya Arusha, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Songwe na Tabora. Awamu ya pili kwa mikoa 13 iliyobaki itatekelezwa kabla ya kukamilika kwa mwaka 2024.

### xiii) Kuanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Kituo cha Uwekezaji kimekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji (Tanzania Electronic Investment Window - TeIW) kwa awamu ya kwanza ambao ulizinduliwa Septemba, 2023 na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfumo huo

umeunganishwa na mifumo ya Taasisi saba (7) ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Idara ya Uhamiaji, Idara ya Kazi, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TIC. Mfumo huo, unamwezesha mwekezaji kusajili mradi popote ndani na nje ya nchi na kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku 3 ikiwa ametimiza vigezo. Awamu ya pili ya ujenzi wa mfumo huo itahusisha uunganishaji wa Taasisi nyingine saba (7) ambazo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wizara ya Kilimo, Tume ya Madini na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

**xiv) Kuendeleza Viwanda vya Serikali vilivyokabidhiwa kwa EPZA**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2022, Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje ilikabidhiwa viwanda nane (8) vilivyokuwa vimebinafsishwa na kurejeshwa Serikalini ili kuvitafutia wawekezaji. Hadi Machi 2024, viwanda vinne (4) vimepata wawekezaji ambavyo ni: Kiwanda cha Nachingwea kilichopata mwekezaji Desemba, 2023 kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo; kiwanda cha Mafuta Ilulu kilichopata mwekezaji Machi, 2023 kwa ajili ya kuchakata mazao ya kilimo; na viwanda vya Mkata Sawmill kwa ajili ya kuchakata nyama na National Steel kilichopo Chang'ombe, Dar es salaam kwa ajili ya kutengeneza samani, vinywaji baridi na kutoa huduma ya ugavi na biashara. Mamlaka ya EPZ inaendelea kutafuta wawekezaji kwa viwanda vinne (4) vilivyobaki.

## 3.3. HALI NA MWENENDO WA UWEKEZAJI NCHINI

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia falsafa ya kuifungua nchi inayolenga kuimarisha na kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, Serikali imeendelea kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji nchini kutoka ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuongeza wigo wa shughuli za kiuchumi nchini kupitia uwekezaji mpya na kulinda uwekezaji ulipo.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika sekta ya uwekezaji hupimwa kwa kuzingatia vigezo vitatu vikubwa: **Moja:** *idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa;* **Mbili:** *kiwango cha ajira kinachozalishwa;* na **Tatu:** *kiwango cha mtaji kinachoingia katika nchi*, ikiwemo mtaji wa moja kwa moja kutoka nje (Foreign Direct Investment-FDI). Uwekezaji nchini huratibiwa na taasisi mbalimbali, zikiwemo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZA), Wizara ya Madini, na taasisi zingine za umma na sekta za binafsi kama inavyofafanuliwa hapa chini


**48.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2024, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilisajili jumla ya miradi mipya **509** sawa na ongezeko la **asilimia 112.1** ikilinganishwa na miradi **240** iliyosajiliwa kwa mwaka katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Miradi hiyo inatarajiwa kuwekeza jumla ya dola za Marekani milioni **4,490.24** na kutengeneza **ajira 229,282**. Aidha, miradi ambayo ni ya watanzania ni **196** sawa na **asilimia 38.5**, wageni **214** sawa na **asilimia 42** na miradi ya ubia wa watanzania na wageni **99** sawa na **asilimia 19.5**.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi kupitia TIC ni uzalishaji viwandani miradi **221** sawa na **asilimia 43,** usafirishaji miradi **106** sawa na asilimia **21,** utalii miradi **54** sawa na **asilimia 11**, ujenzi wa majengo ya biashara miradi **48** sawa na **asilimia 9,** kilimo miradi **43** sawa na **asilimia 8** na huduma miradi 16 sawa na **asilimia 3.** Miradi mingine **21** sawa na **asilimia 5** ipo katika sekta nyingine za miundombinu, rasilimali watu, mawasiliano ya simu, madini, mafuta na nishati kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 1*** cha hotuba hii.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hiyo inatarajiwa kuwekezwa katika mikoa ya Dar es Salaam miradi **206,** Pwani miradi **98**, Arusha miradi **32,** Dodoma miradi **19,** Mwanza miradi **18,** Tanga miradi **16** na Kilimanjaro miradi **15.** Miradi mingine **105** ipo katika mikoa mingine kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na**. **2** cha hotuba hii. Mgawanyo huu wa kimkoa unachangiwa na uwepo wa masoko na miundombinu wezeshi kama vile umeme, maji, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Hivyo, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya msingi katika mikoa

mingine na kuzishirikisha Mamlaka za Mikoa hiyo ili kupanua wigo wa uwekezaji kwa kuvutia wawekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi.


**51.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa ujumla wake, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, katika kipindi cha miaka minne, 2020-2023, TIC ilisajili miradi 1,282 iliyotarajiwa kuajiri jumla ya watu 248,309 na kuingiza jumla ya dola za Marekani milioni 15,100. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya sita, jumla ya miradi 1,004 imesajiliwa katika sekta mbalimbali. Kama inavyoonesha katika **Umbo 1**, sekta tano zinazoongoza katika kusajili miradi ni uzalishaji viwanda (miradi 456, 45%), usafiri na usafirishaji (miradi 179, 18%), utalii (miradi 95, 9%), kilimo (miradi 88, 9%), na huduma (45, 4%).





Umbo 1**: *Asilimia ya Miradi Iliyosajiliwa TIC Kisekta 2021-2023.***

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka 27 (1996-2023), tangu TIC ianze kuweka rekodi za miradi ya uwekezaji, jumla ya miradi 12,381 imesajiliwa iliyotarajiwa kuajiri watu 1,772,607 na kuingiza mtaji kutoka nje wa jumla ya dola za Marekani bilioni 117.821 kama inavyoonekana katika ***Kiambatisho Na. 3***.


**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** maumbo ya 2-4 yanaonesha wastani wa idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na TIC kwa mwaka kwa kila awamu ya uongozi, pamoja na idadi ya ajira na kiwango cha mtaji kilichotokana na miradi hiyo. Kama inavyoonekana katika maumbo haya, wastani wa miradi 281, 708, 282 na 358 ilisajiliwa kwa mwaka kwa awamu ya tatu, awamu ya nne, awamu ya tano na awamu ya sita, mtawalia. Miradi ilitarajiwa kuajiri watu 49,542, 85,954, 37,344 na 76,975, mtawalia. Aidha, wastani wa kiwango cha mtaji kilichotokana na miradi hii kwa awamu za uongozi ni dola za Marekani milioni 1,054 (awamu ya tatu), milioni 7,848 (awamu ya nne), milioni 2,959 (awamu ya tano) na milioni 4,669 (awamu ya sita).




Umbo 2: ***Wastani wa Idadi ya Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa na TIC kwa Mwaka kwa Awamu za Uongozi.***





Umbo 3: ***Wastani wa Idadi ya Ajira Zilizotokana na Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa na TIC kwa Mwaka kwa Awamu za Uongozi***





Umbo 4**:** ***Wastani wa Kiwango cha Mtaji (FDI, Milioni, USD) Kilichovutiwa kutokana na Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa na TIC kwa Mwaka kwa Awamu za Uongozi.***


**54.** ***Mheshimiwa Spika***, kama inavyooneshwa katika maumbo 5-7, idadi ya miradi, kiwango cha mtaji na ajira zitokanazo na miradi ya uwekezaji katika Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC) imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, idadi ya miradi iliongezeka kutoka miradi 207 mwaka 2020 hadi kufikia miradi 526 mwaka 2023. Kiwango cha mitaji inayotokana na miradi ya uwekezaji kilipanda kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,092.7 mwaka 2020 hadi Dola za Kimarekani Milioni 5,720.4 mwaka 2023. Aida, idadi ya ajira itokanayo na miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka 17,385 mwaka 2020 hadi 137,010 mwaka 2023.




Umbo 5**: Miradi Iliyosajiliwa TIC kati ya Mwaka 2020 na 2023**




Umbo 6: **Mitaji Iliyovutiwa Kutoka Nje (FDI) Kutokana na Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa na TIC kati ya Mwaka 2020 na 2021**




Umbo 7: **Idadi ya *Ajira Zilizotarajiwa Kupatikana* Kutokana na Miradi ya Uwekezaji kati ya Mwaka 2020 - 2023**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2024 EPZA imesajili na kutoa leseni 26 zikiwemo leseni 24 za uendeshaji kwa miradi mipya kwenye maeneo ya uzalishaji kwa mauzo nje na leseni mbili (2) za uendelezaji kwa Kanda Maalum ya Kiuchumi za Buzwagi SEZ na

Kilimanjaro Industrial Park kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 4** cha kitabu cha hotuba. Usajili huo ni ongezeko la leseni 12 sawa na asilimia 86 ikilinganishwa na leseni 14 zilizosajiliwa na kutolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** kampuni hizo 25 zinatarajiwa kuwekeza mtaji wa dola za Marekani milioni 225.72, mauzo ya nje dola za Marekani milioni 355.12 na kutoa ajira kwa watanzania zipatazo 19,877. Aidha, miradi hiyo ipo katika sekta za kilimo miradi 12, madini miradi 5 na bidhaa za viwandani miradi 8. Masoko ya bidhaa zinazozalishwa ni pamoja na nchi za Bara la Ulaya, Marekani, Asia, Canada, Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan ya Kusini, China, Ukraine, Vietnam, Zambia, Misri, India, Dubai, Taiwan, Japan na Pakistani.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa na taasisi zingine za umma, hadi Machi, 2024 Serikali kupitia Sekta ya Madini imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 8,480 kati ya 6,920 zilizopangwa kutolewa katika kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 122.54. Mafanikio hayo yametokana na jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha uwekezaji. Leseni zilizotolewa ni: Leseni 9 za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs); Leseni 246 za Utafutaji wa Madini (PLs); Leseni 5,586 za Uchimbaji Mdogo (PMLs); Leseni 1,082 kubwa za biashara (DLs); Leseni 1,525 ndogo za biashara (BLs); na Leseni 32 za Uchenjuaji wa Madini (PCLs).

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** leseni 9 za uchimbaji wa kati wa madini (MLs) zilitolewa zinatarajiwa kuwa na uwekezaji wenye thamani ya takriban dola za Marekani 46,343,900 na kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ajira za kudumu 654. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji ili kuendelea kuwavutia wawekezaji kwa manufaa ya Watanzania katika kukuza Sekta ya Madini nchini na kuongeza Pato la Taifa.

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, nihitimishe eneo hili kwa kutoa taarifa kuwa Serikali inaendelea na majadiliano ya kimkataba na makampuni yanayotarajiwa kutekeleza mradi wa Gesi Asilia (Liquiefied Natural Gas-LNG). Mradi huu utahusisha ubadilishaji wa

gesi asilia kutoka katika hali ya hewa na kuwa kiminika. Kiasi cha gesi iliyogundulika baharini ni futi za ujazo trilioni 45.13 katika vitalu Na. 1,2 na 4. Aidha gesi iliyothibitishwa kuvunwa kwa ajili ya Mradi ni kiasi cha futi za ujazo trilioni 25. Thamani ya uwekezaji inayotarajiwa kufanyika katika mradi huu ni dola za Marekani bilioni 42 (zaidi ya shilingi trilioni 109).

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuchochea kasi ya ukuaji uchumi, kuongeza ajira nchini, kuingiza mtaji mkubwa kutoka nje (FDI), kuchochea ujenzi wa viwanda vinavyotumia gesi asilia kama malighafi, na kupanua shughuli za kiuchumi na kijamii nchini. Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuona kuwa majadiliano yanakamilika mapema iwezekanavyo ili utekelezaji wa mradi huu muhimu uanze.

## 3.4. UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UWEKEZAJI WA SEKTA BINAFSI

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeratibu zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa sekta binafsi ili kufahamu hatua za uendelezaji na changamoto za utekelezaji. Tathmini imebaini kuwa kati ya miradi 509 iliyosajiliwa na TIC hadi mwezi Machi, miradi 292 imeshaanza uendelezaji na miradi yote 26 iliyosajiliwa na EPZA imeanza uendelezaji na uendeshaji. Ofisi imeratibu utatuzi wa changamoto na migogoro mbalimbali iliyojitokeza kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vikao vya pamoja na wadau.  Changamoto nyingi zilizowasilishwa zinahusu migogoro ya ardhi, masuala ya kodi, miundombinu wezeshi ikiwemo nishati, barabara na maji. Aidha, Ofisi inaandaa kanzidata ya takwimu za uwekezaji ambayo itawezesha kujua hatua za uendelezaji wa miradi katika sekta mbalimbali na kutatua changamoto kwa wakati.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya miradi mikubwa ya kimkakati iliyoanza ujenzi na uzalishaji yenye matokeo chanya ya kiuchumi katika kuvutia mitaji, ajira, fedha za kigeni na teknolojia mpya ni kama ifuatavyo:

(i) Kiwanda cha *Sapphire Float Glass* kilichopo Mkuranga,

Pwani chenye thamani ya dola za Marekani milioni 311 (sawa na shilingi bilioni 700) chenye uwezo wa kuzalisha tani 700 za kioo na ajira za moja kwa moja 1,655 na zisizo za moja kwa moja 6,000. Kiwanda hicho ambacho ni cha kwanza kwa ukubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki kilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Septemba, 2023;

(ii) Kiwanda cha mbolea cha *Itracom Fertilisers* kilichopo Nala Jijini Dodoma;

(iii) Kiwanda cha sukari cha *Mkulazi Holdings Limited* kilichopo Mbigiri, Morogoro;

(iv) Kiwanda cha kuchakata gesi asilia kwa ajili ya nishati ya magari cha kampuni ya *Taqa Dalbit*, Jijini Dar es Salaam;

(v) Mradi mkubwa wa kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari cha *Kasulu sugar project* kilichopo Kasulu, Mkoani Kigoma;

(vi) Viwanda vya kuzalisha sukari kwa viwanda vya *Kagera Sugar*, *Kilombero Sugar* na *Mtibwa Sugar*; na

(vii) Kiwanda cha uzalishaji wa kioo kwa ajii ya majengo cha *Keda Tanzania Ceramics Limited* kilichopo Mkuranga, Mkoani Pwani.

## 3.5. UANZISHWAJI NA UENDELEZAJI WA MAENEO MAALUM YA KIUCHUMI NA MIRADI YA KIMKAKATI

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi ya maeneo maalum ya kiuchumi na miradi ya uwekezaji ya kimkakati inayotekelezwa na sekta binafsi na sekta ya umma.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** moja ya miradi hii ni kongani ya viwanda ya ***Modern Industrial Park* (KAMAKA)** iliyopo Kikongo, Mlandizi, Wilaya ya Kibaha mkoa wa Pwani yenye ukubwa wa ekari 1,077.

Jumla ya uwekezaji unaotarajiwa katika mradi huu ni dola za Marekani milioni 51 ikihusisha ujenzi wa miundombinu ya kongani na dola za Marekani bilioni 1.3 ikihusisha uwekezaji wa viwanda ndani ya kongani. Kongani hiyo itakapokamilika itavutia viwanda **210** vitakavyozalisha ajira mpya za moja kwa moja **30,000** na zisizo za moja kwa moja **200,000**.

***65. Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine ni ujenzi wa ***Sino Industrial Park*** unaotekelezwa na Kampuni ya Group VI International. Kongani hii ipo eneo la Kwala mkoani Pwani yenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo uendelezaji wake utagharimu dola za Marekani milioni 327.4. Aidha, mradi huo unatarajia kuvutia viwanda vikubwa 200 na viwanda vidogo 300 vitakavyowekeza mtaji wa dola za Marekani bilioni 3 na kutoa ajira 100,000 za moja kwa moja na 500,000 zisizo za moja kwa moja. Hadi kufikia Machi, 2024, kampuni ya SINO-TAN imesaini jumla ya Hati za Makubaliano 15 na wawekezaji 50 waliooonesha utayari wa kuwekeza katika eneo la kongani hiyo. Aidha, kampuni imesaini mikataba ya upangaji na kampuni tano (5) ambapo kampuni mbili (2) tayari zimeanza uzalishaji wa nguo na vipodozi.

***66. Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine ni ujenzi wa kongani ya viwanda ya ***Elsewedy Industrial Park*** inatarajiwa kujengwa eneo la Kikongo, Mlandizi mkoa wa Pwani itakayokuwa na ukubwa wa ekari 650. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya *Elsewedy Eletric* na inahusisha eneo lenye ukubwa wa ekari 500 ambapo uendelezaji wake utagharimu dola za Marekani milioni 460. Mradi utavutia ujenzi na viwanda takribani 150 vitakavyowekezwa na kuzalisha ajira mpya za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 50,000.

***67. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia inaendelea kuratibu mradi wa uendelezaji wa eneo maalum la kiuchumi Bagamoyo unaotekelezwa na Mamlaka ya EPZ. Katika kipindi cha Mwaka 2023/24, Ofisi imekamilisha uhuishaji wa Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa mradi wa Bagamoyo SEZ kwa malengo ya kuhuisha gharama ya fidia, kuimarisha uwekezaji wa ndani, kuhifadhi maeneo ya kihistoria na kuwezesha uwekezaji shirikishi kupitia ubia na sekta binafsi, na kupitia soko la mitaji. Vilevile, Ofisi imewezesha kazi ya upembuzi yakinifu ya mradi ambao

umebainisha kuwa mradi unatekelezeka na utakuwa na manufaa katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii, masoko na fedha (*economic, social, market and financially feasible*). Aidha, manufaa ya jumla yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na: kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi; ukuaji wa teknolojia, ujuzi na ajira; kuongezeka kwa biashara; kuongezeka kwa fedha za kigeni; kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kunufaika kikamilifu na fursa ya Soko huru la Africa. Ofisi imewezesha pia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami (Asphalt Concrete) yenye urefu wa kilomita tatu (3) ndani ya eneo la mradi mabapo hadi Machi 2024 ujenzi umefikia asilimia 70.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya EPZ pia inatekeleza miradi mingine na maeneo maalumu ya kiuchumi katika mikoa ya Ruvuma, Dodoma na Shinyanga. Katika mwaka 2023/24 Serikali imekamilisha malipo ya fidia kwa Eneo Maalum la Kiuchumi la Ruvuma (Ruvuma Special Economic Zones) lenye ukubwa wa hekta 2,033 ambapo jumla ya **shilingi 5,337,632,743.07** zimelipwa. Aidha, Mamlaka ya EPZ imekamilisha taratibu za kumiliki eneo Maalum la Kiuchumi la Kwala (***Kwala Special Economic Zone***) ambalo lina ukubwa wa ekari 100. Hadi Machi 2024, Mamlaka imefanikiwa kupata hati ya eneo na kukamilisha uaandaji wa Hadidu za rejea ili kumpata mtaalam wa kuandaa michoro na gharama za miundombinu ya msingi. Vilevile, Mamlaka imekamilisha taratibu za kumiliki Eneo Maalum la Kiuchumi la Nala (***Nala Special Economic Zone***) lenye ukubwa wa ekari 1,500 kwa kulipa fidia kwa Jiji la Dodoma **shilingi bilioni 4.57**.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya EPZ imekamilisha taratibu za kutangazwa kwa Eneo Maalum la Kiuchumi la Buzwagi (Buzwagi SEZ) ambalo linamilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Eneo hilo lipo katika eneo la uchimbaji wa madini lililofungwa la Buzwagi lenye ukubwa wa ekari 3,295. Eneo hilo limetangazwa kwa kuzingatia mpango wa ufungaji wa mgodi (*closure plan*) chini ya usimamizi wa Tume ya Madini na kulipa matumizi ya uwekezaji ili kuvutia uongezaji thamani wa madini. Eneo la Buzwagi limevutia uwekezaji wa taasisi na kampuni mbalimbali ikiwemo Chuo cha Barrick Academy ambacho kitatoa mafunzo kwa wafanyakazi wa kampuni za Barrick kutoka

bara la Afrika, Kabanga Company Ltd na Tembo Nickel Ltd zilizopanga kuanzisha miradi ya uchenjuaji wa madini ya Nickel na Cobalt, kampuni ya ISOAF Ltd ambayo ni kampuni tanzu ya the East African Crude Oil Pipeline (EACOP) wanaojishuhulisha na uchakataji wa mafuta, International Apprenticeship & Competency Academy (IACA) inayojishughulisha na mafunzo ya uzalishaji viwandani, SSI Energy, Voltalia na SAFI power zinazojishughulisha na kufua umeme wa sola.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia imeshiriki kwenye mapitio na maandalizi ya kanuni za kusimamia Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rasimu ya Kanuni hizo zitajadiliwa katika Mikutano ya Maamuzi Mei, 2024. Kanuni hizo zitakuwa chachu ya utekelezaji wa malengo ya kimkakati kwenye Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ) ndani ya Nchi Wanachama.

## 3.6 MABORESHO YA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI NA BIASHARA

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (***MKUMBI***), maarufu kama ***Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment***, unaolenga kuondoa vikwazo vya kufanya biashara na uwekezaji nchini. Mpango huu unatekelezwa na wizara zote za kisekta pamoja na mamlaka za serikali za mitaa, pamoja na sekta binafsi, ukiratibiwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Kitengo cha Maboresho ya Mazingira ya Biashara. Pamoja na mambo mengine, Mpango huu unahusisha mapitio ya sheria, kanuni na taratibu, kuondoa muingiliano wa majukumu, ujenzi wa mifumo ya kielektroniki, kuimarisha uwezo wa idara za viwanda, biashara na uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2022 Serikali iliajiri mtaalam mwelekezi kufanya tathmini ya utekelezaji wa MKUMBI ili kubaini hatua iliyofikiwa na changamoto zilizojitokeza katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Taarifa ya tathmini hiyo imehuishwa mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, taarifa ya tathmini hiyo imebaini mafanikio yafuatayo katika uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini.

(i) Maeneo 80 ya Sheria ya Fedha yanayohusiana na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yamefanyiwa marekebisho kati ya mwaka 2018/19 na mwaka 2021/22;

(ii) Sheria na kanuni 55 katika sekta za uwekezaji, viwanda, biashara, kilimo, ufugaji, afya, maliasili na utalii zimerekebishwa. Marekebisho haya yamesaidia kupunguza ushuru na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji;

(iii) Tozo, ada na faini 374 zilizobainika kukwaza uanzishwaji wa biashara na uwekezaji zilifutwa zikihusisha taasisi mbalimbali, zikiwemo TBS, TMDA, Bodi ya Sukari Tanzania (*Sugar Board of Tanzania – SBT*), OSHA, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (***Government Chemist Laboratory Authority-GCLA***), na Jeshi la Zimamoto;

(iv) Kuunganisha mamlaka za urekebi ambazo majukumu yake yalionekana kuingiliana. Kwa mfano majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) yalihamishiwa katika Taasisi ya Viwango (TBS). Aidha, majukumu ya kutoa vibali vya kusafirisha kemikali yalihamishwa kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na hivyo kuondoa muingiliano uliokuwepo miongoni mwa taasisi hii na TMDA na TANROADS. Vivile, Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) Sura ya 415 ilifanyiwa marekebisho ili kuondoa haki pekee (exclusive mandate) ya uondoshaji na usafirishaji (clearing and forwading) wa shehena kwa njia ya maji. TASAC sasa inahusika na bidhaa nne pekee, ambazo ni makinikia, wanyama hai, kemikali zinazotumika migodoni, na nyara za serikali;

(v) Ujenzi wa mifumo ya kielektroniki 42 kupitia wizara na taasisi mbalimbali ambao umeboresha utoaji wa huduma mbalimbali za kibiashara;

(vi) Kupungua kwa idadi ya siku za kupata huduma kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla. Kwa mfano:

a) Muda wa kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka wa Tunduma umepungua kutoka siku saba (7) hadi siku tatu (3);

b) Muda wa kusajili hospitali binafsi umepungua kutoka miezi 12 hadi miezi 3;

c) Muda wa kupata usajili wa sehemu za kazi umepungua kutoka siku 14 hadi siku 1;

d) Muda wa kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya sheria ya usalama na afya mahala pa kazi umepungua kutoka siku 28 hadi siku tatu (3); na

e) Kupungua kwa muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka zaidi ya siku 14 hadi kati ya siku tatu (3) na saba (7).

(vii) Kuongezeka kwa kiwango cha kuzingatia sheria, kanuni na taratibu (compliance);

(viii) Kupungua kwa malalamiko dhidi ya mamlaka za urekebu za serikali;

(ix) Kuongezeka kwa kampuni zinazosajiliwa kutoka kampuni 7,817 mwaka 2018/19 hadi kampuni 10,656 kwa mwaka mwaka 2021/22; na

(x) Kuanzishwa kwa idara/sehemu inayoshughulikia biashara, viwanda na uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, taarifa ya tathmini hiyo imebaini changamoto kadhaa ambazo zinaendelea kukwamisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Changamoto hizi ni pamoja na:

(i) MKUMBI kutofahamika ipasavyo kwa wafanyabiashara na wadau kwa ujumla. Kwa mfano, asilimia 91 ya wafanyabiashara waliohojiwa walisema hawakuwa na uelewa kuhusu MKUMBI;

(ii) Kuanzishwa kwa tozo, ada na faini mpya pasipokufanya tathmini ya kina kuhusu athari zake katika mazingira ya biashara na uwekezaji; na

(iii) Kukosekana kwa utaratibu wa ukaguzi wa pamoja kwa mamlaka za urekebu.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea kutoa elimu kwa Taasisi za udhibiti ambazo zina mwingiliano wa majukumu ya kiutendaji. Hatua hiyo imewezesha baadhi ya mamlaka za udhibiti kuondoa mwingiliano wa majukumu kwa kukubaliana namna bora ya utekelezaji. Mfano Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Bodi ya Nyama zimeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) kuhusu usajili, uuzaji na uhifadhi wa nyama hivyo kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi. Aidha, katika kuboresha mifumo ya ukaguzi kwa mamlaka za uthibiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Jeshi la Zimamoto na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zimeandaa mwongozo wa pamoja wa hatua za kufuata katika kufanya ukaguzi "*Standard Operating Procedures - SOP*" ili kusaidia kupunguza kaguzi za mara kwa mara kutoka taasisi mbalimbali.

## 4. MPANGO NA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2024/25

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/25 umezingatia miongozo mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Miongozo hiyo ni pamoja Mpango Mkakati wa Mpito wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji wa Miaka Miwili 2024/25 - 2025/26; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020;

Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; Mikakati na makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Mkakati wa Sita wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa miaka mitano (2021/22 - 2025/26); Agenda 2063: Afrika Tuitakayo ya Umoja wa Afrika; Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mikakati ya kisekta na masuala mtambuka ikiwemo rushwa (NACSAP IV) na UKIMWI.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo kuu la Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni kuendelea kuimarisha ofisi hii ili itekeleze majukumu yake kikamilifu katika kuratibu mipango thabiti inayolenga kuleta maendeleo endelevu na jumuishi kwa wananchi; kuvutia uwekezaji wenye tija kwa Taifa; uboreshaji wa mazingira ya biashara; na uendeshaji wenye tija wa mashirika na taasisi za umma.

## 4.1 VIPAUMBELE NA KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA MWAKA 2024/25

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imepanga kutekeleza vipaumbele na majukumu yafuatayo:-

(i) Kukamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;

(ii) Kukamilisha uandaji wa sera mpya ya uwekezaji na mkakati wake wa utekelezaji;

(iii) Kukamilisha uunganishaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA) na kuanzisha Taasisi mpya ya kusimamia masuala ya Uwekezaji wa sekta Binafsi;

(iv) Kukamilisha mwongozo wa ujenzi na uendeshaji wa kongani za viwanda nchini;

(v) Kufanya tathmini kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi (special economic zones) nchini;

(vi) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa mageuzi katika uendeshaji wa mashirika ya umma, ikiwemo kuendelea kubaini mashirika ambayo majukumu yake yamepitwa na wakati au yanaingiliana na majukumu ya taasisi zingine na kuchukua hatua stahiki, pamoja na kuweka vigezo bayana vya upimaji wa utendaji wa mashirika ya umma;

(vii) Kuandaa na kutekeleza programu ya kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Uwekezaji Binafsi;

(viii) Kufanya mapitio ya Sheria zinazohusu masuala ya madini, ardhi, kilimo, utalii na biashara kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini;

(ix) Kukamilisha Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake;

(x) Kufanya Stadi ya Kizio (Baseline Study) kwa ajili ya mapendekezo ya kuandaa Sera ya Uwekezaji wa Umma;

(xi) Kuandaa mkakati fungamanishi wa kisekta wa ufuatiliaji na tathmini kuhusu masuala ya mipango na uwekezaji;

(xii) Kuanza utekelezaji mradi wa kielelezo wa ukanda maalum wa kiuchumi Bagamoyo kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa mwaka 2024;

(xiii) Kufanya utafiti wa urahisi wa ufanyaji biashara na uwekezaji Tanzania kwa mwaka 2024 (*National Ease of Doing Business Study 2024*) ili kuchochea ushindani na uwekaji mazingira bora ya biashara ndani ya nchi;

(xiv) Kuanzisha ushindanishi katika sekretariati za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhusu kuvutia wawekezaji na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara;

(xv) Kuhuisha Mpango wa Maboresho wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji utakaoainisha changamoto mpya za Uwekezaji na Biashara nchini; na

(xvi) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

## 4.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa Taasisi

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inasimamia mafungu mengine mawili. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina na Fungu 66 – Tume ya Mipango. Aidha, Ofisi inasimamia taasisi nyingine mbili za EPZA na TIC. Vipaumbele na majukumu ya taasisi hizi ni kama ifuatavyo:

### *4.2.1 Ofisi ya Msajili wa Hazina*

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Ofisi ya Msajili wa Hazina ni pamoja na:

(i) Kuandaa Mpango Mkakati wa Muda Mrefu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kipindi cha miaka ishirini na tano (25);

(ii) Kuongeza makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kuimarisha mifumo ya Usimamizi na TEHAMA;

(iii) Kufanya mapitio ya Uwekezaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina (Investment Portfolio Mix) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa uwekezaji;

(iv) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na tathmini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kampuni Tanzu na Kampuni ambazo Serikali ni Mbia, na Mashirika yaliyobinafsishwa kwa kipindi maalum cha Uwekezaji kulingana na mikataba ya mauzo;

(v) Kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha utendaji kazi; na

(vi) Kuendelea kufanya uchambuzi wa taasisi na mashirika ya umma ili kubaini yanayopaswa kufutwa, kuunganishwa au kurekebishwa kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi.

### *4.2.2 Tume ya Mipango*

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, vipaumbele vya Tume ya Mipango ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na uratibu wa maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 na usimamizi wa Mikakati na Mipango ya Taifa ya Maendeleo katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya Serikali;

(ii) Kufanya tathmini ya thamani ya uwekezaji na athari ya miradi ya kielelezo na kimkakati katika kuendeleza na kukuza uchumi;

(iii) Kuwezesha tafiti za kisayansi, tathmini ya hali ya rasilimali za taifa na Sera mbalimbali kwa lengo la kuimarisha upangaji na utekelezaji kwa kuzingatia mipango ya maendeleo;

(iv) Kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo; na

(v) Kuendelea kuimarisha utendaji wa Tume ya Mipango kwa kuboresha mifumo ya TEHAMA, programu za mafunzo na kuelimisha umma kuhusu majukumu yake.

### *4.2.3 Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA)*

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, vipaumbele vya Mamlaka ni pamoja na:-

(i) Uendelezaji wa miradi ya kitaifa ya Kielelezo ikiwa ni pamoja na kuanza hatua za awali za kuandaa Mipango Kabambe, upembuzi yakinifu, kufanya uthamini katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ) ambayo hayakuthaminiwa awali na kufanya malipo ya fidia ya maeneo ya Bagamoyo, Tanga na Manyoni;

(ii) Kuzindua na kutangaza mradi wa Bagamoyo SEZ kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa nia ya kuendeleza mradi kwa njia mbalimbali ikiwemo ubia na sekta binafsi kwa kufuata mpango uliorejewa;

(iii) Kubaini bidhaa na kutumia huduma za soko la mitaji kupata fedha za kuendeleza miradi ya SEZ;

(iv) Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo saba (7) ya viwanda vilivyokabidhiwa kwa Mamlaka ya EPZ;

(v) Kuendeleza Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ) kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI, Sekta binafsi na Wadau wa maendeleo; na

(vi) Kutoa elimu kwa Umma, kufanya tafiti, ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa na Mamlaka ya EPZ.

***4.2.4 Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)***

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na:

(i) Kuboresha mifumo ya kusajili na kuhudumia wawekezaji;

(ii) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;

(iii) Kuanzisha masijala ya kielektroniki ya ardhi kwa wawekezaji, kuongeza kiasi cha ardhi ya uwekezaji kwenye benki ya ardhi na kuigawa kwa wawekezaji;

(iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya uwekezaji;

(v) Kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kutoa majawabu kuwezesha kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuibua fursa mpya za uwekezaji nchini; na

(vi) Kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuboresha mashirikiano kati ya TIC na wadau wa umma na binafsi ili

kurahisisha jukumu la uratibu wa uhamasishaji na huduma kwa wawekezaji nchini.

## 5. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, OFISI YA MSAJILI WA HAZINA NA TUME YA MIPANGO KWA MWAKA 2024/25

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2023/24 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka 2024/25, ninaomba sasa kuwasilisha rasmi Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25 kwa muhtasari kama ifuatavyo:

### (a) Mapato

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Msajili wa Hazina - Fungu 07 imepangiwa kukusanya na kuchangia kwenye mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya **shilingi trilioni 1.17** kutoka kwenye vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi ya gawio, Michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi, mrejesho wa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTMS), rejesho la riba na mikopo, ziada na mapato mengineyo.

### (b) Matumizi

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji na Taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha jumla ya **shilingi 121,329,199,000** ikiwa **shilingi 100,246,191,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 21,083,008,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2024/25. Uchambuzi wa kina wa matumizi wa kila fungu umeainishwa katika jedwali hapo chini.

| | **Fungu 11 : Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 18,652,532,000 |
| | Miradi ya Maendeleo | Sh. | 11,377,970,000 |
| | **Jumla** | **Sh.** | **30,030,502,000** |
| | **Fungu 07: Ofisi ya Msajili wa Hazina** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 24,898270,000 |
| | Matumizi Maalumu | | 18,889,139,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,289,658,000 |
| | **Jumla** | **Sh.** | **45,077,067,000** |
| | **Fungu 66: Tume ya Mipango** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 37,806,250,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 8,415,380,000 |
| **Jumla** | | **Sh.** | **46,221,630,000** |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.** | **121,329,199,000** |

## 6. HITIMISHO

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** hii ni bajeti ya kwanza ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Kupitia mpango na bajeti niliyowasilisha, viongozi na watumishi wote wa Ofisi hii na taasisi tunazozismimamamia tumejipanga vyema katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango endelevu ya maendeleo ya nchi yetu; kuhakikisha kuwa fursa za uwekezaji zinaendelea kupanuka na kuwanufaisha watanzania wote; na katika kuhakikisha kuwa mashirika ya umma yanaendeshwa kwa ufanisi ili yachangie kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii. Matokeo muhimu tarajiwa ya utekelezaji wa mpango na bajeti hii ni kukamilika kwa dira mpya ya taifa ya maendeleo, kupanuka kwa fursa za uwekezaji nchini, na kuimarika kwa utendaji na tija ya mashirika ya umma katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha hotuba yangu hii, ninaomba kumshukuru tena ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***, kwa kutupa heshima mimi na wenzangu ya kuongoza Ofisi hii nyeti katika maendeleo ya nchi yetu. Tunamshukuru kwa kuifanya kazi yetu kuwa nyepesi kutokana na maono yake mapana na uwezo wake bayana katika kuvutia wawekezaji. Aidha, tunampongeza kwa kuwa Rais wa pili wa nchi yetu katika kuandika Dira ya pili ya Taifa ya Maendeleo. Ninamuahidi kuwa, kwa uongozi na usimamizi makini wa **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Dira, zoezi hili la kuandika Dira

ya Taifa ya Maendeleo tutalisimamia kwa umakini mkubwa. Hatutamuangusha!

**88.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kuwashukuru wadau wote waliochangia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, pamoja na taasisi zilizo chini yake. Wadau hawa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Vyuo Vikuu na taasisi mbalimbali za tafiti.

**89.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru tena viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yetu. Hawa ni Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Ndugu Lawrence Nyasebwa Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; Ndugu Nehemia Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina, Ndugu Charles Itembe, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA; na Ndugu Gilead Teri, Mkurugenzi Mtendajii wa Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Ninawashukuru watumishi wote kwa utendaji wao makini uliochangia mafanikio ya Ofisi yetu katika mwaka mmoja uliopita tangu kuanzishwa kwake. Ninawasihi waendelee na ushirikiano huo na kuongeza bidii zaidi katika kazi ili tupate mafanikio makubwa zaidi.

**90.** ***Mheshimiwa Spika***, sasa ninaliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 121,329,199,000** ikiwa **shilingi 100,246,191,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 21,083,008,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2024/25.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, *www.planninginvestment.go.tz*

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja!

**Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb.)**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nilikuwa naangalia kitabu ulichotupa hapa na mwanzo ulisema tuchukue hiki ndiyo tuweke kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Wakati wa kuhitimisha hapo kuna mambo ya ziada uliyoyasema, kwa hiyo, naamini yale uliyasema, lakini unataka kitabu ndiyo kiingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge ili tujue tunaweka yapi kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Nichukue ya kauli yako ya mwanzo? Weka kisemeo vizuri tu hapo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye *Hansard* za Bunge kitabu chetu ndiyo kiingie, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja ya Mheshimiwa Waziri kuwa imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa niaba yake atakuja kutusomea hapa Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa nzima ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya awali; kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024

pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118, Kanuni Ndogo ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilimefanya kazi; Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati; Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na Sehemu ya Tano inahusu hitimisho.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji na makadirio ya ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawanda ya uchambuzi. Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matatu ambayo ni: -

(a) Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina;
(b) Fungu Na. 11 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; na
(c) Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini, ufafanuzi wa jumla. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, na kwa sababu hiyo, kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili. Naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Makusanyo ya maduhuli;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo;

(c) Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji;

(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(e) Ulinganishi wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ililenga kukusanya maduhuli ya shilingi trilioni 1.06 kupitia Fungu Na. 07, Ofisi ya Msajili wa Hazina. Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa ofisi hii kupitia Fungu Na. 07 imekusanya chini ya lengo. Hadi kufikia Februari, 2024 imekusanya shilingi bilioni 395.965 sawa na 37% tu. Mchanganuo wa maduhuli kwa Fungu Na. 07 unaoneshwa katika Jedwali Na. 1. la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba sababu ya ukusanyaji wa maduhuli kuonekana kuwa chini ya lengo ni kwa kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwenye fungu hili unatokana na gawio na michango kutoka kwenye mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, ambapo kwa utaratibu uliopo, gawio hutolewa ifikapo robo ya tatu na nne ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa maduhuli ya sasa hivi kufikia Februari, 2024 ulitokana na kodi ya upangishaji ya asilimia

15 ya michango ghafi, gawio, rejesho la riba na mikopo, ziada na malipo mengineyo na ukusanyaji wa madeni ya *EX-NBC* na ubinafsishwaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa matumizi ya bajeti Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, kwa mwaka wa fedha 2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 43.76. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 42.820 sawa na 98% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 5.229 ni mishahara na shilingi bilioni 37.59 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi milioni 940 sawa na asilimia mbili ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 17.758 sawa na 40.58% ambapo shilingi bilioni 16.818 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 39.27% ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.650 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 13.167 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 940 sawa na 100% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Fungu Na. 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 40.186. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 16.360 sawa na 41% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 4.501 ni mishahara na shilingi bilioni 11.858 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 23.826 sawa na 59% ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2024, fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 25.161 sawa na 62.61% ambapo shilingi bilioni 8.541 sawa na 52.2% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.543 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 4.997 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 16.620 sawa na 69.75% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, liliidhinishiwa jumla ya shilingi

bilioni 42.247. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 36.325, sawa na 86% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 5.88 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 30.44 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 5.922 sawa na 14% ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 14.743, sawa na 35%. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14.549, sawa na 40.05% kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 485.463 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 14.063 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi milioni 199.335 sawa na 3.36% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:-

(a) Kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 126.194 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi bilioni 57.663 sawa na 46% ya bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge.

(b) Hakuna taasisi yoyote chini ya ofisi hii iliyofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa 66.6% hadi kufikia Februari, 2024.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi hii zinapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Mchanganuo wa fedha hizo kwa mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji unaoneshwa katika Jedwali Na. 2 na Na. 3. ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ulikuwa ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi wa ifuatayo:-

(a) Fungu Na. 11 – Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji, mradi Na. 6260 *Institutional Support* ambao ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 6.710 ambapo mpaka kufikia Februari, 2024 mradi huu haukupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wake; na

(b) Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango, mradi Na. 2229: *Enhancement of Institutional Capacity and Research* ambao ulitengewa shilingi milioni 552.420 na mradi Na. 6389 Uendelezaji wa Miundombinu ya Ofisi ambao ulitengewa shilingi bilioni 5.2. Hadi kufikia Februari, 2024 miradi hiyo haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizopo chini yake. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii. Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina, hadi kufikia Februari 2024 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(a) Ofisi hii imefanikisha uunganishaji, utenganishaji na ufutaji wa taasisi kwa lengo la kuongeza tija ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa zinatoa mchango stahiki katika pato la Taifa na kuchangia bajeti ya nchi kama ifuatavyo:-

(i) Kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje;

(ii) Bodi ya Chai Tanzania na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai;

(iii) Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko na Bodi ya Pareto Tanzania;

(iv) *TARI* na Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania;

(v) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania;

(vi) Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa; na

(vii) Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa na Wakala ya Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imefuta Taasisi ya Lishe na Chakula, Shirika la Elimu Kibaha pamoja na Bodi ya Pareto Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ofisi hii imekamilisha na kuingia mikataba katika viwanda mbalimbali kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Fungu Na. 11 - Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji, hadi kufikia Februari, 2024 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa fungu hili pamoja na mambo mengine, imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(a) Kuratibu zoezi la maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Uzinduzi wa zoezi la ukusanyaji wa maoni kitaifa ambapo hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya maoni 601,349 yamepokelewa; na

(ii) Kufanyika kwa vikao vya majadiliano na makundi mbalimbali ikiwemo Baraza la Maaskofu Tanzania, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania na Baraza la Sunna Tanzania; na

(b) Kukamilika kwa Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ambao

utachochea mageuzi ya mfumo wa uchumi na kukuza ustawi wa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara na Taasisi zilizo chini ya ofisi hii ziliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 30.689 kwa miradi ya maendeleo. Mchanganuo huo wa fedha unaonekana katika Jedwali Na. 6 katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu Sita kwa kuendelea kufungua milango na fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; maduhuli, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.168 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.069 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kama ambavyo imebainishwa katika Jedwali Na. 5 la taarifa yetu. Hii ni sawa na ongezeko la 9.26% ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka ambao unaisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo la makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 litatokana na ongezeko la Mashirika ya Umma yatakayochangia michango ya 15% ya mapato ghafi na ongezeko la gawio kutokana na hisa zilizowekezwa na Serikali kwenye mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini yake, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 100.246, ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 17.885 ni mishahara na shilingi bilioni 82.360 ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali Na. 6 la taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 4.740, sawa na asilimia tano ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 95.505.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa pamoja na huduma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 21.083, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.589 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 5.493 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2024/2025 imepungua kwa shilingi bilioni 9.606 ambayo ni sawa na 31.3% ukilinganisha na bajeti ya mwaka unaoisha. Sababu ya kupungua kwa bajeti kumechangiwa na ukomo wa bajeti ya Serikali kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali namba saba la taarifa yetu. Kamati inapongeza jitihada za

Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati, maoni ya jumla, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kuwa Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 07, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Kamati inashauri: -

(a) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaongeza uwekezaji katika masoko ya hisa na taasisi binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa;

(b) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake;

(c) Serikali iongeze mitaji kwenye taasisi na mashirika ya Umma ili kuleta tija na kuongeza faida.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 11 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Kamati inashauri;

(a) Serikali ihakikishe inaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kwa kutoa huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwenye eneo maalum katika kila mkoa;

(b) Serikali ihakikishe inatenga hifadhi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahususi;

(c) Serikali iendelee kutoa elimu ya uwekezaji na fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali hususani vijana ili kuongeza uwekezaji na biashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 66, Tume ya Mipango, Kamati inashauri:-

(a) Serikali ihakikishe kwamba, Dira ya Mpango wa Maendeleo 2050 iendane na maendeleo ya nchi na maendeleo ya watu sambamba na kufanya mabadiliko ya mifumo ya kiutawala hususani mifumo ya Serikali za mitaa; na

(b) Serikali ihimize matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo *(NPMIS)* kwa watekelezaji wa miradi ya maendelelo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango; Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano ambao wameendelea kutoa kwa Kamati kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida, Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Ndugu Nehemiah Kyando Mchechu, Msajili wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kipekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(iii) Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

(v) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

**1.2. Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

**1.3. Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matatu (3) ambayo ni: -

a) **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina;
b) **Fungu 11** - Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji; na
c) **Fungu 66** – Tume ya Mipango

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matano yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(i) Makusanyo ya maduhuli;

(ii) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(iii) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji;

(iv) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(v) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.2 Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ililenga kukusanya maduhuli ya **Sh.1,069,496,256,000.00** kupitia Fungu Na. 07 Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa Ofisi hii kupitia Fungu Na. 07 imekusanya chini ya lengo, hadi kufikia Februari, 2024 makusanyo ni **Sh. 395,965,599,220.07** sawa na **asilimia 37** tu.

Aidha, mchanganuo wa maduhuli kwa Fungu Na. 07 unaoneshwa katika **Jedwali Na. 1.**

**JEDWALI NA. 1: Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKUSANYO YA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili Wa Hazina | 1,069,496,256,000 | 395,965,599,220.07 | 37 |
| **JUMLA KUU** | **1,069,496,256,000** | **395,965,599,220.07** | **37** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba sababu ya ukusanyaji wa maduhuli kuonekana kuwa chini ya lengo ni kwa kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwenye Fungu hili unatatokana na gawio na michango kutoka kwenye mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa ambao kwa utaratibu uliopo gawio hutolewa ifikapo robo tatu na nne ya mwaka**.**

**Mheshimiwa Spika**, Ukusanyaji wa Maduhuli hadi kufikia Februari, 2024 unatokana na Kodi za Upangishaji, Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi, Gawio, Marejesho ya TTMS, Rejesho la Riba na Mikopo, Ziada na Malipo mengineyo na Ukusanyaji wa Madeni ya EX-NBC na Ubinafsishaji.

**2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti**

**2.3.1 Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili lilidhinishiwa jumla ya **Sh. 43,760,316,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 42,820,316,000.00** sawa na **asilimia 98** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 5,229,041,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 37,591,275,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 940,000,000.00** sawa na **asilimia 2** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 17,758,356,737.83** sawa na asilimia **40.58** ambapo **sh. 16,818,356,737.83** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na **asilimia 39.27** ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 3,650,980,692.04** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh. 13,167,376,045.79** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 940,000,000.00** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**2.3.2 Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili lilidhinishiwa jumla ya **Sh. 40,186,656,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 16,360,334,000.00** sawa na **asilimia 41** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 4,501,598,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 11,858,736,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 23,826,324,000.00** sawa na **asilimia 59** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 25,161,500,849.02** sawa na asilimia **62.61** ambapo **sh. 8,541,025,425** sawa na **asilimia 52.2** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 3,543,078,425.67** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.4,997,947,000.00** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 16,620,475,423.35** sawa na **asilimia 69.75** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**2.3.3 Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili lilidhinishiwa jumla ya **Sh. 42,247,957,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 36,325,202,000.00** sawa na **asilimia 86** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 5,880,000,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 30,445,202,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 5,922,755,000.00** sawa na **asilimia 14** ilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 14,743,385,029.16** sawa na asilimia **35** kati ya fedha hizo **sh. 14,549,050,029.16** sawa na **asiliimia 40.05** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 485,463,618.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.14,063,586,411.16**

ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo(OC), na **Sh. 199,335,000.00** sawa na **asilimia 3.36** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 126,194,929,000.00** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hii iliokea Jumla ya **Sh. 57,663,242,616.01** sawa na **asilimia 46** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

(b) Hakuna taasisi yoyote chini ya Ofisi hii iliyofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Ofisi hii zinapatikana kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2** na **Jedwali Na. 3**.

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 42,820,316,000.00 | 16,818,356,737.83 | 39.27 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | 16,360,334,000.00 | 8,541,025,425.00 | 52.2 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | 36,325,202,000.00 | 14,549,050,029.16 | 40.05 |
| **JUMLA KUU** | **95,505,852,000.00** | **39,908,432,191.99** | **41** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**JEDWALI NA. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 940,000,000.00 | 940,000,000.00 | 100 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | 23,826,324,000.00 | 16,620,475,423.35 | 69.75 |
| **Fungu 66** – Tume Mipango | 5,922,755,000 | 199,335,000.00 | 3.36 |
| **JUMLA KUU** | **30,689,079,000.00** | **17,759,810,423.35** | **58** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ni wa kuridhisha, isipokuwa katika miradi wa ifuatayo;

a) **Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji**
**Mradi Na. 6260: Institutional Support** ambao ulitengewa kiasi cha **sh. 6,710,090,000.00** ambapo hadi kufikia Februari, 2024 mradi huu haukupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wake; na

b) **Fungu Na. 66 – Tume ya Mipango**

**Mradi Na. 2229: Enhancement of Institutional Capacity and Research** ambao ulitengewa **Sh. 523,420,000.00** na **Mradi Na. 6389: Uendelezaji wa Miundombinu ya Ofisi** ambao ulitengewa **Sh. 5,200,000,000.00,** hadi kufika Kufikia Februari 2024 Miradi hiyo haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo.

**2.4 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais,**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:

**2.4.1 Fungu Na. 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:

Ofisi hii imefanikisha Uunganishaji, Utenganishaji au Ufutaji wa Taasisi kwa lengo la kuongeza tija ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa zinatoa mchango stahiki katika Pato la Taifa na kuchangia Bajeti ya Nchi. Kama ifuatavyo: -Kuunganishwa kwa: -

(i) Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA);

(ii) Bodi ya Chai Tanzania na Wakala ya Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai – TSHTDA;

(iii) Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) na Bodi ya Pareto Tanzania;

(iv) TARI na Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (Tea Research Institute of Tanzania -TRIT), Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku Tanzania (Tobacco Research Institute of Tanzania – TORITA) na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI);

(v) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO);

(vi) Bodi ya Nyama (TMB) na Bodi ya Maziwa (TDB); na

(vii) Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (National Identification Authority – NIDA) na Wakala ya Usajili, Ufilisi na Udhamini (Registration, Insolvency and Trusteeship Agency - RITA). Aidha, Serikali imefuta Taasisi ya Lishe na Chakula (TFNC), Shirika la Elimu Kibaha (KEC) pamoja na Bodi ya Pareto Tanzania (TPB); na

(viii) Ofisi hii imekamilisha na kuingia Mikataba kwa masharti mapya na wamiliki wawili kwa lengo la kuendeleza viwanda vya CDA Integrated and Concrete Industries Ltd na Sikh Sawmill Ltd. Aidha, majadiliano na wamiliki wa awali wa viwanda viwili (2) vilivyobaki yanaendelea. Vilevile, mchakato wa kutafuta mwekezaji wa kiwanda cha Kilimanjaro Paddy Hauling Company Limited unaendelea.

**2.4.2 Fungu Na. 11- Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:

(a) Kuratibu zoezi la maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa kufanya yafuatayo: Uzinduzi wa zoezi la ukusanyaji wa maoni kitaifa ambapo hadi Februari 2024 jumla ya maoni 601,349 yamepokelewa; na kufanyika kwa vikao vya majadiliano na makundi mbalimbali ikiwemo Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA); na

(b) Kukamilika kwa Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25 ambao utachochea mageuzi ya mfumo wa uchumi na kukuza ustawi wa maendeleo ya watu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha.

## 2.5 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara na taasisi zilizo chini ya ofisi hii ziliidhinishiwa jumla ya **Sh 30,689,079,000.00** kwa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** PFMRP | 940,000,000.00 |
| **Fungu 11** – Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji | **NA. 4920** Tanzania Min Tiger Plan 2020<br>**NA. 4933** Export Processing zone Development.<br>**NA. 6260** Institutional Support<br>**NA. 4901** Implementation of BEST Programme | 1,896,549,000.00<br>2,000,000,000.00<br><br>6,710,090,000.00<br>13,727,640,327.35 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | **NA. 2229** Enhancement of Institutional Capacity<br>**NA. 6389** Uendelezaji wa Miundombinu ya Ofisi<br>**NA. 6526** Mradi wa Poupulation Planning | 523,420,000.00<br><br>5,200,000,000.00<br><br>199,335,000.00 |
| **JUMLA KUU** | | **29,300,485,327.35** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza Serikali ya awamu sita kwa kuenelea kufungua milango na fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi**.**

### 2.6 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 1,168,543,413,000.00** ikilinganishwa na **Sh. 1,069,496,256,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ambavyo imeainishwa katika **Jedwali Na. 5**. Hii ni na sawa na ongezeko la **asilimia 9.26** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha.

**JEDWALI NA. 5: Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025**

| FUNGU | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 |
|---|---|---|
| **Fungu 7** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 1,069,496,256,000.00 | 1,168,543,413,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **1,069,496,256,000.00** | **1,168,543,413,000.00** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo la makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 litatokana na ongezeko la Mashiriika ya Umma yatakayo changia Michango ya asilimia 15 ya Mapato ghafi na ongezeko la gawio kutokana na hisa zilizowekezwa na Serikali kwenye Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

## 3.2 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 100,246,191,000.00** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 17,885,398,000.00** ni mishahara, na **Sh. 82,360,793,000.00** ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 6**

**JEDWALI NA. 6: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | 7,305,056,000.00 | 36,482,353,000.00 | 43,787,409,000.00 |
| **Fungu 11**– Ofisi Rais Mipango na Uwekezaji | 6,774,092,000.00 | 11,878,440,000.00 | 18,652,532,000.00 |
| **Fungu 66** – Tume ya Mipango | 3,806,250,000.00 | 34,000,000,000.00 | 37,806,250,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **17,885,398,000** | **82,360,793,000** | **100,246,191,000** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha **Sh. 4,740,339,000.00** sawa na **asilimia 5** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 95,505,852,000.00**.

Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili

kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.3 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 21,083,008,000/=** kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 15,589,062,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 5,493,946,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepunguaa kwa **Sh. 9,606,071,000.00** sawa na **asilimia 31.3** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya kupungua kwa bajeti kumechangiwa na ukomo wa bajeti ya Serikali. Kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 7.**

**JEDWALI NA. 7: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 07** – Ofisi ya Msajili wa Hazina | **NA. 6251** Programu ya maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 617,818,000.00 | 671,840,000.00 |
| **Fungu 11**– Ofisi ya Rais,Mipango na Uwekezaji | **NA. 4429** 6260 Institutional Support<br>**NA 4933** Export Processing Zone Development<br>**NA 4920** Tanzania Mini Tiger Plan 2020<br>**NA 4901** Implementation of BEST Programme | 4,410,226,000<br><br>1,314,506,000<br>1,246,512,000 | 1,000,000,000<br><br><br>3,406,726,000 |
| **Fungu 66** – | **NA. 2229** Enhancement | 8,000,000,000 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tume ya Mipango | of Institutional Capacity and Research<br>**NA 6251** PFMRP VI | | 415,380,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **15,589,062,000** | **5,493,946,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **21,083,008,000** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kuwa Serikali ijiwekee malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji, na hali halisi ya vyanzo vya mapato.

### 4.2 Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

(i) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaongeza Uwekezaji katika masoko ya Hisa na Taasisi Binafsi zenye tija na manufaa kwa Taifa;

(ii) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ihakikishe kwamba inaweka makadirio ya makusanyo ya maduhuli yanayoakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyanzo vyake;

(iii) Serikali iongeze mitaji kwenye taasisi na Mashirika ya Umma, ili kuleta tija na kuongeza faida.

### 4.3 Fungu 011 - Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji

(i) Serikali ihakiikishe inaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, kwa kutoa huduma kwa wafanyabiashara na wawekezaji kwenye eneo maalum katika kila Mkoa;

(ii) Serikali ihakikishe inatenga hifadhi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahususi;

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu ya Uwekezaji na fursa za Uwekezaji kwa wadau mbalimbali hususani Vijana ili kuongeza uwekezaji na biashara ndani na nje ya nchi.

### 4.4 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu

### 4.4.1 Fungu 66 – Tume ya Mipango

(i) Serikali ihakikishe kwamba, Dira ya Mpango wa maendeleo 2050 iendane na Maendeleo ya Nchi na Maendeleo ya watu sambamba na kufanya mabadiliko ya mifumo ya Kiutawala hususani mifumo ya Serikali za mitaa; na

(ii) Serikali ihimize matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo NPMIS kwa watekelezaji wa miradi ya maendelelo.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**

3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ambae pia ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo, (Mb) –Waziri Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa ushirikiano ambao wameendelela kutoa kwa Kamati kwa wakati wote.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi hiyo pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Tausi Mbaga Kida, Ndg. Laurence Mafuru – Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Ndg. Nehemiah Kyando Mchechu - Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya

Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
22 Aprili, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage kwa niaba ya Kamati kwa kutupa maoni haya.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshasikiliza hotuba kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini pia upande wa Kamati wameleta maoni yao hapa.

Sasa kama ilivyo ada, tutaanza uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge na ninayo majina hapa, lakini kabla hatujaanza kutangaza hayo majina, nimeletewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwamba kati ya wageni wa Wizara au wageni wake Mheshimiwa Profesa yupo pia Dkt. Binilith Mahenge ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya halafu Mheshimiwa Neema William Mgaya ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na pumzi ya kuendelea kuishi. Natoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kuridhia kwake na kuleta mabadiliko ya sheria na kurudisha Tume ya Mipango. Kipekee nampongeza pia kwa kuchukua muda mfupi sana, akaunda Wizara ambayo ndiyo hii leo tunajadili hotuba yake ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Huyu ni mwanazuoni mahiri ambaye hatuna wasiwasi naye. Timu ambayo Mheshimiwa Rais amesaidia kuiunda kwenda kusimamia eneo hili la Mipango na Uwekezaji imejaa watu mahiri. Hatuna wasiwasi na utendaji wa Katibu Mkuu, Tausi Kida, hatuna wasiwasi na Katibu wa Tume ndugu yetu Lawrence Mafuru, pia hatuna wasiwasi na Ndugu Nehemia Mchechu ambaye ni Msajili wa Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pia ina jukumu la kutazama Dira ya Maendeleo ya Taifa letu na miongozo yote. Napenda leo kushauri maeneo machache hasa kwenye upande wa Sera. Nitagusia kwenye eneo la elimu, kilimo kidogo na pia kwenye ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera yetu ya Elimu ambayo imehuishwa hivi karibuni, bado inahitaji kufanyiwa maboresho zaidi na hasa iwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba yote yaliyoingia katika sera yanakwenda kutekelezeka, kwa sababu tunapozungumza elimu tunazungumza rasilimaliwatu, hapa ndipo tunapoandaa rasilimaliwatu ambao watakwenda kuwa watumishi wa maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tuwe na sera ambayo inaweza ikazalisha Watanzania ambao watakuja kuwa wazalishaji wazuri kwenye Taifa hili ambalo sasa hivi vijana ni wengi zaidi kuliko makundi mengine. Kwa maana vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa, sasa ni muhimu sana tukaiwezesha kwa kuipatia elimu na maarifa ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo mahususi ambalo nataka kulishauri hapa ni kuona kwamba bado tunazalisha sana watumishi katika kada ya Ualimu. Kada hii imeshakuwa *saturated*, haiwezi tena, ni wengi sana wako mtaani ambao hawajaajiriwa, lakini bado vyuo vyetu vinaendelea kuzalisha tena walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaiomba sasa Wizara hii ya Mipango ilitazame hili jambo kwa mapana, kwamba, kuna vyuo 35 vya Serikali ambavyo *traditionally* vinazalisha walimu ngazi ya *Certificate* na ngazi ya *Diploma*. Je, kuna umuhimu wa kuendelea kuzalisha kwa wingi tena katika ngazi ya *Degree*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa chuo kama Chuo cha Kilimo - *SUA* kuwa na udahili na wanafunzi wa Ualimu? Hili ni lazima tulitazame. Mimi nadhani ni vizuri mipango ikatuelekeza tuwe na wanafunzi wengi katika ngazi ya *Degree* au *Diploma* kwenye vyuo vya aina ya *DIT*, taasisi ya teknolojia. Huku ndiyo tuwe na wanafunzi wengi ambao hata baadaye hawatatusumbua kulazimika kuwatafutia ajira kwa sababu wanaweza wakajiajiri wenyewe kulingana na maarifa ambayo watayapata kupitia vyuo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tume hii itusaidie. Tumetoka kwenye sensa, sensa inatupa *projection* ya idadi ya watu baada ya muda fulani. Kwa hiyo, lazima tujue pia kwamba leo baada ya miaka mitano tutahitaji walimu wangapi? Kwa hiyo, idadi hiyo ndiyo tujue tutazalisha kiasi gani cha walimu ili waweze kuziba hilo pengo ambalo tunakusudia. Tukiendelea kuwazalisha, halafu hatuna ajira na hawana shughuli mbadala watakazokuja kufanya tunakuwa tunaharibu hiyo rasilimaliwatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni rasilimali ya ardhi; Sera yetu ya Ardhi ni ya mwaka 1995 sitaki kuamini kwamba imepitwa na wakati, lakini imepitwa na wakati. Japo bado tunaaminishwa kwamba Sera yetu ya Ardhi ni Sera bora ambayo nchi nyingine zinakuja kujifunza, lakini hebu tuambiane ukweli. Haya matatizo ambayo tunayaona Waziri wa Ardhi anahangaika nayo kila siku, bado sitaki kuamini kwamba sera yetu ni bora. Lazima hili nalo tulitazame, kwa sababu tunapozungumza uwekezaji wowote, utafanyika juu ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ardhi yetu mpaka leo haijapimwa, ndani ya miaka 60 ya uhuru tuko chini ya 50% ya ardhi yote iliyopimwa, maana yake bado tuna tatizo. Tungependa kuona mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ardhi ipimwe, hasa vijijini ambako ndiko kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji, lakini ndiko ambako sasa uwekezaji unaelekea huko kwa sababu tunakwenda kuwekeza kwenye eneo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwamba ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi ambazo ndiyo hizi sera tunazozizungumza na mwisho wa siku tunahitaji *good governance*. Tunapokuwa na *good governance* maana yake tunaondoka sasa kwenye haya matatizo ya migogoro ya ardhi isiyokwisha kila mara. Ni vyema sasa eneo hilo nalo Mipango ikalitazama kwa mapana na marefu kwa ajili ya kulinda uwekezaji. Hatutarajii kwamba tuwe na wawekezaji ambao wanakumbana na kadhia hii ya umiliki wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwenye kilimo. Nimetazama hapa, Sera ya Kilimo ni ya mwaka 2012. Hawa wamejitahidi, ni *current* sana. Hata hivyo, tunawaomba sasa wawe na *masterplan* ya mkakati mahususi wa kusukuma ajenda za kilimo. Miongoni mwa mikakati hiyo iwe sasa kukiweka kilimo katika umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana hapa, hizi mvua ambazo tunaendelea kuhangaika nazo, zimeharibu miundombinu ya barabara, majengo na kadhalika. Tungekuwa na sera madhubuti katika eneo zima la umwagiliaji ya kuvuna haya maji ya mvua inawezekana mwezi wa saba au wa nane tungejikuta tuko kwenye kiangazi ambacho tunahitaji maji ambayo leo yamekuwa ni adha kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, mpaka sasa hivi asilimia mbili tu ya ardhi yetu ambayo inatumika katika kilimo ndiyo ipo katika umwagiliaji, ni asilimia ndogo sana. Miaka 60 ya uhuru tunazungumzia asilimia mbili. Ni vyema sana tukawekeza hapa, tukawa na mipango ya muda mrefu kwenye Tume ya

Umwagiliaji, tukaiwezesha tuwe na mpango endelevu angalau wa miaka mitano mitano kuhakikisha kwamba tunaongeza eneo la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kuongeza eneo, ni lazima tuangalie pia uwezekano wa kutumia maji katika maziwa yetu. Tunalo Ziwa Victoria, tumechukua maji kwa ajili ya shughuli za majumbani. Siyo dhambi maji ya Ziwa Victoria na yenyewe tukayabadilisha matumizi tukayapeleka kwenye shughuli za kilimo. Siyo dhambi tukayafanya maji ya Ziwa Victoria yakatumika kwenye shughuli za ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Ziwa Tanganyika linazunguka karibu mikoa mitatu. Itakuwa ni ajabu sana kama na mikoa hii nayo tutasubiri mpaka mvua za vuli na masika ndiyo twende tukalime. Tutumie maji ya Ziwa Tanganyika kwa ajili ya shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, hapa Mheshimiwa Kitila kuna jukumu kubwa sana la kufanya kwa sababu hili tatizo kubwa la ajira ambalo tunalizungumza ni kwa sababu hatujaweka mipango yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuweke mipango yetu katika ardhi, tuweke mipango yetu katika kilimo. Huku kukiwa kumeimarika, hatutaona Mtanzania anazunguka na bahasha kutafuta ajira kwa sababu tayari wanaweza wakajiajiri kupitia kilimo. Hatutaki kiwe kilimo hiki cha kutangatanga ambacho hakiaminiki. Tunataka kilimo kinachoaminika, ndiyo maana tunasisitiza kwamba tutengeneze mipango katika eneo zima la umwagiliaji, hata kuihusisha Sekta Binafsi katika eneo zima la kujenga miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo dhambi kama kuna watu wenye uwezo wa kuwekeza katika eneo hili la kilimo kwa maana ya kujenga miundombinu. Naamini Watanzania wapo tayari kulipia kama ni kwa gharama ambazo zinaeleweka. Pia hata kuifanya Tume ya Umwagiliaji kuwa ni wakala.

Mheshimiwa Spika, tunazo wakala; *TARURA*, *RUWASA* zinafanya kazi zinazofanana na hiyo. Kwa nini hii Tume ya Umwagiliaji tusiifanye kuwa ni wakala na ikafanya kazi hii

kuhakikisha kwamba wakati wote wananchi wanaweza kupata ardhi ya kutosha na kulima kwa msimu mzima wa mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo nataka kuchangia ni suala zima la uwekezaji. Katibu Mkuu wa Chama alivyokuwa Mbarali juzi ameagiza shamba la Mbarali lipewe kwa wananchi. Tunaiomba Serikali ipokee agizo hili kwa sababu tunajua kule kuna shida. Pokeeni agizo hili lakini mhakikishe mnalinda maslahi ya mwekezaji.

Mhshimiwa Spika, eneo lile ambalo halitumiki, basi wananchi wapewe ili waweze kujikimu na kuendesha maisha yao kwa sababu tunaamini uwepo wa mashamba yale ya Mbarali umesaidia kwa kiasi kikubwa sana sisi kama Taifa kupunguza kuagiza mchele kutoka nje. Sasa hivi mchele wetu pia unaweza ukapenya katika mipaka mingine kwa sababu tunazalisha mchele mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia leo kwenye Wizara (Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji). Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Mheshimiwa Waziri hapa amesema, nasi kule Manyoni tunasema, miradi mingi sana tumepata Jimbo la Manyoni Mashariki ya mabilioni ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa heshima ambayo ametupatia na ameiweka katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Namshukuru sana

Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Spika, natambua amepewa Wizara hii ikiwa changa lakini tunaona ameweka mifumo na inaenda vizuri. Namshukuru sana Msajili wa Hazina, ndugu yangu Mchechu, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, Mkurugenzi *EPZA* na Mkurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumekuwa tuna-*interact* na hawa Wakurugenzi, Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Ofisi ya Waziri. Tunaona kuna mambo mazuri ambayo yatatokea hapo mbeleni hususani katika uandaaji wa dira hii ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili napenda kuchangia leo. Eneo la kwanza nitachangia kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma, pia kama muda utaniruhusu, nitachangia kuhusu fursa za uwekezaji pale Manyoni.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Serikali imewekeza zaidi ya shilingi trilioni 76 katika mitaji katika mashirika mbalimbali ambazo zimewekezwa na Serikali. Maana yake ni kwamba, kama tutasimamia vizuri, huu uwekezaji wa shilingi trilioni 76 ambao umewekezwa na mashirika yetu mbalimbali *return on investment* (tija/faida) ya huu uwekezaji unaweza ukaonekana. Kwa hiyo, hatutaweza kulalamika kwamba tumeshindwa kujenga labda zahanati, kukamilisha maboma pamoja na kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana ya kuanzisha hii Wizara ya Mipango na Uwekezaji ni kutaka sasa ije isaidie katika huu uwekezaji ambao Serikali inafanya, lakini vilevile kusimamia uwekezaji katika sekta binafsi. Hivi karibuni, wote ni mashahidi, tulitakiwa kuleta muswada ambao unahusu sheria ya usimamizi wa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, mimi ni muumini wa hii *reform* na bahati nzuri Mheshimiwa Rais amekuja na zile *4Rs*. Katika zile *4Rs*, mojawapo ya *R* ni *Reform*, na mojawapo ya eneo ambalo

tunahitaji kulifanyia kazi ni *Reform*, mabadiliko katika Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kusema kwamba Serikali imewekeza zaidi ya shilingi trilioni 76 na ofisi ambayo inasimamia uwekezaji ni Ofisi ya Msajili wa Hazina. Ofisi ya Msajili wa Hazina ukiiangalia ni ofisi ya siku nyingi sana. Kimsingi, naweza nikasema imepitwa na wakati. Kuna mambo mengi sana ambayo tunahitaji kuyaboresha katika Ofisi ya Msajili wa Hazina ili awe na meno yatakayomwezesha kusimamia vizuri huu uwekezaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana tunapotosha. Huko zamani uwekezaji ulikuwa haujafika shilingi trilioni 76, lakini sasa hivi tunaongelea *huge amount of investment*, shilingi trilioni 76 ambayo Serikali imewekeza. Kwa hiyo, tunahitaji jicho la karibu kwa hii mifumo mizuri ambayo itahakikisha kwamba huu uwezekaji sasa unakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? Bado naendelea kuishauri Serikali ikamilishe ule utaratibu wa kuleta Sheria ya Mabadiliko ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Bado naweka msisitizo kwamba tunahitaji mabadiliko ya sheria ya uwekezaji katika mitaji ya umma. Nakumbuka Mheshimiwa Profesa Kitila alianza huu mchakato wa kuleta ile sheria.

Mheshimiwa Spika, ile sheria itatupa mambo mawili; eneo la kwanza tunahitaji kubadilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina; Ofisi ya Msajili wa Hazina imepitwa na wakati, tunahitaji kuja na taasisi kubwa, mamlaka, *Public Investment Authority* ambayo kwa kweli itaweza kusimamia haya mashirika mengine ili huo uwekezaji wa shilingi trilioni 76 uwe na tija.

Mheshimiwa Spika, hizo ni fedha za wananchi, tuna uhakika gani hizo fedha zinasimamiwa vizuri? Tunahitaji kuwa na mamlaka ambayo itakuwa na meno, ambayo itakuwa na nguvu ya kuhakikisha kwamba sasa uwekezaji ule ambao tumeufanya kule ambao Mheshimiwa Rais ameufanya, unaleta tija na hatimaye hizo fedha zirudi Serikalini ili zikasaidie kwenye suala la Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami naendelea kusisitiza na kumkumbusha Mheshimiwa Profesa Kitila, najua hili hawezi kushindwa. Atuletee Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tupitishe ili tuhakikishe kwamba tunaenda kusimamia fedha za wananchi ili tija iweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, tumewekeza kwenye maeneo mengi sana, ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, lakini Watanzania ni mashahidi. Tunahitaji kumsaidia Mheshimiwa Rais ili kuhakikisha kwamba zile fedha na yale mashirika yaliyowekeza yanakuwa yana tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, tuna taasisi nyingi zinatamani kuwekeza lakini hazina mitaji. Kuna fursa nyingi za uwekezaji na kuna taasisi nyingi zina maeneo *potential* ya uwekezaji, lakini hayana mitaji. Sasa kwenye ile sheria, eneo mojawapo ambalo nashauri liwekwe ni kuanzisha mfuko wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, tunapokuwa na ule mfuko wa uwekezaji itakuwa ni sehemu ya kutafuta fedha na kuziweka kwenye ule mfuko, *then* zile taasisi ambazo hazina uwezo wa ku-*raise* fedha zitaenda kwenye ule mfuko, zitapewa kwa mfumo wa *revolving fund*. Hata kama kutakuwa na *interest* ndogo, lakini *at least* wawe na uhakika wa kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza hili, hili ni eneo muhimu kwa sababu lazima tuzijengee uwezo taasisi zetu ziweke kuwekeza. Bado narudia kusisitiza, tunahitaji uwekezaji wenye tija *(return on investment)* ambayo itakuwa na tija ili iweze kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni fursa za uwekezaji Manyoni. Manyoni tuna fursa nyingi za uwekezaji. Nimetangulia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kule kwetu Manyoni. Sisi Manyoni tuna maeneo mengi ya uwekezaji. Hawa ndugu zangu wa *EPZA* wana eneo la zaidi ya ekari 2,600 ambalo walilikamata tangu mwaka 2013. Hili eneo ni *potential* kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nawakumbusha watu wa *EPZA* kwamba hili eneo mnalo ingawa fidia mlikuwa hamjatoa. Haya ni maeneo *potential*, naomba mtafute wawekezaji waje wawekeze. Pia halmashauri imetenga eneo la zaidi ya ekari 250 kwa ajili ya viwanda mbalimbali kama vile viwanda vya korosho. Vilevile kule sisi tunafuga sana mifugo na hivyo kujengwe viwanda vya maziwa na kadhalika. Haya ni maeneo ambayo Mheshimiwa Profesa Kitila anahitaji kuvutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Majiri tuna ekari zaidi ya 100 kwa ajili ya kuwekeza viwanda vya chumvi. Nimeuliza sana swali hili Bungeni, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara anafahamu na bahati nzuri walishawahi kufika. Kuna *potential* kubwa sana ya uwekezaji kwenye suala la viwanda vya chumvi kule Manyoni hasa katika Vijiji vya Kinangali, Mpandagani na Majiri. Mheshimiwa Waziri, najua hili hawezi kushindwa. Namwomba sasa atafute wawekezaji, awalete Manyoni, maeneo yapo, sisi tutatoa maeneo ili wawekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba kila uwekezaji mpya huchochea uchumi mpya kukua, lakini vilevile inakwenda kuchagiza ongezeko la kodi ambalo linaenda kuchangia katika maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uwekezaji, tunaangalia mambo matatu. Tunaangalia miradi inayosajiliwa, ajira zinazotokana na miradi hiyo iliyosajiliwa pamoja na mtaji.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ukurasa wa 10, ameonesha mwenendo wa uwekezaji nchini kuanzia mwaka 2020 – 2023. Nasema kweli, kwa mwenendo ule nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika miradi iliyosajiliwa na *TIC* kati ya mwaka 2020 – 2023, mwaka 2020 miradi ilikuwa 207 na ikapanda mpaka 2023 ikafikia miradi 526. Natambua kwamba mwaka 2019/2020 kulikuwa na shida ya *COVID* ndiyo maana hii miradi ilikuwa siyo mingi, lakini tangu kuapishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwezi Machi, 2021 amefanya kazi kubwa sana ya kuongeza miradi iliyosajiliwa *TIC* kati ya mwaka huo 2020 – 2023. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa miradi hiyo imeweza kuchagiza mitaji kutoka mwaka 2023 dola za Kimarekani 1,092.7 hadi kufikia dola za Kimarekani 5,704. Vilevile idadi ya ajira ziliendelea kuongezeka kutoka 17,385 mwaka 2020 hadi kufikia 137,010. Naweza kusema kwamba kwa takwimu hizi Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba ameendelea kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara, kitu cha kwanza napenda kuishauri Wizara iendelee kufanya ufuatiliaji katika miradi ambayo imesajiliwa. Kwa hiyo, muimarishe suala zima la ufuatiliaji wa miradi hiyo ambayo imepatikana. Vilevile mfanye kazi kwa kushirikiana na sekta pamoja na Wizara nyingine kama vile Wizara ya Madini, Wizara Kilimo, Wizara TAMISEMI, Wizara Utalii, Wizara Viwanda na Biashara pamoja na Wizara Nishati.

Mheshimiwa Spika, natambua kabisa kwamba kulikuwa na changamoto ya kutokupatikana kwa umeme, lakini na sehemu nyingine ambazo umeme ulikuwepo, ulikuwa unakatikakatika. Kipekee, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kwa

kazi nzuri aliyoifanya ya kukamilisha miradi ya umeme ambayo itawezesha kutatua changamoto hii. Nampongeza kwa kukamilisha mradi mkubwa wa umeme kama wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania tunaamini kwamba kwa kukamilika mradi huu, kutachochea uwekezaji na pia itaondoa kabisa zile changamoto ambazo zilikuwa zinatokea kwenye viwanda ambavyo vimeshaanzishwa na vitakavyoanzishwa. Hivyo basi, tutaenda kuchagiza uchumi wetu na vilevile kuvutia wawekezaji kwa kuwa na nishati ya umeme ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye mikoa na halmashauri zetu. Kule kwenye mikoa yetu na halmashauri zetu kuna idara za uwekezaji, viwanda na biashara; na ziliwekwa kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji pamoja na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo katika maeneo yetu nchini kwetu. Kule mikoani kuna Wakuu wa Mikoa, kuna Wakuu wa Wilaya, na kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kote huko kuna hizi idara za uwekezaji wa viwanda na biashara.

Mheshimiwa Spika, kuna fursa nyingi ambazo zinatoka kwenye wilaya na mikoa yetu ambazo zingeweza kusaidia kuchagiza katika uwekezaji. Hivyo basi, nilikuwa nawashauri Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wasimamie vizuri fursa ambazo ziko kwenye maeneo tunayotoka kule wilayani na mikoani ili kuweza kuisaidia Serikali katika kufungua mwanya mkubwa wa uwekezaji katika nchi yetu. Hii ni kwa sababu wao ndio wanaziona moja kwa moja fursa ambazo ziko katika wilaya zetu kwenye maeneo ya utalii, kilimo na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa kila Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kuhakikisha kwamba anaisaidia Serikali katika kutambua fursa hizo za uwekezaji sambamba na kuboresha miundombinu ambayo itasaidia kurahisisha uwekezaji wa haraka. Kwa mfano, kuangalia barabara zetu, kuangalia viwanja vya ndege ambavyo sehemu husika vinahitajika viwepo ili kuvutia wawekezaji waweze kuja kuwekeza na kuweza kukuza uchumi wetu. Vilevile tupate kodi ambayo itasaidia katika kutatua kero na katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, halafu Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba hii muhimu sana ya Wizara ya Ofisi Rais, Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)*. Pamoja na kwamba bado kuna mambo ambayo inabidi yaboreshwe, lakini natumia fursa hii kuwapongeza sana Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kazi kubwa ambayo wamefanya mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kituo hiki cha uwekezaji unaweza kukipima kwa mambo matatu makubwa. Jambo la kwanza ni idadi ya miradi ya uwekezaji ambayo kituo kinasajili. Jambo la pili ni kiwango cha ajira ambacho kinazalishwa na hiyo miradi ya uwekezaji na kipimo cha tatu ni kiwango cha mtaji ambacho uwekezaji huo unaingiza nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuangalia vigezo vyote hivyo vitatu ni kwamba hiki kituo cha uwekezaji tangu kianze, sasa hivi kina takribani miaka 27 kimeanza tangu mwaka 1996. Ukiangalia kwa wastani kwa miaka hii mitatu ambayo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeingia madarakani, kimekuwa na ongezeko kubwa sana la uwekezaji ambalo limefanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, idadi ya miradi ya uwekezaji kwa kipindi hiki, kituo hiki kimeweza kusajili miradi 1,004 kuzalisha ajira za moja kwa moja 248,000. Kutokana na uwekezaji huo, kituo hiki wameweza kuingiza nchini mtaji wa moja kwa moja *(direct foreign investment)* wa takribani Dola za Kimarekani bilioni 15. Wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kuna mambo ambayo inabidi yaboreshwe. Sisi kama Kamati tulifanya ziara ya kutembelea baadhi ya wawekezaji ambao wamesajiliwa na kituo hiki cha uwekezaji na wameingiza mitaji yao hapa nchini. Kwa ujumla, kazi ni nzuri na mambo yanakwenda vizuri. Ila kuna mambo madogo madogo ambayo hawa wawekezaji wali-*raise concern*. Kwa mfano, maeneo ya kikodi kama vile *VAT Return* na punguzo la *Import Duty* ambayo walikuwa wameahidiwa, yamekuwa yakichelewa sana.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo kubwa ambalo naungana na Mheshimiwa Neema Mgaya ambaye naye amelizungumzia, la kutokuweka vipaumbele katika kupeleka miundombinu muhimu kwenye maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, tumefika pale Kibaha, unakuta mwekezaji ameweka *billions of dollars* kwa ajili ya kutengeneza zile kongani za uwekezaji, *industrial shade* na kadhalika, lakini unakuta ana muda wa miezi kadhaa anahangaika umeme ufike pale kwake lakini inashindikana; anahangaika maji yafike kwake, lakini inashindikana; anahangaika barabara nzuri ifike, lakini jambo linakuwa gumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali hapa ni kwamba, miundombinu muhimu ya kuwawezesha wawekezaji waanze kufanya shughuli zao kama umeme, maji, barabaraba, yapewe kipaumbele kupelekwa maeneo ambayo wawekezaji wamewekeza dola zao ili uzalishaji uweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, inabidi tuangalie faida za uwekezaji, tusiziangalie kwenye *angle* ya kodi peke yake, kwani faida za uwekezaji tunaweza tukazipata kwenye maeneo mengine kama ajira au *local contents*. Kwa hiyo, siyo lazima sana kumbana mwekezaji na wakati mwingine wawekezaji wanashindwa kwa sababu ya masharti ya kikodi, lakini kumbe ukiruhusu huo uwekezaji uje ndani, hata kama utakosa kwenye kodi, lakini utapata kwenye ajira na utapata kwenye *local contents*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la muhimu sana ni ile *skills transfer/knowledge transfer,* kwamba wawekezaji wanapokuja wanakuja na teknolojia mbalimbali za kuzalisha bidhaa mbalimbali. Kwa hiyo, wananchi wetu wanapata fursa ya ku-*acquire* hizo *knowledge* na *skills* (ujuzi) ambao ni faida kubwa pengine kuliko tungetazama tu kodi na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye eneo la uwekezaji kwenye maeneo ya Jimbo langu la Bukene na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Pale sisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega tulitenga eneo la uwekezaji, tuna takribani ekari 46,000. Kuna eneo linaitwa Kisasiga pale kwenye Kata ya Igusule, mpaka sasa hivi tulishalipima, lina rutuba nzuri, linaweza kuzalisha mazao kadhaa, lakini mpaka leo ekari 46,000 zimekaa *idle,* hazitumiki.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaalika Wizara ya Kilimo, njooni Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, njooni Kisasiga, kuna ekari 46,000 hazitumiki kuzalisha chochote. Kwa hiyo, hii mipango ya *block farms* ya ukulima mkubwa na wapi, tuna Serikali inahangaika kupata maeneo, lakini kuna maeneo ambayo tayari yapo makubwa yanahitaji tu uwekezaji pale ili yaanze kuzalisha. Kwa hiyo, Wizara ya Kilimo njooni Kisasiga Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, kuna ekari 46,000 zinafaa kwa *block farm* na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tuna mabonde makubwa ya umwagiliaji ambayo Wizara ya Kilimo pia tunawaalika waje kwa ajili ya kufanya uthamini na kuanza Miradi ya Kilimo. Kuna mabonde makubwa maeneo ya Budushi, kuna mabonde ya Manonga huko Kata za Sigili – Mwangoye, kuna mabonde makubwa Mambali – Kahamanhalanga – Kasela ambayo yapo *idle* yanafaa kwa miradi mikubwa ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji iangalie kwamba tunayo ardhi na mabonde makubwa ambayo yangeweza kutumika kikamilifu tungeweza kupata uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwamba Serikali iendelee kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Ujenzi wa Reli ya

Kisasa *(SGR)* ambayo pia inapita jimboni kwangu. Tunajua faida ya Miundombinu ya Reli kwa uwekezaji. Wawekezaji wanataka *facility* za usafiri kwa ajili ya kusafirisha bidhaa, kwa ajili ya kusafirisha *raw material.* Kwa hiyo, ujenzi wa reli hii hauna shaka yoyote kwamba unakwenda kuongeza na kuimarisha uwekezaji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye kipande cha Tabora – Isaka ambacho ukamilishaji wake umefikia asilimia tano, kuna shida kubwa ya wale wananchi waliopisha maeneo ili reli ya *SGR* ijengwe, hadi sasa hawajalipwa fidia. Wananchi wanadai fidia yao, na kimekuwa ni kilio, kwa sababu ni muda mrefu zaidi ya mwaka wananchi wamepisha mashamba yao, hawajalipwa fidia. Masika imefika, hawana hela ya kununua mashamba mengine, kwa hiyo, wamepata kwa tabu sana kipindi hiki cha masika mpaka leo ninavyoongea.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Uwekezaji, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Miundombinu ili kuharakisha bajeti kutoa fedha ili wananchi waliopisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa, walipwe fedha zao, walipwe fidia yao kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono suala la kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuendelea kuchangia kwenye hisa zetu za bomba la mafuta na ukamilishaji wa *process* nzima ya bomba la mafuta. Niseme tu kwamba, hapa changamoto kubwa ni *local contents* kwamba mambo mengine kwa mfano suala la fidia, kama kuna mradi ambao umeendesha zoezi la fidia kwa wananchi vizuri sana mo huu Mradi wa Bomba la Mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wananchi waliopisha maeneo yao wamelipwa fidia ipasavyo na hakuna malalamiko yoyote isipokuwa inabidi tuendelee kuboresha eneo la *local contents* kwa maana ya ajira kwa wazawa hasa wanaozunguka eneo lile. Wale ambao hawana *skill* sana, wananchi wa kawaida, wapate ajira za vibarua.

Mheshimiwa Spika, *local contents* nyingine, ni kwa wale wazabuni ambao wanatoa huduma katika eneo lile, basi wawe ni

Watanzania wenye uwezo wa kutoa huduma ile na hasa wale ambao wanakaa maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hiyo, naunga mkono hoja kwa 100%. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza na Mheshimiwa Godwin Kunambi, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kurudia pongezi zilizotolewa na wengi. Shukurani kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuunda Tume ya Mipango na kuunda hii Wizara ya Mipango na Uwekezaji ambavyo vyote ni taasisi, ameviweka chini ya ofisi yake. Tunaamini kwamba taasisi hizi zimeweza kuanza kutekeleza majukumu yake kwa kasi ya juu sana kutokana na usimamizi shupavu wa Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo pamoja na timu yake, Dkt. Kida, Lawrance Mafuru pamoja na Mchechu na wafanyakazi wote wa pale kwenye Wizara hii mpya.

Mheshimiwa Spika, kama ungeniambia niseme majumuku ya hii Tume ya Mipango ni nini? Yameorodheshwa 20, lakini naweza kusema ni *coordination* ya Mipango ya Serikali; ni *coordination* ya Sera za Serikali kwenye sekta mbalimbali. Kila sekta inakuwa na *interest* zake. Kwa hiyo, kila sekta inataka ipate zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu ambaye ni *neutral,* au taasisi ambayo ni *neutral* ambayo Wabunge walisisitiza iundwe, ni Tume ile, kwa sababu haina sekta. Kazi yake ni kuhakikisha kwamba *resources* zinakuwa *allocated in a balance manner* ili uchumi ukue *in a balance way*. Kuwe na *both, social and economy balance. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta za jamii zisipokee *too much* zikasahau kwamba ili sekta za jamii ziweze kuzalisha huduma zile

ambazo zinahitajika za afya, elimu na kadhalika, ni lazima zipate fedha kutokana na sekta za uzalishaji, sekta za kilimo, viwanda na huduma mbalimbali kwa jamii, pamoja na sekta nyingine. Kwa hiyo, naamini kwamba sasa tumepata chombo ambacho kitatuwezesha kututengenezea mipango ambayo ina tija kwenye maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchangiaji wa mwanzo alisema tusianze tena kuongeza walimu na kadhalika, lakini kazi ya mipango ndiyo hiyo, kuona kwamba ni wapi ambapo sasa tulenge rasilimali yetu ili iweze kuchaji maeneo yale ambayo yamekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna dhana moja kwamba ili uweze kwenda sawasawa, ni lazima uweze kusema nalenga kitu gani? Inavyoonekana, mwelekeo wa Tume *so far,* au wa Wizara, zaidi unalenga wawekezaji wakubwa kutoka nje, na wawekezaji wa ndani wakubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kwamba nchi hii haiwezi kutoboa bila kulenga *SMEs* na wawekezaji wadogo wadogo, ambao ndiyo kule chini tuliko, ndiyo kule kwenye halmashauri zetu tuliko, wawekezaji wadogo; kuona ile mikopo ya wanawake, vijana na walemavu isimamiwe namna gani ili iweze kuleta tija? Iendelee kutolewa kwa mbinu zipi? Ni kitu gani cha ziada kifanyike ili mikopo inayotolewa kwa kupitia *empowerment funds* zote na kwa namna nyingine ambayo mabenki yanatoa ili iweze kuleta tija kwenye uchumi wetu na fedha yetu iwe na thamani na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, naomba katika vitengo vyote, na sijaona kama kuna kitengo kwenye hii Wizara ya Mipango kinachoshughulika na wawekezaji wadogo wadogo na *SME*. Ukishakuwa nacho na kikatumia sasa wale Maafisa Mipango na Maafisa Uwekezaji kwenye halmashauri, tutaweza kuhamasisha uwekezaji mdogo mdogo na kufanya *incubations* ili watu waweze kutekeleza miradi midogo midogo ambayo itakuwa ina-*hide* kwenye mnyororo kwa thamani *(value chain)* wa hawa wakubwa wakubwa ambao Mheshimiwa Rais amefanikiwa kupata.

Mheshimiwa Spika, ninaamini pia kwamba hawa wawekezaji wanaosajiliwa kwenye *TIC,* pia hiyo orodha ingekuwa inachapishwa ili tujue ni wapi wanaenda kuwekeza, ili nasi tuanze kujipanga, wanapokuja kuwekeza tuweze ku-*supply* vile vitu ambavyo wanahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri hilo ni la msingi sana na ninaamini pia kwamba suala zima la *PPP* liwekewe mkazo kwenye Wizara hii ambayo ndiyo inaenda kusaidia kuona kwamba wakubwa na wadogo wanapata msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, pia niseme kwamba kuna ile *investments forums* ambazo zilikuwa zinafanyika, zilikuwa zimeanza kwenye mikoa na kwenye wilaya mbalimbali na naona zimefanyiwa tathmini na Tume. Naamini kwamba hizo nazo sasa zianze kuhimizwa ili ziweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ni *think tank,* kwa sababu ina-*coordinate* vitu vingi na inatakiwa iwe na utaalamu, iwe na watu ambao inawasaidia katika kufanya utafiti. Wasifanye utafiti wenyewe, wawe na Taasisi za Utafiti. Sasa kuna Taasisi za Utafiti kama *REPOA*. Na-*declare conflict of interests,* mimi ni *Board Member* wa *REPOA*.

Mheshimiwa Spika, *ESRF*, *REPOA* na Taasisi nyingine hata Vyuo Vikuu kama Sokoine wana taasisi na Idara za Tafiti. Sasa watenge fedha kwa ajili ya utafiti. Kwa mfano taasisi hizi ninazotaja, hiyo sarafu, wanapata kidogo, lakini wanapata fedha za nje, ni wafadhili ndiyo wanafadhili utafiti ambao unaenda kusaidia Serikali hii kutengeneza sera za kiuchumi na kutengeneza mipango ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, kwa nini hawajatenga fedha kwa ajili ya taasisi za utafiti? Naomba sana, sijawahi kushika shilingi ya Waziri, lakini nitashika shilingi kama hatasema kwamba ametenga kiasi gani cha fedha ambazo zitaenda kugawa kwa hizi taasisi za utafiti ili zimsaidie yeye na zitusaidie sisi Wabunge pia.

Mheshimiwa Spika, watu wanakuja kutusaidia kutupa *percentage* kwenye Kamati ambazo hata wazungu hawawezi

kutengeneza. Wale wanakujanazo wanatuelewesha namna gani mapato yanaweza kukua, kwa nini hatuwapi fedha? Naomba sana jamani, naomba sana Mheshimiwa Waziri na Profesa Kitila uende ukaangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishangaa kidogo, huwezi kuwa na mpango ambao hauna bajeti, yaani bajeti na mpango zinaenda sambamba, zile *process* zinaenda sawia. Ukiniambia kwamba msimamizi wa Tume ya Wizara hii ya Uwekezaji na Mipango na Tume yuko kwenye; sijui namna gani unapita kwenye Kamati ya Bajeti. Kwa sababu mimi niko kwenye Kamati ya Bajeti na sijaona chochote na nilikuwa nasita hata kuchangia, lakini nimeona nichangie tu kwa sababu ni vizuri kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri kutafutwe namna yaku-*link* hapo ili Kamati ya Bajeti iweze pia kupata nafasi ya kuona mipango hii na ndiyo watu wanaweza pia wakajua bajeti inaweza kuwa ya namna gani? Siyo tu ya Wizara, lakini bajeti kwa ujumla na mipango ya kutekeleza mipango hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kuona kwamba *blue print* inatekelezwa kwa ujumla na inatekelezwa vizuri, na inawasilishwa kwenye wasilisho. Hata hivyo, nafikiri ni wakati sasa wa kusema kwamba hii *blue print* tui-*review* tena, tuone kwamba ni kitu gani bado kimebaki? Ni kitu gani kimefanyika, lakini kimefanyika kinyume ya namna tulivyotarajia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupunguza tozo siyo kusaidia uwekezaji. Unaweza ukatoa tozo zote na usipate hata mwekezaji. Kuna vitu vingine ambavyo vinahitajika ili uwekezaji uweze kuonekana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anayehusika aone namna gani pia ya kurahisisha na kuelimisha umma ni kitu gani kimefanikisha kwenye hili la kurahisisha uwekezaji na kuhamasisha au kupunguza gharama za uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi pia kuona kwamba Tume chini ya Mheshimiwa Mafuru imeanza sasa kufikiria upya namna ya ufuatiliaji, kwa sababu ufuatiliaji na tathmini ndiyo jambo kubwa

pia katika kuhakikisha kwamba fedha inapata thamani. Sasa kama kweli Tume inafikiria namna hii, maono yake ni kwamba tutengeneze mifumo ya ufuatiliaji. Mradi ukiingia tu kutekelezwa kunakuwa na *dashboard* ambayo hata Mheshimiwa Rais mwenyewe anaweza akaona *dashboard* kwamba mradi huu sasa umefikia hapa na hapa na hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuliona juzi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alituonesha pale. Unaenda pale unaangalia Bwawa la Nyerere, huna haja ya kwenda kule, unaliona linavyotiririsha maji na linavyozalisha umeme. Ni mambo ya namna hiyo tunataka kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukafungamanisha ule mfumo wake wa mradi na mifumo mingine, ukafungamanisha, na kila mtu anaweza akajiaonea, hata Spika akikaa ofisini kwake akaweza kuona akiingia kwenye *websites.* Siyo lazima atengenezewe mfumo wa ajabu, ni *web base system* ambao mtu ukiingia ukitaka kuona huo Mradi wa *SGR* umefika wapi? Unaingia, unaona. Mradi huu umezalisha kiasi gani au umekufa au ni kitu gani? Unaona. Naomba tuendelee kwa mawaidha hayo ili tuweze kurahisisha shughuli nzima ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba mawanda ya ufuatiliaji ya Tume yako *limited* kwa sababu ya *resource* ya watu pia. Sasa kuna miradi hii ya *Pension Funds,* miradi ya *Pension Funds* inafadhiliwa na nani? Kwa sababu ile miradi katika zile sijui shilingi trilioni 76 au 78 alizosema Mheshimiwa mwenzangu ni kwamba, nyingi pengine ni miradi ya *pension*.

Mheshimiwa Spika, sasa tunachouliza, inafadhiliwa na nani? *Return* kwenye *Assets* ya miradi ya *Pensions* ni *zero point something percent*. Mimi nashukuru kwamba sasa hivi *Registrar* Mheshimiwa Mchechu ameanza ku-*recruit* wasimamizi na Bodi kwa njia ya ushindanishi na ameanza kuwapa mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa huyu kwa sababu anajua mambo, naomba katika mafunzo anayotoa, achukue *top business schools, Harvard Business School* kuna wahadhiri wazuri, waletwe wawafundishe hawa watu namna ya kusimamia,

wanatoa *case studies* ambazo ni nzuri. Mkienda kule tutatoboa, *seventy six trillion is a lot of money.* Kwa hiyo, mimi naamini kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga…

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nilifikiri nitazungumza kidogo sana, lakini naona muda umeenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa, nakupa dakika moja, malizia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba basi tuangalie namna ya kutumia wahadhini kutoka kwenye *top business school,* kwa sababu ni njia pekee ya kuweza ku-*sharpen skills* za *management* katika nchi yetu na katika Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na uchangiaji, wapo wageni ambao wameingia hapa baada ya tangazo la kwanza la wageni.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na huyu ni Profesa Mamoun Homeida ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Udhamini Chuo Kikuu cha Madawa na Teknolojia kutoka Sudani, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 39 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambao ni wawekezaji kutoka makampuni mbalimbali hapa nchini, karibuni sana wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo anao wageni wengine tena ambao ni Wenyeviti na Makatibu 105 wa Umoja wa Wanawake Tanzania, Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi

na Wazazi kutoka Jimbo la Ubungo Kibamba na Wilaya ya Ubungo Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 95 wa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na uchangiaji. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache katika Wizara hii muhimu. Awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo ameonesha kufungua milango ya kiuwekezaji na anaendelea kufungua milango mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona jinsi ambavyo wawekezaji wengi wanaendelea kuingia nchini kwa ajili ya kuwekeza. Hii ni ishara tosha kwamba, Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweka demokrasia, na pia kuna utulivu na amani ya kweli inayosababisha wawekezaji hawa waone kwamba kuna tija kuwekeza hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila pamoja na timu yako nzima, kwa maana ya watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya. Nasema mnafanya kazi nzuri kwa sababu hii ni Wizara mpya na leo ndiyo kwa mara ya kwanza tunakwenda kupitisha bajeti yenu. Pamoja na huo upya, Wizara hii imefanya mambo mengi; imeweza kuipeleka Kamati ambayo mimi ni Mjumbe, kwenda kujionea kwa macho hizi kongani za viwanda ambazo wawekezaji wetu wanawekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara yetu, kama jinsi ambavyo mjumbe mwenzangu Mheshimiwa Zedi amesema, tumekutana na

mambo mengi sana sambamba na changamoto nyingi ambazo tumezikuta kule kwa wawekezaji wetu ikiwa ni pamoja na miundombinu. Huko katika kongani ambazo tulikwenda Mkoa wa Dar es Salaam kwa maana ya Kigamboni, Ubungo, Pwani kwa maana ya Jimbo la Kibaha Vijijini kule Kwala, tumekuta jinsi ambavyo miundombinu kwa kweli haijakaa sawa, hususan barabara, maji na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema umeme kwa sababu, kule kongani ni kubwa, nitaelezea baadaye jinsi ambavyo uwekezaji ni mkubwa. Umeme uliopo ni mdogo na hivyo, unahitajika umeme mkubwa ambao utekwenda kuwasaidia hawa wawekezaji waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Pamoja na changamoto hizo za miundombinu, lakini tumeona jinsi ambavyo Sheria yetu ya Uwekezaji iko vizuri, lakini ni kama haisomani na sheria nyingine zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya Uwekezaji…

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**TAARIFA**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na mchango mzuri ambao anaendelea nao Mheshimiwa Mbunge, napenda kumpa taarifa kwamba, pamoja na hiyo Kongani ya Kwala anayoizungumza, hilo Jimbo la Kibaha analolitaja kuna eneo lingine la uwekezaji lipo pale Soga. Eneo hili nalo lina tatizo la barabara kwenda kwa wawekezaji wa *Tanchoice*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nikawa nawaza, mbona makofi yamekuwa ya ziada? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba niipokee hiyo taarifa kwa sababu, kwanza kabisa inatoka kwa Mbunge wa Jimbo na analifahamu jimbo lake kuliko sisi ambao tumekwenda siku moja. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naendelea kuelezea Sheria za Uwekezaji. Nimesema Sheria za Uwekezaji hazisomani na sheria nyingine. Kwa mfano, mwekezaji akiwa China, Uturuki au Marekani, anapokuwa anasoma Sheria hii ya Uwekezaji, anasoma yale yanayohusiana na uwekezaji, lakini anapoingia nchini hapa sasa, tayari anaanza uwekezaji, ndipo anapokutana na sheria nyingine ambazo kimsingi, kama angekutana nazo *day one* anavyokuwa anasoma kwenye Sheria ya Uwekezaji ni aidha angeamua kuongeza mtaji aliokusudia au angeamua asubiri kwanza na vitu kama hivyo. Mwekezaji huyu anapoingia nchini anakutana na Sheria ya Ardhi, anakutana na Sheria ya Mazingira, mambo ya Uhamiaji, mara *OSHA*, *NEMC* pamoja na mambo ya *CEA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najaribu kuwaza na siku hiyo tuko kwenye ziara tuliuliza, hivi ni kwa nini hizi sheria zisisomane? Kwa mfano, mwekezaji anapokuwa anasoma ile Sheria ya Uwekezaji afahamu moja kwa moja, kwenye ardhi kuna nini? Kwenye suala la mazingira kuna nini? *OSHA* wanataka nini? Ili anapokuwa anaamua kuwekeza awe kweli amejifunga mkanda akijua ugumu au wepesi anaokwenda kukutananao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna hili suala la *CEA*. Natambua eneo lile kongani, mfano ya kule Kwala ambako tulienda ukiondoa ile ya Ubungo pamoja na Kigamboni, huu ni mpango mkakati wa Serikali kwamba, kule ni sehemu ya Kongani za Viwanda.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ni jukumu la Serikali kutenga lile eneo, wakati mnalitenga ni kwa nini hamkufanya hii *CEA*? Kwa sababu, mwisho wa siku ninyi ndio mnaomwambia mwekezaji tunataka ukae hapa. Huenda usingemwambia akae hapo, angeenda kuwekeza kwetu Kagera ambako labda hakuna hayo mambo ya kufanya *CEA* na vitu kama hivyo, lakini kama Serikali mkasema hili eneo tunaliweka maalumu kwa ajili ya Kongani za

Viwanda, ni kwa nini sasa gharama hizi zimwendee mwekezaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu tumekutana na wawekezaji wa namna hiyo. Hii inanipeleka sasa moja kwa moja kwa mwekezaji mmoja ambaye ana kiwanda kinachoitwa *Modern Industrial Park.* Mwekezaji huyu ni Mtanzania mwenzetu ambaye ameamua kuwekeza *a lot of money* kwenye hii kongani. Kiwanda chake ndani yake kuna viwanda 202, pia ajira rasmi kwenye hii kongani ni 30,000. Hizi ni ajira *direct,* lakini ajira ambazo ni *indirect* ni 200,000. Kwa hiyo, kwa jumla mwekezaji huyu anakwenda kutoa ajira kwa Watanzania 230,000.

Mheshimiwa Spika, pia mwekezaji huyu gharama za uwekezaji wake wote mpaka unakamilika ni shilingi trilioni 3.5. Hii ni pesa nyingi, ni uwekezaji ambao kama Serikali, kiukweli tunapaswa kuuangalia kwa jicho la pili, kuwaondolea kadhia ambazo walizieleza siku ile tukiwa kwenye ziara. Kwenye hii kongani huyu mwenyeji ambaye nimesema kwamba ni mzawa, ni Mtanzania, ameweza kufanya mambo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, wakati anaendelea kusubiri mfumo wa maji rasmi, ameweza kuchimba visima vingi sana pale. Ametengeneza barabara mwenyewe zenye kilometa 29, kwa maana ya ndani kwa ndani, ule mzunguko wa ndani na wa nje, kwa fedha zake yeye mwenyewe. Hii inaonesha ni namna gani mwekezaji huyu amedhamiria kabisa kuwekeza nchini, lakini anakumbana na hizi changamoto ambazo nimesema ziweze kufanyiwa kazi ili mwisho wa siku uwekezaji uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, katika kiwanda hicho wameenda mbali, wameweka kituo cha zimamoto, wameweka zahanati, wamefanya kila kitu na wakati wanasubiri umeme wa *TANESCO* ambao uko kwenye *process* nzuri sana, hapa ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kwani mwekezaji huyu ameamua kuvuta mwenyewe umeme wa Megawati 52. Kwa sasa, anahitaji ile kazi ya kupeleka umeme mkubwa zaidi iweze kufanyika, ili mwisho wa siku uwekezaji wake uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, tumeenda kwenye Kiwanda cha *SINO TANS*. Kiwanda hiki ndani yake kuna viwanda vidogo 200, ajira rasmi ni 100,000 na ajira ambazo ni *indirect* ni 500,000. Mradi huu mpaka unakamilika unakwenda kutumia dola za Kimarekani 300,000,000. *This is a lot of money. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema ni pesa nyingi kwa sababu, ukiangalia mazingira, siyo rafiki sana pamoja na jitihada zote ambazo tunaziona. Sasa naishauri Serikali, hizi changamoto ambazo nimezielezea, Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila sina wasiwasi na wewe, sina shida na wewe, najua nia yako njema ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, naijua vizuri sana. Hata kule katika ziara yetu tumeambiwa jinsi ambavyo una *PR* nzuri sana na wale wawekezaji. Hiyo haitatosha kama wawekezaji hawa hamtawapa vile vitu ambavyo mliwaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mliahidi vivutio vya kikodi. Mheshimiwa Profesa Kitila wakati tupo kwenye ziara wawekezaji wote tuliokutananao wameongelea suala hili. Mnawaahidi vivutio, lakini wakija mambo yanakuwa siyo shwari.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Profesa Kitila, wakati anakuja hapa ku-*wind up* anisaidie huu mkwamo wa kufanikisha jambo hili la vivutio vya kikodi, umekwama wapi? Atueleze amekwama wapi, ili kama Bunge sasa tuweze kusaidia kwa nia njema ya kuweza kutimiza ile nia njema ya Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niseme jambo moja lingine, katika nchi yetu tunatambua pamoja na jitihada za Serikali za kuleta ajira, bado suala la ajira ni changamoto kubwa sana, lakini wawekezaji hawa, nimesema na nimetaja kwa baadhi, unaweza ukaona jinsi ambavyo wanaajiri vijana wengi, akinamama wengi na baba zetu walio wengi.

Mheshimiwa Spika, tulienda kwenye kiwanda kimoja cha kutengeneza nguo pale Ubungo, tulipoingia kwenye kile kiwanda tulitiwa moyo sana. Kwanza, tulikuta wanawake ni wengi kuliko wanaume ambao wanashona zile nguo; *jeans,* ambayo kushona

huitaji elimu ya kuwa na *degree*. Hata kama ni darasa la saba anafundishwa mpaka anakwenda kuwa fundi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ungefika pale ungeona jinsi ambavyo wanawake wale, mabinti wale, kama siyo kwa ajira ile ungewakuta wanavuta bangi mtaani, ungewakuta wanajiuza barabarani kwa sababu hawana kipato. Kupitia ajira hizi, tuna akina dada wameajiriwa wanasaidia familia zao, mama zetu na mashangazi zetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, wawekezaji hawa *(investors)* tukiwatengenezea mazingira rafiki ya kuwekeza zaidi, tutakuwa tunakwenda kutatua changamoto kubwa sana ya ajira kwa vijana waliosoma, ambao hawajasoma, mama zetu na kila namna ya watu wa aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia…

**SPIKA:** Kengele ya pili ilikuwa imeshagonga. Dakika moja, malizia.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa, kwa nia yake njema ile ile ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, atuelezee kabisa haya mambo niliyoyasema akianza na lile la vivutio, kwa sababu, wameeleza kinagaubaga wakasema mpaka wanafika sehemu wanatamani kwenda kuwekeza kwa wenzetu. Ni kwa nini tuondoe ajira? Ni kwa nini tuondoe mzunguko wa pesa ndani ya nchi wakati vitu vidogo vinaweza kupatiwa ufumbuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa machache hayo, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, pia ahsante kwa kunivumilia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia afya njema hata siku ya leo ninashiriki Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naanza na shukurani. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa na maono chanya kwa Taifa letu. Huko tulikotoka, kama Taifa, tulikuwa hatujui tunataka nini kwa sababu, tuna ardhi yenye rutuba, tuna maliasili na tuna madini. Mungu ametupa kila kitu, lakini inafika mahali hatujui wapi tuende au tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Rais kwa kufanya maamuzi haya ya msingi kabisa kwamba awe na Wizara mahususi ya Mipango na Uwekezaji nchini, jambo hili ni la kupongezwa na ndiyo maana nimesema naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, mwanazuoni mahiri na msomi mbobezi kwenye masuala haya ya uchumi. Pia nampongeza Dkt. Tausi Mbaga, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu yangu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na Msajili wa Hazina, kaka yangu Nehemia Mchechu na bosi wangu wa zamani, nimeambiwa yupo hapa Dkt. Binilith Mahenge aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, mimi nilikuwa Mkurugenzi wa Jiji. Nakupongeza sana kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya *TIC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi naomba nianze kwa kumnukuu Hayati Baba wa Taifa. Hayati Baba wa Taifa aliwahi kusema; "Taifa lolote ili lipige hatua ya kimaendeleo, lazima liwe na ardhi, watu, siasa safi na utawala bora."

Mheshimiwa Spika, leo hii najikita kwenye eneo la ardhi. Tuna dhana moja, kama Taifa ambayo nadhani siyo dhana sahihi.

Tunaitazama ardhi kama migogoro. Tunaona sekta ya ardhi kama jukumu lake ni kutatua migogoro nchi nzima, hapa tuna changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yoyote ardhi ni rasilimali kubwa sana kwa uchumi wa nchi hiyo na ndiyo maana leo hii ukitazama Taifa letu, mimi nasema halijapimwa. Kwa nini halijapimwa? Kwa sababu, kama Taifa, unapozungumzia upimaji, ni lazima uwe na mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo yenyewe inaeleza mashamba yatakuwa wapi, makazi yatakuwa wapi na uwekezaji sekta ya madini na rasilimali nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa, ukitazama masuala ya ardhi wanajikita tu kupima viwanja vya makazi, jambo ambalo kimsingi kwenye uwekezaji linaturudisha nyuma. Sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii ya mipango na uwekezaji, nakuomba kaka yangu, wewe umepewa jukumu la kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera kuhusu mipango na uwekezaji. Hapa unapaswa kuwa na wivu usiogawanyika na ukigawanyika labda kwa Mama Kitila. Kwa nini nasema haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitarajii kuona Wizara za kisekta zinakuja na mipango yao. Mipango iko kwa Mheshimiwa Profesa Kitila. Wale wenye *vision* 2030, itoke kwa Mheshimiwa Profesa Kitila, ndiyo maana nasema awe na wivu usiogawanyika. Jukumu lake yeye ni kubuni na kusimamia sera zote za utekelezaji kwenye mambo ya uwekezaji na uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ikikupendeza nitoe mfano, mathalani tumeambiwa hapa na Wizara ya Kilimo kwamba kwenye Bonde la Mto Kilombero wanakwenda kuweka kilimo cha umwagiliaji kwenye hekta takribani 53,344.

Mheshimiwa Spika, sasa eneo hilo Mheshimiwa Waziri wa Mipango na uwekezaji kazi yake ni kumtazama Waziri wa Kilimo anapopeleka umwagiliaji; Wizara ya Nishati inafanya nini kwenye eneo hilo? Wizara ya Ujenzi inafanya nini kwenye eneo hilo? Hali kadhalika na Wizara ya Maji? Wizara zote za kisekta wewe ndiyo mratibu na msimamizi pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, changamoto kubwa kwenye Wizara za kisekta, Waziri wa Kilimo anakwenda kwenye umwagiliaji, lakini miundiombinu hakuna, umeme hakuna, mwekezaji gani atakuja? Ni kweli Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa kwenda kutangaza Taifa letu huko duniani, mwekezaji anakuja hapa Tanzania, haji na ardhi, anakuja na fedha *(capital),* akifika hapa unampeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mimi ni mkulima, mathalani mwekezaji mkulima ndani ya nchi hata nje ya nchi anataka kwenda kuwekeza kwenye kilimo cha zao la mpunga, unampeleka wapi? Wizara ya Kilimo imeandaa wapi? Wizara ya Nishati inafanya nini? Wizara ya Ujenzi inafanya nini? Wizara ya Uchukuzi inafanya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima kuwe na uratibu wa pamoja wa Wizara za Kisekta. Ndiyo maana nasema uwe na wivu usiogawanyika na ikiwezekana unavyoweka jitihada zako katika uwekezaji halafu kuna Waziri fulani hawajibiki, mwambie Mheshimiwa Rais, mama nina mpango wa uwekezaji kwenye sekta ya madini, lakini mtu wako naona anaturudisha nyuma. Eeh, kuwa hivyo tu, amua tu, kwa sababu, tunataka kulitoa Taifa letu hapa lilipo liende mbele.

Mheshimiwa Spika, sasa mwisho wa siku nikueleze, ukishindwa kusimamia eneo hili Mheshimiwa Waziri kitakachokukuta ni wajukuu zako watakuja kulichapa fimbo kaburi lako, babu alikuwa Waziri, alifanya nini? Watachapa fimbo kaburi lako badala ya kupalilia. Kwa hiyo, lazima uache *legacy* Mheshimiwa Waziri na uwe na wivu usiogawanyika kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuzungumzia kuhusu Serikali za Mitaa. Jamani nchi iliyobaki duniani, nchi inayoteua Wakurugenzi wa Halmashauri ni Tanzania peke yake. *I stand to be corrected*. Nchi iliyobaki kuteua Wakurugenzi wa Halmashauri, *Local Government Directors* ni Tanzania peke yake kwenye sayari ya dunia. Ukienda *South Africa* wanaitwa *managers.* Ili Mkurugenzi wa Halmashauri apatikane, anapitia mchakato wa ajira, lazima awe *professional.* Katika sehemu ambayo haitakiwi

ateuliwe mwanasiasa ni Mkurugenzi wa Halmashauri. Tusaidie eneo hilo pia.

Mheshimiwa Spika, wanachoweza kufanya wanampelekea Mheshimiwa Rais, baada ya mchakato wa ajira wapelekee majina matatu ya watu *competent*, tutaona mambo yanakwenda vizuri. Sasa kwa sababu waligombea Ubunge muweke pale, *no, no we can't move like that*. *As a nation we need to transform our mindset*. Kwa hiyo leo hii ndiyo maana hushangai, mimi sishangai kuona mkurugenzi wa halmashauri amekaa kwenye kiti anatamalaki. *We need fresh mind in a changing world*, lazima tuwe na fikra chanya katika ulimwengu unaobadilika, fikra mpya katika ulimwengu unaobadilika *(fresh mind in a changing world)*. Sasa unapataje fikra mpya? Lazima upate watu wenye uwezo kwenye kusimamia majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umezungumzia habari ya kuratibu ahadi, mipango na uwekezaji kwenye halmashauri. Pale kwenye halmashauri tuna Kitengo cha Mipango na Uwekezaji, lakini ukiwauliza wanafanya nini mpaka leo, hawana cha kufanya wametamalaki. Sasa nenda uratibu na kile kitengo, halmashauri zetu zianze kuwekeza ziachane na *mindset* ya kutoa huduma tu. *Anyway* ninavyozungumza, niliwahi kuwa mkurugenzi wa jiji, kwa hiyo *am not speaking from without*, *am speaking from within*. Nataka kusema nini hapa? Halmashauri zetu nchini ili ziweze kuwekeza, lazima kuwe na *special purposes vehicle*, Mheshimiwa Waziri andika hiyo itakusaidia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, *special purposes vehicle* ni kitengo maalum cha uratibu na uwekezaji ndani ya halmashauri. Mathalani nilianzisha mchakato Dodoma Jiji Mheshimiwa Waziri Mavunde atakuwa shahidi. Tulianzisha kitu kinaitwa *special purposes vehicle* kama chombo cha kuratibu uwekezaji katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Sasa sijui kama kinaendelea au wamefikia wapi wenzangu niliowaacha. Chombo hiki ni kizuri sana kuratibu uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano halmashauri zikiwa zinawekeza kwenye hoteli hawawezi ku-*operate hotel*, kwa hiyo

hiki chombo ndicho kinachokwenda kuratibu uendeshaji wa hoteli. Nitolee mfano pale *Metropolitan City Council* pale *Victoria South Africa*, wale jamaa wana kampuni sita, wanatoa *dividend central government*. Sisi Serikali za Mitaa zinasubiri Serikali Kuu kwenye kila kitu *90%, are we serious, are we genuine*?

Mheshimiwa Spika, hivi kuna haja gani ya kuwa na halmashauri ambayo inategemea Serikali Kuu *90%, is there any local government*? Waziri aondoe hiyo. Sasa niseme ni lazima tuwe na *mindset* ya uwekezaji kwenye halmashauri zetu na inawezekana. Kwa mfano, halmashauri zina uchumi kule walipo, natoa mfano tena niseme tu Mlimba *DC*, tuna shamba la miti pale Uchindile la ekari 1,300, kama uwekezaji wa miti ya mbao na *next 10 years* mambo yatakuwa mazuri kwenye mapato yetu ya ndani. Niliwahi kusema tuondoe halmashauri kwenye kufikiria masoko na stendi kama vyanzo vya mapato. Masoko na stendi ni huduma siyo mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na namshukuru sana kwa sababu ile Wizara yake ni *think tank* ya Taifa letu na Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare ajiandae.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua na kunipitisha kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Niipongeze na kuishukuru Kamati Kuu ya Chama changu Cha Mapinduzi kwa kuniteua. Pia, nichukue nafasi hii kuishukuru na kuipongeza UWT (Umoja wa kina Mama wa Chama Cha Mapinduzi) unaoongozwa na Mary Chatanda na Dada yangu Zainab Shomari. Pia, niwashukuru viongozi wa UWT kwa niaba ya Umoja wa Wanawake wa Mkoa wa Tabora,

Mwenyekiti wetu Mwanne Mchemba na Rhoda ambaye ni Katibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa mapenzi yako na maelekezo yako juu yangu. Umekuwa ni mtu wa karibu sana kwangu katika kuniongoza katika Bunge hili nilipokuwa mgeni, nakushukuru sana na Mungu akubariki sana. Niipongeze ofisi yako kwa ushirikiano wote ambao wamenipa na wanaoendelea kunipa, ofisi yako inanipa ushirikiano mzuri kwa kupitia Katibu wetu wa Bunge, mdogo wangu Nenelwa ananipa ushirikiano wa kutosha na watendaji wote katika ofisi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wabunge wenzangu, Wabunge wenzangu wamekuwa ni chachu kwangu kwa ushirikiano, pia, Kamati yangu inayoongozwa na Mwenyekiti wetu Mhagama. Nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika nchi hii. Mama huyu amejitoa kwa mapenzi na kwa moyo kama tunavyofahamu mwanamke anapofanya kazi, anafanya kazi yake kwa jitihada na kwa moyo wake wote ili afanye vizuri na amefanya vizuri, ana haki ya kupongezwa kwa yale ambayo ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nipo kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria; katika maeneo ambayo tumeweza kuyatembelea moja wapo ni Sehemu ya Kwala. Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri atuletee hapa *screen,* bahati nzuri hizi ni nzima tuletee picha ya ile Sehemu ya Kwala ambayo tumeitembelea ili watu waone. Kusema na kuona ni vitu viwili tofauti, waone pale Kwala, waje waone na Ubungo ni sehemu ambazo huyu Mama amefanya kazi nzuri sana. Kila atakayeona kwa picha tu ambayo bado zoezi halijakwisha, lakini ataelewa ni nini ambacho kinataka kufanyika katika nchi hii na ni nini Mheshimiwa Rais anachotaka kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na yale mazuri ambayo ameyafanya Mheshimiwa Rais, nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Uturuki pamoja na Chuo Kikuu kwa kumpa tuzo Mama Samia Suluhu Hassan. Wameona kazi anayoifanya Mama Samia Suluhu Hassan na macho yao yameona ndiyo maana wameweza

kumpa tuzo. Nawashukuru sana na naipongeza Serikali ya Uturuki kwa thamani kubwa waliyompa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawapongeza pia washauri wa Mheshimiwa Rais, wote ambao wameweza kumshauri na kushirikiana naye na utendaji wote mkubwa ambao ameufanya, kwani wao ni chachu kwake ya kuweza kumwonesha na kumpa dira Mama yetu mpaka anafanya mazuri ambayo tumeyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niangalie kero ambazo wanapata wawekezaji. Wawekezaji wetu wana moyo, tumewatafuta, tumewaleta na tumewapa maeneo, lakini bado wanakumbana na kero ambazo zinawarudisha nyuma. Nina imani haya yanaweza yakamuumiza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu alitoka kwenda nje kutafuta wawekezaji na akaleta wawekezaji, wawekezaji wanakuja. Kuna tatizo gani *TIC*? Kabla wawekezaji hawajaja waweke kwenye *website* vigezo vyao ambavyo wanahitajika kuwa navyo ili mwekezaji anapokuja kuwekeza hapa nchini, basi awekeze bila ya kuwekewa kikwazo chochote na wale ambao tayari wameshawekeza, basi tuangalie kama kulikuwa na makubaliano tuendeleze makubaliano yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo mwekezaji amekuja na ameshaanza kuweka majengo yake anaanza kuleta wawekezaji wengine, leo unaanza kukataa kutoa vitu ambavyo tayari mmeshakubaliana. Hili ni miongoni mwa vitu vinavyorudisha nyuma maendeleo ya uwekezaji nchini kwetu. Tunachohitaji, ifikapo 2025 tuone uwekezaji umeamka kwa kiasi kikubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikufahamishe kama alivyoongea mwongeaji mwingine aliyemaliza, wawekezaji ni wengi ambao wanakuja katika nchi yetu, lakini kutokana na vigezo vinavyoweza kuwashawishi wawekezaji kuja hapa kwetu hawavipati, hivyo wanakwenda Uganda na wanapofika Uganda wanafungua viwanda, malighafi zinazotoka kule zinakuja hapa Tanzania. Sasa kuna sababu gani ya sisi kushindwa kuweka vile vigezo na kuwapa nafasi kidogo? Tunawakimbiza watu na muda

ambao tunawakimbiza wawekezaji wanakwenda kuwekeza kule, sisi bado pale panasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo ni dogo au ni kubwa, wawekezaji wanaandika barua kwenda Wizara ya Fedha, *GN* mwekezaji hawezi kulipia chochote lazima itoke Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha barua inakaa zaidi ya miezi sita, wana tatizo gani? Wana kitu gani kinachoweza kuchelewesha barua isitoke? Wawajibu, kama wataweza kuwapunguzia kodi wawaambie tutaweza, hawawezi waache. Wanampa wakati mgumu hata huyu Mheshimiwa Waziri mwenyewe anayeshughulika na jambo hili, Waziri anapata unyonge kwa kufanya kazi kwa sababu ya wizara nyingine. Hiyo kwa kweli haiwezi kumpa nafasi Waziri akafanya kazi yake vizuri, wapeni nafasi Waziri afanye kazi yake vizuri. Wawajibu wawekezaji kwa wakati ili kazi iweze kuendelea na mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shida nyingine ni vivutio kwa wawekezaji. Tunaweka vivutio gani kwa wawekezaji? Mwekezaji anaweza akaamua kuja kuanzisha kilimo cha miwa, ambayo atawekeza kiwanda cha sukari. Muda anapofika tu, hajatulia Wizara ya Ardhi wameshakwenda, wakitoka Wizara ya Ardhi, wanaingia *OSHA*, *OSHA* wakitoka, *NEMC* inaingia. Sasa kuna tatizo gani hapa? Sisi tunategemea kama wanaweka utaratibu mmoja ambao utaweza kuwasaidia wawekezaji wetu watakaokuja bila ya kupata matatizo na wakawekeza kwa haraka. Hiyo inasaidia kuwapunguzia kero kwa kiasi kikubwa wawekezaji wetu kwani wao ni binadamu. Huwezi jua mwekezaji labda ameenda kukopa pesa ili aje kuwekeza hapa na aanze kuleta maendeleo yake. Aanze kuzalisha na kulipa kodi, lakini unapomchelewesha unachelewesha kwa kiwango kikubwa maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba wajipange vizuri ili kuweza kutoa kero hizi, kama ni vivutio waviweke na viwe ni vya kweli na hata watakapokuja basi wasiwe wenye kubadilika badilika. Wizara wawe na msimamo, wakiweka msimamo hata nchi yetu itaheshimika na kuthaminika kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze sehemu nyingine ambazo tumeenda, mfano kwa kina Mzee Kamaka, ni mwekezaji wa Kitanzania lakini pamoja na kuwekeza, Idara ya Maji tu wanashindwa kumchukulia maji na kumsogezea pale. Yule amewekeza na akaweka miundombinu yeye mwenyewe, ni Mtanzania wa hapa hapa, lakini kumvutia maji tu kumwekea inakuwa shida. Wanamvunja moyo na wanawavunja moyo wawekezaji wa ndani ya nchi hii, wanakuwa hawana moyo tena wa kuwekeza, kwa sababu ya kitu kidogo. Je, wanahitaji kitu gani pale ili wamvutie na kumwekea maji kusudi shughuli zake ziweze kuendelea? Amewekeza pesa nyingi sana na ni mtu mzima lakini hakujali utu uzima wake kaamua kuwekeza katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mapenzi makubwa ambayo ameyafanya. Mheshimiwa Waziri, tunaomba atuwekee, narudia tena Mheshimiwa Waziri naomba atuwekee zile picha za tulipotoka na tunapokwenda. Ubungo pale amefanya vizuri sana na kazi kubwa imefanyika. Kwa wale ambao tumeweza kutembeatembea kidogo tumeona pale Ubungo itakuwa ni sehemu ya kituo cha biashara kikubwa sana katika nchi hii na nchi Jirani zote maana viwanda vyote ambavyo vipo China vitakuja pale kufungua biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wananchi wetu waliokuwa wanasafiri kwenda China wote watachukua bidhaa zao pale. Tanzania, Kenya, Uganda na nchi nyingine watafanya pale. Zoezi ni kubwa sana na soko litakuwa zuri sana, soko lenye maendeleo na nchi yetu itabadilika kwa kiasi kikubwa sana. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hongera kwa kazi kubwa ambayo amefanya. Nchi yetu ameifanyia haki, anaitendea haki na ni mama mwenye mapenzi, maono na mwelekeo wa mbali sana na nchi hii. Tunajua anaumia kwa nchi yake, ana mapenzi na nchi yake, Mungu atamsaidia atafanya kazi zake kwa amani na baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Kama muda

utakuwa umesalia basi Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo atamalizia.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kitila *mate* wangu. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kutoa mchango wangu huu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote (watendaji wote). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pamoja na kwamba Wizara hii ni Wizara mpya, lakini inafanya kazi kubwa, maono yao ni makubwa. Mimi ni mmoja kati ya watu tulio na matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Kitila na Wizara hii kufanya Taifa hili liweze kuwa Taifa imara kiuchumi, lakini liweze kutenda yale ambayo wananchi wanatarajia, kuwaimarisha kiuchumi lakini na kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri nikitambua kwa ujumla wake kazi kubwa inayofanyika kwenye Taifa letu. Kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba mipango inayopangwa inatekelezeka, lakini wananchi wa Taifa hili wananufaika na rasilimali za Taifa hili tulizojaliwa na Mwenyezi Mungu. Pamoja na changamoto kadhaa tulizozipitia hapo nyuma ikiwemo habari ya UVIKO, vita huko duniani lakini bado tumepata wawekezaji wengi kwenye Taifa hili. Jambo ambalo limeongeza hata pato la Taifa na Taifa letu kimsingi linafanya vizuri hata kwenye mtiririko wa kupanda kiuchumi lakini na namna linavyoendelea. Ndiyo maana kwa mfululizo karibu kila mwaka *GDP* imekuwa inaongezeka kwa zaidi ya asilimia tano na kufanya Tanzania kuwa moja kati ya nchi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pia na Wizara ya Mipango. Pamoja na haya kuna maeneo ambayo nilitamani nitoe mchango wangu. Mheshimiwa Waziri anaonesha jinsi Wizara yake inavyojiandaa

kuandaa mpango wa mwaka mmoja, lakini vilevile kuelekea kuandaa Mpango wa 2050.

Mheshimiwa Spika, kupitia *FDI* uwekezaji mkubwa umefanyika na ajira nyingi zimezalishwa. Kama nilivyosema ni kweli kwamba kama Taifa uchumi unapanda na natambua kwamba kwenye kukua kwa uchumi wetu kuna sekta mbalimbali zilizochangia kukua kwa uchumi wetu ikiwa ni pamoja na kilimo. Ni kweli kupitia uwekezaji ajira nyingi zimezalishwa lakini nafikiri katika mipango inayokuja bado ni muhimu sana kufikiri na kuwekeza kwenye uendelezaji wa kilimo kwa sababu tumejaliwa ardhi nzuri na kubwa ya kutosha. Kilimo hiki ambacho kinaajiri zaidi ya 70% ya wananchi tulionao kiweze kuchangia vilevile kujenga kwanza uchumi wetu kama Taifa pia na kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja, ili kuwapa nguvu ya kufanya manunuzi ili uwekezaji unaofanyika kupitia *FDI* uweze kuwa na *reflection* kwenye maisha halisi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo ndiyo maana naona pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika bado hatujaweza kutumia vizuri rasilimali maji tuliyonayo ili tuweze kufanya kilimo chenye tija, kilimo cha umwagiliaji. Amesema mchangiaji mmoja hapa tuna maziwa mengi mojawapo ni Ziwa Victoria, tumetumia Ziwa Victoria kwa ajili ya maji ya kunywa, maji safi kwa ajili ya Taifa letu, lakini naona bado hatujalitumia vizuri Ziwa lile kufanya kilimo cha kisasa, kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Kilimo, amewekeza kiasi kikubwa kwa miaka michache iliyopita kuhakikisha kwamba tunafanya mapinduzi ya kilimo. Ni kweli kwamba, kuna maeneo tumewekeza kwa ajili ya kujenga mabwawa ili tufanye kilimo cha umwagiliaji, lakini naamini kama tutatumia vizuri maziwa tuliyonayo, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Maziwa mengine tunaweza kufanya mapinduzi makubwa sana ya kilimo na hatimaye kuzalisha ajira nyingi sana zitakazoleta mapinduzi ya kiuchumi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo kama Ukerewe, limezungukwa na maji, tuna maeneo mengi ambayo tunaweza tukafanya kilimo

cha umwagiliaji, nashauri tufanye uwekezaji mkubwa sana kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria ili tuweze kufanya mapinduzi ya kilimo. Hata zile hekta karibu 2,000 zilizoko Ukerewe na kwa sababu imezungukwa na maji tuweze kuzitumia vizuri tufanye mapinduzi ya kilimo, tuondokane na shida ambazo tumekuwa nazo ambazo zinadhoofisha hasa uchumi wa wananchi wetu kupitia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitamani kuchangia ni kweli tunakaribisha wawekezaji, uwekezaji mkubwa unafanyika. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati hali ya umeme sasa inaridhisha, lakini bado pamoja na uwekezaji mkubwa tulionao, natambua katika *energy mix* karibu 30% na zaidi ya umeme kwenye *energy mix* inategemea *hydro*. Sasa kama inategemea *hydro* tuna kila sababu ya kulinda vyanzo vya umeme huu ili huko mbele pamoja na kukaribisha wawekezaji, baada ya wawekezaji kumewekeza, isitokee *energy failure* ikaathiri mfumo mzima wa uwekezaji na kuathiri uchumi wa Taifa letu kwa hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilishauri katika vyanzo tulivyonavyo, kwa mfano sasa tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuna Kihansi, tuna Kidatu na kadhalika lakini vyanzo vya maji yanayotiririka kuelekea kwenye vyanzo hivi bado hatujaweza kujenga mfumo au sera ya kulinda vyanzo hivi ili kesho na kesho kutwa tusipate janga la kupungukiwa na maji na hatimaye kuathiri mfumo mzima wa umeme, kwa sababu katika megawati karibu 2,000 tunazozitegemea sasa ikitokea 31% hiyo inayotegemea *hydro* ikaathirika, mfumo mzima wa kiuchumi kama Taifa utaathirika, jambo ambalo litaathiri hasa uchumi wetu kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, katika mipango wanayoipanga moja katika hiyo aangalie ni namna gani wanakuwa na mipango endelevu ya kuhakikisha kwamba, hatuwezi kupata athari za kinishati, jambo ambalo litaathiri uwekezaji na mambo mengine yote na nguvu kubwa tunazoziwekeza, sasa kutafuta wawekezaji na kadhalika zikawa hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana hilo liwe jambo muhimu sana, kwenye *issue* ya kilimo katika mipango tunayoipanga tuhakikishe kwamba ni ajenda muhimu na ulinzi wa nishati tuliyonayo, tunayoitegemea na tunayoitengeneza kwa ajili ya kuwezesha viwanda vyetu, tuweke mifumo, tuweke mipango na tuweke sera kuhakikisha kwamba tunailinda ili kuhakikisha kwamba haiathiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, nikushukuru kwa nafasi hii, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, amefanya uchumi wetu umeendelea kuwa *stable*, ndiyo maana leo pamoja na kwamba kuna malalamiko ya wananchi juu ya mfumuko wa bei, lakini napata faraja kwamba mfumuko wa bei kwa Taifa letu upo kwenye asilimia zaidi ya nne ukilinganisha na maeneo yanayotuzunguka. Kwa mfano, Zimbabwe wana zaidi ya 90%, Sudan wana zaidi ya 80% na Ghana wana 50%, kwa hiyo hili ni jambo ambalo linatia faraja. Pia nikiona namna ambavyo pato letu la Taifa linavyoongezeka inatia faraja. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ili kuhakikisha kwamba, Taifa letu linaendelea ku-*prosper* kiuchumi ili hatimaye wananchi wa Taifa hili waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa muda uliobaki nadhani tutaweza kupata mchangiaji mmoja, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja ya Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere moja ya vitu ambavyo alituachia na akilihutubiia Taifa miaka ile, maadui wetu wakubwa walikuwa ni watatu ambao sisi watoto wake na wajukuu zetu tunatamani nao wajue kwamba maadui hawa tunaenda nao namna gani? Alituambia maadui hao ni ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Spika, leo nijadili jambo moja tu la umaskini wa Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Duniani nchi hutegemea rasilimali zake ili kujikwamua na kujitoa katika umaskini. Afrika ilikuwa ina-*host* sana wageni kutoka Bara la Asia miaka ya nyuma kwa sababu gani? Bara la Asia walikuwa na hali ngumu ya uchumi. Kwao mvua zilikuwa hazinyeshi na ndiyo utamaduni wao na ndiyo tabia ya nchi za kwao. Sisi mvua zilikuwa zikinyesha na tunapata chakula na walikuwa wanakuja kuhemea katika nchi hizi, tukawa hadi na ukoloni ambao umetokana na Nchi za Kiarabu katika Pwani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa maana gani? Kwa maana kwamba, sisi uchumi wetu tunazo rasilimali, kama wale ambao walikuwa wanakuja hapa kuhemea chakula, leo wana rasilimali ya mafuta na gesi, sasa tunaenda kuhemea kwao vitu vya viwandani kwa sababu tumeshindwa kuheshimu rasilimali yetu ambayo tunayo na kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama Jamhuri ya Muungano, tunayo gesi asili, leo toka tumeanza mchakato wa kufanya gesi hii iwe kimiminika kuwa *LNG* mchakato huu ni miaka 12 sasa bado upo juu ya meza na hatujamaliza, shida yetu nini? Nadhani wale tunaowateua kuwa katika meza ya mazungumzo inawezekana nao wana shida, kwa sababu wanapokaa vikao wanapewa posho, sasa hawawezi kumaliza mchakato kama zile posho zitakatika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuchakata jambo kwa miaka 12, toka 2012 mpaka leo bado *LNG* ipo kwenye mchakato. tunategemea nchi hii kweli tutakwenda? Hebu tuone mifano michache ya nchi ambazo zimenufaika na gesi asilia, *Qatar* juzi walikuwa ni *host* wa *World Cup,* hawana rasilimali nyingine zaidi ya gesi. Wenye uchumi mkubwa duniani, wanaoshindana na Marekani, Warusi uchumi wao mkubwa unategemea gesi na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunapigana vita vya Uganda na nchi jirani hapa, mtu aliyetusaidia mafuta ilikuwa ni Nchi ya Algeria lakini Algeria uchumi wake mkubwa haubebwi na mafuta umebebwa na gesi. Leo sisi tuna gesi kwa miaka 12 tumekaa

tunazungumza juu ya meza ni namna gani twende, namna gani tufanye, tunashindana wapi? Wapi tunakwama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani kuiona Tanzania kwa macho yangu angalau pamoja na umri huu mkubwa, lakini natamani kuiona nchi hii inanufaika na rasilimali zake. Leo pale Dar es Salaam kuna vituo vichache vya *CNG*. Ukikuta foleni ni kama hapa na kule *CBE,* magari yanasubiri kujaza gesi. Hivi kweli Watanzania tupo hapo? Namwomba Profesa na timu yake na Tume hii ya Mipango, watupe mipango endelevu juu ya hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunaagiza *LPG (Liquid Petroleum Gas)* kwa ajili ya kupikia, lakini sisi tuna *natural gas* hapa ambayo tunatakiwa tusambaze tu mabomba, watu wapikie gesi. Tulishindwa kutengeneza *biogas* hata vijijini tu kwa uwekezaji wa Serikali, leo ni msamiati, mtu ukimwambia *biogas* ni nini hapa Tanzania, hajui. Namwomba Mheshimiwa Kitila Mkumbo Profesa wa Uchumi atusaidie kwenye mambo haya, waje na mipango ambayo itawezesha kama nchi tutoke hapa kwenye mchakato tufike mahali sasa uchumi wetu ubebwe na gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua gesi asilia ikishachakatwa kuwa kimiminika itabebwa na meli kwenda nchi nyingine. Leo lazima utengeneze *pipe* ili gesi ifike Dodoma, sasa tunashindwa hapo lakini hata kuchakata? Kuzungumza na mtu kuzungumza na mabenki, trilioni 100 ni nini? Wakati tunakwenda kuokoa bajeti ya miaka na miaka!

Mheshimiwa Spika, leo Bunge hili tunaidhinisha bajeti ambayo ina utegemezi wa zaidi 38%, kwa nini tusitoke huko? Tuna vitu vya kutosha, tuna rasilimali ya gesi asilia ya kwetu ipo ndani ya ardhi. Hata kama huyo anayetuchimbia anachukua kiasi chake kuna ubaya gani? Wewe una shamba huwezi kulilima akaja mtu akalima na wewe ukapata chakula shida ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninalo jambo lingine ambalo natamani kulichangia leo, tuna mipango mingi ya Serikali katika kilimo, katika nishati, katika barabara, katika maji, katika afya, katika

maliasili na maeneo mengine lakini hatuna mipango ya maendeleo vijijini. Nchi yetu 80% ya wananchi wetu wanaishi vijijini. Leo tuna dude kubwa TAMISEMI linasimamia maeneo yote Majiji, Manispaa, Miji, Miji Midogo na Vijiji, hivi kweli tutafika?

Mheshimiwa Spika, natamani kuona waje na mipango ambayo itafanya tuje na mpango ambapo aidha kuwe na Mamlaka au Taasisi, aidha chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo itashughulika na maendeleo vijijini peke yake. Leo TAMISEMI wanashughulika na elimu msingi hadi sekondari kidato cha sita, TAMISEMI hao hao wanashughulika na afya kuanzia zahanati mpaka hospitali za wilaya. TAMISEMI wanashughulika na maeneo mengi yanayohusu maendeleo ya jamii kule kwetu kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa waje na mipango ambayo itatupa Taasisi nyingine ambayo aidha ni Wizara au ni Idara au ni namna gani watatusaidia wataalamu, tuje na kitu ambacho kitasimama kwa ajili ya maendeleo vijijini peke yake ili nchi nayo iweze kwenda. Huwezi kuchanganya vijiji na majiji kama Dar es Salaam, Mwanza au Dodoma halafu wakawaweka katika *level* moja, hatuwezi kufika. Natamani kuona haya yatokane na mipango ambayo tutakwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo la Msajili wa Hazina, ametuonesha dhamira njema. Juzi tulipokuwa na maonesho ya nishati hapa kuna vitu nimevibaini naomba nivizungumze. Tuna *TGDC* hawa watu wa joto ardhi, tunao *TPDC*, tunao *TIPA* na tunao *EWURA* wote ni wamoja. Kwa nini tusije na Taasisi moja nzito yenye nguvu yenye kusimamia haya mambo? Huyu anayechakata utafiti wa gesi na mafuta kule baharini na huku maeneo mengine ni mwingine, akitaka kuzalisha anakuja mwingine, hizi taasisi kwa nini haziendi pamoja? Pia, mifumo ya Serikali haisomani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu anayefanya *exploration* akishatoa taarifa yake haisomwi na mwingine inabaki kwake na mwingine mpaka akaiombe. Kwa nini tusiwe na uwazi na tujenge mifumo? Nataka niombe pia ikiwezekana *eGA* waingie hapa waweze kuona mifumo ya Serikali kama kuna *exploration,* basi taarifa zake

ziwe wazi kila mahali ili hata kama kuna mwekezaji mwingine atataka kwenda mbele zaidi ya huyu alipoishia aweze kuona.

Mheshimiwa Spika, natamani kuona nchi yangu inakwenda lakini haiwezi kwenda ila kwa mipango ambayo imeundwa na Wizara hii ya Uwekezaji na Tume ya Mipango, watu wa Mipango wa Wizara ndiyo watatusaidia zaidi kwa sababu Tume wao wataangalia namna gani, kwa sababu Mwenyekiti wa Tume hatuwezi kumgusa, tunamgusa huyu ambaye ni wa kwetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimeona nitoe maoni haya na naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya Kikao chetu cha siku ya leo. Nitataja baadhi ya majina ambao tutaanza nao uchangiaji mchana. Tutaanza na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na wengine tutaendelea kuwataja kadiri muda utakavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, pia, tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Olelekaita kutoka Kiteto, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itakuwa na kliniki ya ardhi katika viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 22 Aprili. Sasa hii tarehe ya kumaliza sina uhakika sana hii itatangazwa baadaye, lakini kliniki inaanza leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huduma zitakazotolewa ni pamoja na utoaji wa hati, utatuzi wa migogoro ya ardhi, utoaji wa ankara za ulipaji wa kodi ya pango la ardhi na uthamini, elimu ya ardhi na masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kitu chochote kinachohusu neno ardhi tunayo fursa ya kujifunza katika kipindi hiki, pia changamoto

za wananchi tunaowawakilisha kama tunazo tuzipeleke ili zitafutiwe ufumbuzi. Yamkini huko baadaye maadam leo tunazungumzia Bajeti ya Wizara hii muhimu kabisa na Mheshimiwa Waziri yupo hapa, mipango itakuwa mizuri, tutaondokana na hoja za migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia, katika Wizara yetu mpya hii ya Mipango na Uwekezaji. Mahususi naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kweli ameanzisha Wizara hii na kwa umakini kabisa akaweka Wizara hii chini ya Ofisi yake ili aweze kuisimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila Mkumbo kwa kuwa Waziri wa kwanza kuongoza wizara hii. Naamini ndugu yangu kwa weledi wake amepewa ukapteni kuhakikisha kwamba sasa jahazi linakwenda vizuri akisaidiana na wenzake Katibu Mkuu, Dada yetu Dkt. Tausi Kida na watendaji wake wakuu wote; Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Ndugu Lawrence Mafuru, Msajili wa Hazina, Ndugu Nehemia Mchechu, Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA*, Charles Itembe na Mkurugenzi wa *TIC,* Gilead Teri pamoja na watumishi wote ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mahususi kabisa naomba kutumia mchango wangu katika Wizara hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jambo la kihistoria katika uwekezaji ndani ya Taifa letu. Jambo lenyewe ni jana tumeona treni yetu ya *SGR* kwa mara ya kwanza inatembea kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na ikibeba viongozi na imetumia takribani masaa manne. Ni jambo la kujipongeza sana katika ukombozi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona kazi njema ya Wizara hii na mimi nikisema ni Mjumbe wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ambayo inasimamia Kamati hii, wanafanya kazi nzuri sana. Tumeona katika mpango wa kurekebisha mazingira ya biashara (*blue print)* kuna mambo mengi ambayo mpaka leo yamefanyika. Tunaona mapitio ya sheria ambazo zilikuwa zinabainika kuchelewesha au kukwamisha uwekezaji ndani ya nchi yetu. Mpaka leo tunaona zaidi ya sheria 55 zimeshafanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Spika, tunaona tozo mbalimbali ambazo zilionekana kwamba hizi tozo zinaweza kuleta kero na zimeweza kupunguzwa au nyingine kufutwa. Zaidi ya tozo 374 zimefanyiwa marekebisho. Ni jambo la kujipongeza sana kwa kuleta mazingira ya uwekezaji ndani ya nchi yetu yakawe huru zaidi na kuvutia sana wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii haijaishia hapo, imeendelea kuunganisha majukumu ya taasisi, yale yanayofanana na kuondoa yale yanayoingiliana. Tumeona Taarifa ya Mheshimiwa

Waziri asubuhi hapa, ameunganisha taasisi nyingi, lakini tukiangalia mahususi tunaona kweli wakati mwingine unasema wakati wote tulikuwa wapi. Ukiona Bodi ya Maziwa na Bodi ya Nyama, sasa hivi zinaenda kutengeneza Bodi ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia yale majukumu yaliyopo ndani ya bodi hizo ni kama yanafanana. Ukiangalia sasa katika Taasisi ya Utafiti wa Tumbaku, ilikuwa Taasisi ya Utafiti wa Kahawa na sasa hivi tunaona Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Ni mambo ambayo kwa kweli ukiyaangalia na matokeo yake unajivunia kwamba kwa kweli nchi yetu imedhamiria kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji lakini pia na kurahisisha uwekezaji ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya tunaona kweli pia kuna Tume ya Mipango ambayo ipo katika maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Tunaona dira ndiyo kiongozi na mwongozo unaosaidia katika kuendesha nchi. Kwa hiyo tunaamini Dira hii ya 2050 ikishakamilika, basi nchi yetu itakuwa katika mwelekeo ambao kila kiongozi anayekuja anafuata mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo tunaona dira yetu lazima ifungamanishe nchi yetu na malengo ya kikanda na kimataifa. Tunayo malengo ya *Africa Agenda 2063* ambayo lazima tujifungamanishe nayo. Pia, tunayo malengo ya *East Africa Vision 2050,* lakini pia tunayo malengo ya *SADC Vision 2050*. Haya yote na nchi yetu ikiwa na dira ambayo imekuwa *reflected* katika eneo hilo basi tunaamini kwamba tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, niombe tu ufafanuzi wa Wizara wakija kuhitimisha. Tunaona mchakato wa kutengeneza hii Dira ya Taifa ya 2050 inapitia kama hatua tatu. Tunaona katika maandalizi ya awali, tunaona katika usanifu na uidhinishaji. Tukiangalia huu muda na tukiangalia katikati hapo inapitia katika maeneo mbalimbali kukusanya maoni ya wadau. Kwa kweli ni *process* ambayo ni ndefu.

Mheshimiwa Spika, sasa hii Dira yetu ya 2025 inakaribia mwisho. Kwa hiyo watupe *comfort* na msimamo wa Serikali

kwamba ni kwa jinsi gani wataweza ku-*catch up* katika muda huo kabla ya Dira 2025 haijaisha, basi na hii angalau imeshakuwa *in place* kwa ajili ya ku-*take over* na nchi yetu sasa iendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kimsingi nitaongelea katika suala la kujumuisha mienendo ya kikanda na kimataifa na hivyo kutuleta sisi tukawa sehemu ya malengo uliyotaja *Africa Agenda 2063, East Africa Vision* na *SADC* na za kimataifa. Nitaongelea suala la *health safety* na nitaangalia *vis a vis Bureau of Standards.*

Mheshimiwa Spika, na-*declare* kwamba *once upon a time* nilikuwa mtumishi ndani ya taasisi ambayo inasimamia suala la afya. Katika eneo hili kwa weledi ambao nimeuona ndani ya Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji, kwa weledi ninaouona kwa wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri hili suala sitaki kulisema na Mheshimiwa Waziri, naomba anisikilize vizuri. Hapa nina-*deal* na *health safety vis a vis Bureau of Standards.*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Bodi ya Madawa na Tume ya Kudhibiti Chakula Salama Tanzania ziliunganishwa. Hiyo Tume ya Chakula ilikuwa inaitwa TUKTA na lengo la kuunganisha Bodi ya Dawa na Tume ya Kudhibiti Chakula ilikuwa kuunganisha nguvu moja ya udhibiti na kuunda chombo ambacho ni kimoja, yaani kuleta *harmonization*. Pia, ililenga kupanua wigo katika udhibiti, kuongeza bidhaa nyingine za vifaa tiba na vipodozi, viungane na dawa na chakula iwe moja.

Mheshimiwa Spika, msingi wa udhibiti huu unazingatia malengo ya kikanda na malengo ya kitaifa *(Regional and International Best Practice)* duniani kote. Ukiangalia katika maeneo hayo upande wa *Bureau of Standard* si wadhibiti wa bidhaa ambazo zinahusiana na afya ya binadamu, si wadhibiti wa bidhaa ambazo zinahusiana na afya ya wanyama, si wadhibiti wa bidhaa ambazo zinahusiana na afya ya mimea. Maana yake viongozi wangu wakienda kuangalia kwenye *Sanitary and Phytosanitary Agreement* ya *World Trade Organization* watakuta haya mambo yote yameainishwa pale yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali; ukiangalia duniani kote zimeunda chombo cha udhibiti na kuweka bidhaa zote ndani ya mamlaka moja. Wameweka dawa ndani ya mamlaka moja, wameweka chakula ndani ya mamlaka moja, wameweka vipodozi na vifaa tiba. Naelewa inawezekana nchi yetu kuna vitu ambavyo iliona na hasa najua changamoto ilikuwa ni tozo mbalimbali, lakini si huo uhalisia wa *health safety* katika bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, tukitoka hapa twende Kenya hapa jirani wanayo *Kenya Food and Drugs Authority* ambayo inasimamia bidhaa zote. Ukienda Marekani utakuta kuna *USFDA,* Canada, *heath Canada* inasimamia vyote, China utakuta *CFDA*, India kuna India *FDA*, Thailand utakuta Thailand *FDA*, Singapore na Ghana *FDA*.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kushangaza na kizuri zaidi mtoto wetu ambaye amezaliwa hapa Zanzibar Visiwani, *Zanzibar Food and Drugs Authority* ambaye tumemlea sisi na sasa hivi anafanya kazi nzuri iliyotukuka, yeye bado ni taasisi moja ambayo inasimamia bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, naongea haya kama sehemu ya utaalamu wangu kwamba pamoja na changamoto za kibiashara ambazo naungana na Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya, zitatuliwe. Tunapokuja kwenye suala la afya kidunia niombe Mheshimiwa Profesa Kitila, yeye ni mweledi pamoja na wasaidizi wake, hili suala tusilichukulie kwa mtazamo wa kawaida, wa juu juu. Leo tunazo bidhaa nyingi mtaani ambazo ni za chakula, leo tunazo bidhaa nyingi za vipodozi na kila nikisimama nasema kuhusu suala hilo. Hii nchi tunaendelea kubana matumizi, hatuwezi kuwa tunatafuta dawa lakini vyakula vilivyopo huku mtaani na vipodozi vinaenda kutumia zile dawa na nyingine kuathiri hata afya za wananchi. Kwa hiyo niombe, tukiweka udhibiti mzuri katika bidhaa hizi na sioni Serikali inakosa nini kwenda na mfumo kama ambavyo malengo yetu katika *blue print* yanatutaka kujumuisha mienendo ya kikanda na mataifa, tukaenda kama nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, niombe sana katika eneo hili, suala la vyakula na vipodozi. Sina *interest* na Wizara yoyote lakini naiangalia Serikali yangu ifanye kazi vizuri, imsaidie mwananchi kulinda afya yake, isaidie kabisa katika udhibiti bidhaa hizo ambazo zote zina *market* sana sokoni. Tukisikiliza wafanyabiashara wetu wakataka mteremko bila sisi kuweka udhibiti ambao unatakiwa kidunia na kikanda nasita kusema huko mbele tunapokwenda bajeti ya dawa itaongezeka, vifaa tiba ambavyo tunanunua havitatosha na hospitali anazojenga Mheshimiwa Rais hazitatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana na nihitimishe kwa kusema, Mheshimiwa Waziri aangalie kwenye *blue print* yake. *Page* nyingi zimeelezea kinagaubaga kwamba, hizi bidhaa zinatakiwa kusimamia nini na naamini kwa weledi wake ataweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kengele ya pili, naomba nikushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai. Leo kama siku nyingine nilizopata kuchangia namshukuru kwa fursa hii. Pia, niwashukuru familia yangu kwa kunivumilia kwa muda mrefu nikifanya kazi hii ya kuwatumikia wananchi wa Jimbo langu lakini na wananchi wa nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, binafsi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kutengeneza ustawi wa nchi hii. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa kama nilivyosema hapo mwanzo kwa sababu kila tunachojaribu kukiongelea kuhusiana na jitihada zake alizozifanya zipo wazi.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nawaasa wasaidizi wake kwenda na kasi yake. Mheshimiwa Rais amekuwa akienda kwa

kasi kubwa kiasi cha kuwaacha baadhi ya watendaji wengine wakiwa wanatambaa. Sasa kama nilivyosema ni muhimu sana watendaji na wasaidizi wake kwa ujumla tukajitahidi kutaka kuangalia na kufahamu kwamba Mheshimiwa Rais ana maono gani na anatarajia nini kutoka kwao, hali kadhalika matokeo ya kile anachokitarajia huko mbeleni ni nini?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ni kama vile sehemu hizi mbili kuna nyimbo hizi mbili tofauti zinaimbwa. Upande huu huku inachezwa nyimbo hii lakini upande mwingine unacheza wimbo mwingine; hakuna *correlation*. Natofautiana kidogo na wenzangu kuhusiana na suala la Tume hii ya Mipango kwamba labda inaweza ikatutoa sana katika mazingira yetu tuliyokuwa nayo kama sisi hatutabadili *mind set* zetu; kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba mipango ilikuwepo muda wote, hakuna hata mwaka mmoja ambapo mipango ilisimama. Kilichobadilika ni kwamba mipango hii imebadilishwa katika utekelezaji kwamba nani anaisimamia. Kuna wakati mipango hii ilisimamiwa na Wizara ya Fedha, kwa hiyo Idara ikawa ndani ya Wizara. Kuna wakati pia mipango hii ilikuwa imesimamiwa yenyewe ikiwa na Wizara maalum kabisa ikijitegemea kufanya mipango.

Mheshimiwa Spika, muda huo wote tumeona kwa kadiri mambo yalivyokuwa. Hali kadhalika hivi sasa toka mwaka 2023 Tume ya Mipango pia imerudi ikijitegemea na kuwa ni Wizara kamili kabisa ambayo inashughulika na mipango hii. Kwa hiyo nyakati hizi zote mbili tumepitia, kipindi ambacho Wizara imeshughulika na mipango, lakini kipindi ambacho Tume imeshughulika na mipango. Bado kumekuwa na mapungufu kwa nyakati hizo tofauti, licha ya kama nilivyosema viongozi wetu wakubwa kwa maana ya Marais kwa muda tofauti tofauti, kujitahidi sana kuhakikisha kwamba ustawi wa nchi hii unakuja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jitihada zao binafsi zilikuwa zikionekana, lakini mipango ile ilikuwa inashindwa kuunganika kutoka kwa wenzetu, watekelezaji. Kwa hiyo kama nilivyosema nafikiri *mind set* ni muhimu sana katika kuhakikisha tunavuka hapa tulipo. Kusema peke yake kwamba Tume ya Mipango imekuja,

kwa hiyo tutakuwa na hali nzuri, huko ni kujidanganya. Tunahitaji ku-*change mind set completely* kutoka kwa watendaji na wale wanaopanga hii mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikisema kwamba ni kwa nini, ni jitihada binafsi? Ukiangalia kutoka mwaka 1996 mpaka kufikia hivi leo, *TIC* ilivyoanza kusajili wawekezaji ilisajili takribani watu au kampuni 12,381 zilizokuwa na nia ya kuja kuwekeza katika nchi hii. Tafsiri yake ni nini? Kampuni hizi au watu hawa kama wangekuwa wamekuja wote wangetuletea pesa za Kimarekani takribani bilioni 117. Hizi ukizibadilisha ni pesa nyingi sana. Ni kama shilingi trilioni mia mbili hivi na kitu, ni pesa nyingi mno.

Mheshimiwa Spika, sasa pesa hizi kama zingekuja maana yake nini? Zingeleta mtaji kutoka pesa ya kigeni kuja hapa kwa kiasi cha pesa nilichokitaja hapo. *Impact* ya hii ingekuwa ni nini? Kungekuwa na vitu mbalimbali vingejitokeza. Kwanza hawa wawekezaji wanakuja na pesa ya kigeni kama nilivyosema kwa maana kungekuwa na pesa ya kutosha kwenye *reserve* kwa maana ya dola ya kutosha kwenye *reserve*. Hii ingeimarisha Uchumi, kwa sababu gani? Kwa sababu pesa yetu ya Kitanzania ingeimarika, kwa maana mahitaji ya dola yangekuwa yanaenda *proportional* kabisa na uwepo wa pesa hiyo.

Mheshimiwa Spika, si kama hali iliyopo sasa hivi kwamba tunatamani kuwa na matumizi ya dola kwa ajili ya kununua au kuingiza kutoka nje, lakini dola hizo hatuna tunalazimika sasa kuzinunua dola zile kwa kutumia pesa ya Kitanzania, pesa nyingi sana. Wakati ambapo ungeweza ukanunua kikombe kwa shillingi mbili unalazimika kununua kikombe hicho hicho kwa shillingi 100 na sababu ni tofauti ya dola *(exchange)* iliyotokea pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona kwa kiasi gani athari inajitokeza kwa kuja na kiasi hicho kikubwa cha fedha. Maana yake tungekuwa na fedha nyingi kwenye uchumi na uchumi ungekua. Pamoja na hiyo hali jinsi ilivyo, kungekuwa na wawekezaji wengi, kiasi hicho kingi cha fedha kingeingia. Hatuoni na hiyo fedha haionekani wala wawekezaji hawajaja kwa kiwango hicho. Hii inaonekana kwa uhalisia wa hali ya malalamiko yaliyopo sasa hivi ya dola na ni tafsiri ya wazi kabisa

kwamba hizi fedha za kigeni ambazo kupitia kwenye *investors* hawa, ambazo wangezileta kama miradi hazipo au kama zimekuja basi ni kiwango kidogo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalozungumzia kwamba hakuna *correlation* ya mipango ni pale ambapo tunatamani kabisa miradi mikubwa ya kimkakati, ambayo tungetamani tufahamu kama imeshaanza kufanya kazi, ni kama vile Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mradi huu umezungumzwa tangu wengine sisi hatujazaliwa, lakini mpaka sasa hivi bado umebaki kuwa kwenye karatasi. Kila wakati wa mipango, iwe ni mipango ya kutoka kwenye Wizara au kutoka kwenye Tume yenyewe, bado mpango huu ulikuwepo na umeendelea kuwa kwenye mchakato.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie kwamba, hili neno la mchakato ndilo neno gumu sana na tena linaleta ukakasi mkubwa, kwa sababu mara nyingi sana kila kinachoshindikana kufanyika kwa kifupi tu utapewa taarifa kwamba, bwana hili jambo liko kwenye mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mradi mkubwa, kwa mfano Mradi wa Gesi Mtwara. Huu ni kati ya mradi ambao tungetegemea kwamba nchi hii isingekuwa hivi ilivyo. Tulipewa matarajio makubwa sana wakati ule mradi unaanza na kila mtu alielewa hivyo kwa sababu uhalisia ndivyo ulivyo. Nchi kubwa zilizoendelea zenye vyanzo vya gesi zimekuwa zikiendelea kwa kasi kubwa, lakini ule mradi bado umebakia kwenye mchakato. Ukiuliza utaambiwa kwamba hili jambo liko kwenye mchakato na kama kuna kiwango kimetumika au kimetusaidia ni kiwango kidogo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Mradi wa Gesi ya *LNG*, ndugu zangu wa Likong'o pale kuna wakati nalazimika kuwakimbia, nikipita pale hata kusimama sisimami kwa sababu nikipita pale swali la kwanza kuulizwa ni kuhusiana na mradi huu, kwamba unakuwaje na utaanza lini.

Mheshimiwa Spika, kuna *project* pia ambazo tumeshawahi kuzizungumza hapa; mimi mwenyewe nilishawahi kuzizungumzia

kama vile Mradi wa Magadi Soda, Engaruka. Mradi huu umeendelea kuwa kwenye karatasi kama miradi mingine. Kwa hiyo ukiangalia hapa ninachoweza kuzungumza ni kwamba Waziri aliye kwenye nafasi hii sasa achukue *reference* kwenye miradi ile yote ambayo iko kule nyuma na *failures* ambazo tumekutana nazo kusudi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, dakika moja malizia.

**MHE. ISSA ALLY MCHUNGAHELA:** ... tuweze kujirekebisha, twende katika hali ile inayotarajiwa na watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Ofisi hii muhimu sana. Kwanza, wazee wetu waliwahi kusema kwamba kupanga ni kuchagua. Kwa hili nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kuitenga Ofisi hii ya Rais, Mipango na Uwekezaji kusimama peke yake na kumpa mtu makini kabisa, Profesa Kitila Mkumbo kuisimamia. Namwamini Profesa na naamini kwamba anakwenda kutuongoza vizuri na kuweka mipango ya nchi yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sensa tuliyofanya mwaka 2022 inaonesha kwamba 76% ya Taifa hili ni vijana chini ya miaka 35. Kwa maana hiyo nilitegemea kwamba mipango yote ambayo tunaipanga sasa hivi katika kila sekta kwa asilimia kubwa ni lazima izunguke kundi hili kubwa, 76% ni nyingi sana na katika hili ningependa sana tuangalie changamoto ambayo ni ya kwanza kabisa kwa vijana wa Taifa hili, changamoto ya ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mipango yetu ni muhimu tukawaelekeza vijana kwamba nchi hii inakwenda wapi na wao waendeje. Ni muhimu kwa sababu sidhani kama kuna afya kuliacha kundi hili lijiindee katika karne hii ya 21 kuji-*surprise* na kuwa na kesho ambayo hawaitambui; kwenda na kutegemea kwamba tutaikuta kesho na tutapambana nayo tutakavyoikuta, sitegemei hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Katika nchi yetu sasa hivi kuna maeneo matano ambayo tunayaona kulingana na *projections* zake, utashi wa viongozi wetu na maendeleo ya sekta hizo, kwamba ni sekta ambazo zitaendelea ku-*boom* kwa miaka 20 mpaka 50 inayofika. Kuna sekta za utalii, viwanda, kilimo, uchukuzi na sekta ya uchimbaji. Nategemea katika mipango yetu tuoneshe ni namna gani tumejipanga kulielekeza kundi hili kubwa. Kwanza katika namna ya uelimishaji wake kwenda ku-*tackle* mabadiliko watakayoyakuta katika sekta hizi, lakini pili kuangalia namna gani tuna wa-*groom* kuendana na mabadiliko ya nchi hii katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaongelea biashara katika eneo huru la Afrika ambapo Afrika nzima, nchi zaidi ya 50 zitakuwa na soko huru la pamoja. Lazima katika mipango yetu tuoneshe ni namna gani tunakwenda kuwa-*groom* vijana wetu kupambana na uhuru huu ili kuweza kunufaika na eneo hili huru la biashara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima Wizara hii ituambie, je, inafurahishwa na vijana ambao wanatoka katika vyuo na vyuo vikuu vyetu katika nchi hii? Kama sivyo, je, tunaingiaje katika mpango wao wa kuweza kutuinua na kutuweka sawa ili leo hii tunapokuwa tunaongelea dira ya mpaka mwaka 2050 tuone namna gani vijana tunafika 2050 tukiwa imara?

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Profesa, anatuonesha namna ambayo amechukua maoni sehemu mbalimbali za nchi hii kwenye Dira hii ya 2050, waliotoa maoni haya 80% ni vijana kati ya miaka 15 mpaka 35. Hii inaonesha kwamba moja, vijana wanataka sana sana kushiriki kwenye kushauri namna Serikali na nchi yao inavyoenda na mbili, wanapenda na wao wahusishwe

kwenye mipango ya nchi hii. Kwa hiyo naiomba sana Ofisi hii katika kupanga mipango yake na namna inavyoshauri sekta mbalimbali, isilisahau kundi hili muhimu sana la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, nizungumzie sekta ya kilimo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Leo hii tunakwenda kuzungumzia sekta ambayo tunaitengea zaidi ya trilioni moja kwenye bajeti, kwa hiyo ni lazima tuonyeshe ni namna gani sekta hii inakwenda kutusaidia kuzalisha zile ajira milioni tatu zilizokuwa zimeahidiwa tangu mwanzo. Tuna Miradi kama ya *BBT*, naomba sana katika mipango yetu tuoneshe ni namna gani tunakwenda kushusha Mradi wa *BBT* kwenda kuwa *localized* kwenye wilaya na mikoa yetu. Hii itatuondolea sana changamoto na malalamiko ya vijana wengi kwamba wameachwa nje ya mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna maeneo ambayo yalikwishatolewa maelezo na Mheshimiwa Waziri Mkuu yatengwe kwenye kila halmashauri zetu ili kuhakikisha kwamba vijana wanapewa maeneo hayo kujiendeleza wao wenyewe. Maeneo haya yatumike kwenye miradi hii ili vijana kwenye wilaya zetu na mikoa yetu, waende kunufaika huko moja kwa moja na ndipo tutakapoona hizi ajira milioni tatu zinazalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazungumzia bajeti ya trilioni moja kwa ajili ya sekta hii. Naamini, tusije tukafanya kilimo cha kizamani. Ili tufanye kilimo cha kisasa ni lazima tuuangalie ugani kwa namna ya tofauti sana. Napendekeza tuanzishe mamlaka ya ugani kama tulivyoanzisha *TARURA* na *RUWASA*, ili kusudi mamlaka hii ishuke mpaka vijijini kwenda kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kulima kibiashara na kujiongezea thamani ya mazao wanayoyazalisha. Hivi ndivyo ambavyo tunaweza kwenda kweli kukomboa kilimo chetu na kukiweka kwenye *value* sawasawa na bajeti tunayoitengea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inabidi vilevile tuwekeze kwenye *value addition*, lazima tuwekeze kwenye viwanda. Kwenye hili nilikwishashauri ndani ya Bunge hili Tukufu, kwamba ni lazima tutoe *incentive* kwa Watanzania wanaotaka kuanzisha viwanda katika Serikali zingine za nchi hii tofauti na Dar es Salaam na Pwani. Baba

wa Taifa alikuwa na maana kubwa sana kuanzisha viwanda katika kila sehemu kulingana na mazao au na vitu vinavyopatikana kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kitu hatari sana kuona viwanda vyote vya nchi hii, *almost 80 percent*, viko sehemu moja. Siku maeneo haya yakipatwa na *emergency* yoyote, maana yake ni kwamba uchumi wa Taifa hili utayumba kwa kiasi kikubwa. Lazima tuoneshwe mipango na *incentive* gani watatoa kwa Watanzania. Iwe ni *incentive* za kikodi au mapunguzo ya thamani ya vitu kadhaa ili kusudi waweze kuanzisha viwanda na *processing industries* katika sehemu mbalimbali za nchi kwa ajili ya kusaidia wale wanaozalisha kule kule waweze kuona tija ya maendeleo haya ya miundombinu ambayo tunafanya kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kushauri, leo hii sisi watu wa Kanda ya Ziwa, tuna Ziwa Victoria. Sasa, ni lazima tuone mipango ya kutumia ziwa hili kuondokana na kwanza, shida ya maji na pili tuwe na *scheme* za umwagiliaji za kutosha. Ni aibu sana kwa sisi ambao tuna maji ya Ziwa Victoria kuanza kuja humu Bungeni na kulia changamoto ya maji. Tunalia na changamoto ya kwamba, kipindi cha kiangazi hatuwezi kulima ilhali tuna ziwa. Tunaweza kutengeneza *irrigation schemes*. Lazima kwenye mipango yetu Waziri atupe mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha maeneo haya yanazalisha kwa wingi kulingana na rasilimali tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina zaidi ya 51% ya Ziwa Victoria, kwa hiyo ni lazima tujue ni kwa namna gani tunakwenda kulitumia ili kukuza uchumi wetu hasa wa maeneo ambayo yanazunguka eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, kwenye sekta ya nishati nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu ameonesha dhima na nia ya moja kwa moja ya kufanya Watanzania tuanze kutumia nishati safi. Katika hili nampongeza sana. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa *scheme* waliyoifanya ya kugawa mitungi ya gesi katika sehemu mbalimbali. Nawapongeza kwa

sababu nimefuatilia katika bajeti watakayoileta katika Bunge hili Tukufu wamekwenda mbele zaidi, kuona ni namna gani tutapeleka nishati ya gesi asilia vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunagawa mitungi ya gesi lakini si Watanzania wengi watakaokuwa na uwezo wa kwenda ku-*refill* mitungi ile ikiisha. Ni lazima tutafakari namna gani tutakuwa na uendelevu wa *project* hii, hasa kwenye jamii za ufugaji. Wao tayari nishati ya kuzalisha hii gesi asilia wanayo ya kutosha na gharama yake ni nafuu. Tutenge bajeti twende tukawekeze huko ili tuwe na uendelevu wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *economies of scale;* nilitegemea, kwa sababu sasa hivi kuna matumizi makubwa sana ya hii nishati safi, basi angalau gharama ya gesi ingeshuka kulingana na matumizi yake makubwa. Naomba sana pia kwenye mipango tuliangalie hili la namna gani ya kushusha nishati hii ya gesi ili wengi waweze kuipata kwa wepesi. Kwa sasa hivi inatumika kwa wingi na kwa *economies of scale*, naamini kwamba tunaweza tukashusha. Tusije tukaishia ku-*mobilize* Watanzania kutumia nishati safi, lakini tukapandisha faida na kuwanufaisha watu kadhaa; wakati tungeweza kushusha na kufanya Watanzania wengi zaidi wakatumia nishati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho ni kwenye suala zima la uwajibikaji na utawala bora. Kwenye hili nampongeza sana Profesa kwa sababu katika hotuba yake, ameelezea misingi 10 ambayo ataisimamia kwenye Ofisi yake. Msingi namba nane amesema nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na msingi namba 10 amesema ni kusimamia mipango tutakayoipanga na kuitekeleza. Kwenye hili amenipa imani kubwa sana. Nimwombe sana Profesa ili tuweze kufikisha au kufikia kule tunakopanga kufikia ni muhimu sana tukaimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma. Kwa kufanya hivyo tu ndiyo itatuwezesha kufikia huko, kwa sababu tukiendelea kupanga mipango mizuri lakini fedha ambazo zinaenda kutimiza mipango hiyo hazifiki kule zinakotakiwa, naamini tutakuwa na mkwamo mkubwa sana katika mipango hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sofia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Ofisi hii ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Nafahamu kabisa kwamba Serikali imefanya vizuri sana kurudisha Ofisi hii baada ya kutolewa kwa muda fulani. Kama wenzangu walivyosema, tunaamini sana vijana ndio watakaolisaidia Taifa hili na Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Kitila ni kijana, hivyo naamini katika ujana wake atasimamia na kuhakikisha anasaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba, katika mambo ya uwekezaji kumekuwa na shida kidogo katika maeneo ya kuboresha mazingira ya uwekezaji. Ninapozungumzia maeneo ya mazingira ya uwekezaji namaanisha uwekezaji wa nje na wa ndani pia. Tukienda kwa wawekezaji wa nje, tuliomba hapa siku za nyuma kuwepo na *one stop centre*. Tukimaanisha *one stop centre* siyo majengo, kwamba ataiona *TRA* hapa au ataiona *OSHA* hapa, bali tunataka huduma na utendaji wa haraka. Hicho ndicho tunachokitaka na si majengo na kuwa na ofisi tu peke yake. Kwa hiyo, inawezekana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri anaenda kwa *speed* lakini akawa amewaacha wenziwe nyuma, wale watendaji wake. Kwa hiyo, naomba sasa *performance appraisal* aisimamie vizuri kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo wawekezaji wengi wanalalamika, anaweza akafuatilia kitu kwa mwaka mmoja au hata zaidi. Sasa siyo vizuri Mheshimiwa Waziri na ikumbukwe kwamba Tanzania hatujajitenga, kuna majirani zetu wanaweza wakawaalika hao wawekezaji. Kwa hiyo tusipofanya kazi kwa bidii na kwa u-*smart* tutaendelea kulalamika na kuwa watazamaji wa maendeleo yakienda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wawekezaji wa ndani, kuna watu wanawekeza; tumesema viwanda vya kati ni viwanda

muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa hili. Kwa mfano mtu anafungua kiwanda cha kusaga unga na ni mzawa, anapata shida kubwa sana kupata *documents.* Anapata shida sana kila siku kuripoti nenda hapa rudi hapa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema, atumie elimu yake na ujana wake ili kuhakikisha kwamba Taifa lake linasonga mbele. Tunaomba uwekezaji huu uwe wa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imetoa maoni hapa kuhusiana na kutenga ardhi ya wawekezaji. Ni vyema kujua ni eneo gani wawekezaji watakuwepo. Ni kweli wakijazana sehemu moja pia pana madhara na hatimaye isiwe mtu anapotaka kuwekeza kitu tunaanza kuhangaika tunamweka wapi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna wawekezaji hasa kwenye sekta ya madini wamechukua maeneo makubwa kabisa. Ikumbukwe kwamba watu wetu wamezaliwa katika maeneo haya. Unaenda kwenye maeneo kama Nyamongo unakutana na watu waliozaliwa pale, maisha yao yote wako pale; lakini anakuja mwekezaji anachukua eneo kubwa na halitumii kwa wakati na wale watu ambao ni wazawa, wanakosa sehemu ya kufanya ule uchimbaji mdogo mdogo. Kwa hiyo nafikiri ili uchumi uendelee ni lazima kwanza kila mtu kuanzia ngazi ya chini awe anashika hela kiasi. Kwa hiyo tunaomba waweke mazingira mazuri kwa vijana wetu, lakini na ardhi yetu pia itunzwe na mtu anapopewa ile ardhi aiendeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashamba makubwa kama vile ya Mbarali yamekaa kwa miaka na miaka na wananchi wanaozunguka maeneo yale wanapata shida ya kulima; mwisho wa siku wanaenda kukodisha na kumpatia mwekezaji faida na kumwacha Mtanzania katika hali isiyofaa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri asimamie maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu uwekezaji wa vijana. Tumemaliza sensa juzi hapa, leo hii tuna asilimia kubwa sana ya vijana. Vijana hawa tusipowawekea msingi wa kujua ni namna gani wanaweza kutoka katika maisha yao tutakwama kama Taifa. Naomba sana tuhakikishe vijana hawa wanajengewa uwezo wa kuwekeza kwa *level* zote; *level* ya chini, ya kati na ya

juu. Tuhakikishe, kama ni vijana tunawasimamia. Kwa mfano Soko la Kariakoo, pale utakuta kuna wawekezaji wenye rangi nyeupe, naomba nisitaje mataifa yao kwa sababu unajua hili ni Bunge, siwezi kuwataja. Naomba wawepo wazawa zaidi na kwa upande wa wageni, kutokana na mitaji waliyonayo wapewe uwekezaji mkubwa ili uwekezaji huu mdogo mdogo waachie watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii huwezi kwenda kwenye nchi jirani ukasema kijana wa Kitanzania anakwenda kuwekeza eneo ambalo jirani yetu Mkenya, Mganda na mtu yeyote akaacha watu wake akawapa watu wako; siyo sawa, naomba msimamie hilo. Mtazame hata hao wanaokuja kuwekeza kwenye madini pia, ni lazima tuhakikishe watoto wetu wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, kuna ujanja unaotumika, mtu anakuja kuwekeza anatafuta bosheni, anamtafuta Mtanzania, anachukua *document* zake halafu inaonekana kama na yule Mtanzania ni mwekezaji, lakini baada ya muda mfupi wanamwacha kwenye mataa na watu wetu elimu hiyo hawana. Naomba kama Serikali wasimamie hilo ili kuhakikisha Watanzania hawa hawadhulumiwi na wanapata haki, *fifty-fifty* ile ambayo imeandikwa *BRELA* au sehemu nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iongeze mitaji kwenye mashirika ya umma ambayo tunafikiri yalianzishwa kwa ajili ya kuongeza uchumi wa Taifa letu. Tunaomba wapewe mitaji. Kuna wakati unaweza ukalaumu, ukasema watu wetu hawafanyi kazi lakini bajeti inapitishwa katika Bunge lako, 40% ndiyo inawafikia; wanawezaje kuendelea. Tunaomba sana, Bunge ni taasisi kubwa, inapopitisha fedha halafu 40% au 35% tu ndiyo inatoka, nafikiri hatuwatendei haki wataalam ambao wamesoma kwa kodi za Watanzania, naomba Serikali iwekeze fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viongozi waliotutangulia kama Mwalimu Nyerere walifanya mambo makubwa, alipoanzisha ZZK - Mbeya alijua kwamba Nyanda za Juu Kusini kunahitaji dhana za kilimo, leo hii yamekuwa magodauni ya pombe. Alipoanzisha viwanda mbalimbali vingine vikubwa, wao wamesoma wanaelewa na ndiyo maana walienda shuleni wengine walikimbia, tukakimbia

wao wakaenda, basi wachangamke, kuangalia, kuchanganua vizuri na kujua ni namna gani tunaweza tukalisaidia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani bado tuna nafasi ya kutengeneza. Madini yetu yatatuongezea sana fedha. Leo Mwadui wamechimba miaka 84 kama siyo 86, lakini *still* mzigo bado uko chini, mikataba kama ilikuwa mibovu basi tutafute namna ya kuweka mikataba vizuri ili madini yatuokoe. Pia tuna kilimo, kwenye kilimo tunayo nafasi ya kusaidia Taifa hili. Tuwekeze kwenye kilimo, tuongeze bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nitaunga hoja pale ambapo Mheshimiwa Waziri atakuja na majibu mazuri na mpango unaoweza kumsaidia Mtanzania, nitamuunga mkono kama atasema vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza kabisa, napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa hotuba ya bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ambayo imewasilishwa hii leo. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa wananchi wenzangu wa Bagamoyo kutokana na mvua kubwa iliyonesha leo na kusababisha nyumba nyingi kuingia maji na watu wengi kupata karaha kidogo ya hapa na pale, nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, bingwa *number* moja wa kufukuzia na kufuatilia uwekezaji katika nchi mbalimbali duniani na kuuleta hapa katika nchi yake. Tunampa pongezi sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpa pongezi Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo pamoja

na Katibu Mkuu wake Bi. Tausi Kida na viongozi wote wa Wizara pamoja na Taasisi ambazo zipo chini ya Wizara yao kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Spika, niipongeze tena Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Uwekezaji wa viwanda Tanzania umekuwa mkubwa sana. Leo hii nashukuru katika Mkoa wetu wa Pwani kuna viwanda vingi sana, nafikiri ndiyo Mkoa ambao unaongoza kwa viwanda katika nchi hii. Ukianzia Kibaha – Mkuranga mpaka ukija Bagamoyo, kuna viwanda vingi vya kutosha, hii ni juhudi ya makusudi inayofanywa na Serikali pamoja na viongozi wetu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nataka kuzungumzia masuala machache tu. Suala kubwa ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *EPZA*. Mnakumbuka mnamo tarehe 13 Septemba, 2023 Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji baada tu ya kuchaguliwa siku siyo nyingi sana kwa makusudi kabisa alifunga safari kuja Bagamoyo. Alipokuja tulifanya kazi kubwa mbili:-

(i) Tulitembelea miundombinu iliyokuwa ikijengwa katika eneo ambalo linakusudiwa kujengwa viwanda; na

(ii) Tukaenda kufanya kazi moja ya kuzindua *masterplan* ya *EPZA* (Kongani ya Viwanda) ambayo kwa kipindi kile ilivyowasilishwa ilisema kwamba itagharimu shilingi trilioni 11, namshukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, katika ile kazi ambayo tulikwenda kuitembelea ya kukagua miundombinu ya Mradi wa *EPZA,* napenda kuchukua nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, bado ile kazi inasuasua. Nimepitia hotuba yake na nimesoma hapa kwamba kilometa tatu za lami mpaka sasa hivi zimekwisha kwa 70% tu, 30% bado haijaisha. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri ile sehemu ni muhimu sana, wawekezaji hawawezi kuja wanapoona sehemu yoyote ambayo haina miundombinu. Tujitahidi, Ofisi yake ihakikishe kwamba ile miundombinu inamaliziwa ili wawekezaji waweze kuja na kuwekeza katika sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimetumwa na Wanabagamoyo ambalo hilo ni masikitiko yao makubwa sana na changamoto kubwa sana kwao na hasa wananchi wa Kata ya Zinga, ni kuhusu suala la fidia. Toka *EPZA* wachukue lile eneo sasa hivi ni mwaka wa 14 wananchi wanahangaika hawajui lini watalipwa fidia zao. Hata hivyo, nimepata faraja kidogo katika hotuba ya bajeti ya Waziri upande wa vipaumbele na kazi zitakazotekelezwa amelizungumzia kidogo suala la fidia. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, muda umekwenda sana miaka ni mingi, hawa watu wanateseka, maeneo yao yamepigwa pini, leo hii mtu hata akienda ardhi akitaka kuuza hata hekari moja, hawezi anaambiwa hili ni eneo la *EPZA* wakati yeye mpaka sasa hivi hajafaidika chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wa vitongoji mbalimbali, kuna Kitongoji cha Kibuba, Gongoni, Mikungalungo, Kokoto, Mkusangalakichwa, Mkunguni, Dagaza, Gwazo, Kondo, Gongoni, Chaponda, Bondeni na Changuruwe wana masikitiko makubwa, wanahitaji Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma, ikiwezekana bajeti ya mwaka huu wawafikirie angalau kupata chochote kwa sababu ni miaka 14 sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika huu mpango wa *EPZA*, kuna maeneo ambayo wenzetu wa *EPZA* wameyatoa katika mpango wao. Nafahamu ikiwemo Kijiji cha Mlingotini wamekiondoa katika mpango wao wa *EPZA*, kwa hiyo yale maeneo yatabakia. Naomba maeneo yote yale ambayo yatabakia, basi kwa wananchi wale iende ikaondolewe *GN*, ilimradi wananchi wale waweze kuyamiliki maeneo yao ili wafanye maendeleo yao wanayoyataka, kwa kweli hii itawasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nigusie pia mpango wa Bandari ya Bagamoyo, kwa kweli hakuna kitu ambacho Serikali inakipoteza au inakwenda kukipoteza kama kutoharakisha ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Kwa kweli, bandari ile ikijengwa itasaidia sana kuondoa msongamano wa meli ambazo zinarundikana katika Bandari ya Dar es Salaam na kuiingizia faida nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, leo hii, kama unasafiri unakwenda Zanzibar meli zimejaa, zinakaa mwezi mzima hazijashusha mzigo, kwa nini, basi mpango wa kujenga Bandari ya Bagamoyo usiwasilishwe mapema sana. Tunamtegemea sana Mheshimiwa Waziri, yeye ni Profesa wa Mipango, ni Profesa wa Uchumi, ajaribu kuangalia mpango gani wa haraka ambao anaweza kuufanya kuhakikisha Bandari hii ya Bagamoyo inajengwa kwa haraka zaidi ili kupunguza msongamano wa meli pale Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuisaidia nchi yetu katika mpango mzima wa uwekezaji. Mheshimiwa Rais, amejipambanua wazi katika kila sekta, katika Sekta ya Utalii, ameleta *Royal Tour*, katika sekta za viwanda anasafiri kila siku na wawekezaji wanakuja kwa hiyo, nimpe pongezi zake za pekee kabisa kwa kazi hiyo kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumwambia tena na tena Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la fidia kwa Wanazinga. Ingekuwa ni kipindi ambacho Ofisi hii ameishika kwa muda mrefu ningeshika shilingi, miaka 14 ni mingi sana, lakini, kwa sababu Ofisi hii ameichukua juzi, hakuna sababu ya kufanya hivyo. Tutaenda mwakani kama Wanazinga, Wanamlingotini pamoja na hivi vitongoji nilivyovitaja, kama hakuna chochote kitakachofanyika basi kwa kweli itakapofika bajeti ya mwakani ataniona mbaya, nitakuja kukamata shilingi hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunipa nafasi hii ya kipekee ili niweze kuchangia katika Ofisi hii muhimu ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo ameanza kuifanya vizuri, nampa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi ambazo amezifanya katika kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano, ameutekeleza vizuri sana. Tuna kila sababu ya kumpongeza, kwa sababu, tunaona kabisa kwa mfano sasa hivi Bwawa la Nyerere limeshaanza uzalishaji na tumepata faraja sana juzi tuliposikia sasa Tanzania umeme tunaozalisha ni mwingi kuliko mahitaji. Kwa kweli hiyo ni pongezi kubwa sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mradi mwingine wa kielelezo, tulianza ujenzi wa *SGR* ambayo tumetumia muda mrefu kuujenga, lakini kipande cha Dar es Salaam mpaka Dodoma kimekamilika, ni faraja kubwa na ni pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Jana treni hiyo imefanyiwa majaribio, imetumia masaa manne kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, ni faraja kubwa sana na ni maendeleo makubwa. Wale waliokuwemo kwenye hiyo treni jana wakikusimulia unatamani hata leo na wewe angalau uende, kwa kweli ni maendeleo makubwa ambayo tumeyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mafanikio makubwa Rais amenunua ndege ya mizigo, tumenunua ndege za abiria ili kuchochea uchumi, hayo ni mafanikio makubwa. Zaidi ya hapo tumeona ujenzi wa majengo ya Ofisi hapa Makao Makuu Dodoma katika eneo la Mtumba, tunaona majengo yanaota kama uyoga kwa sababu ya kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais. Majengo yanapendeza, Mji wa Magufuli unapendeza, Dodoma imebadilika, ni kwa sababu ya kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tumeona jinsi alivyofanya kwenye upande wa elimu, karibu majimbo yote madarasa yamejengwa ya shule za msingi, shule za sekondari na vyuo vinajengwa. Kwenye afya, hospitali zinajengwa, vituo vya afya na zahanati.  Kwenye maji sijui tutumie maneno gani ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, wakulima amewawekea ruzuku, ambayo imewasaidia sana wakulima kuweza kupata pembejeo. Pembejeo za kilimo ambazo zimesaidia sana upatikanaji wa chakula na malighafi kwenye viwanda vyetu. Kwa kweli, ni kazi nzuri ambayo tumeiona na wakulima wa nchi hii kama hawatatoa kura watakuwa watu wa ajabu, lakini, imani yangu watatoa kura kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu wamepata ruzuku na imewasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, tumeona jinsi alivyojenga meli na vivuko ambavyo vinajengwa. Tulienda kule Ziwa Victoria tukaona meli kubwa ambayo imeundwa hapa Tanzania, imezinduliwa na imeanza kufanyiwa majaribo. Meli ambayo huwezi kuamini kama kweli imeundwa hapa Tanzania, ni kazi kubwa ambayo wameifanya, tumeona vivuko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo viwanja vya ndege vinajengwa kila mahali, tumeona kwenye Mhimili wa Mahakama kumejengwa jengo zuri na la kisasa hapa Dodoma ambalo linapendeza sana. Sidhani majengo kama yale kama yapo mahali pengine kama ambavyo linaonekana japo sijaingia ndani kwa nje tu kunaonesha jengo la Mahakama lilivyopendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hajaishia hapo na sisi hapa Bungeni amesema tupanue eneo, nimesikia kuna fununu tunaanza kutoa fidia kwa majirani hawa ili tupate eneo kubwa la Bunge na tuweze kufanya mambo mengine mengi. Kwa kweli, hiyo ni kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya, kwa hiyo, amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango yetu na bajeti ya Mheshimiwa Waziri lazima itupelekee katika kukamilisha Dira yetu ya Miaka Mitano. Dira yetu ya mwaka 2025 ambayo inaenda kukamilika na tunakuja na dira nyingine mpya. Dira yetu inasema; "Tunahitaji maisha bora kwa kila Mtanzania," kwa hiyo, hii Bajeti ya Mipango itupelekee namna ya kuboresha maisha ya Mtanzania. Sasa hivi maisha katika maeneo mengi wananchi wanalalamika lalamika, maisha hayajawa mazuri. Kwa hiyo, lazima kwa kweli Ofisi hii sasa

ituambie namna maisha yatakavyoboreka, yatakavyokuwa mazuri, Watanzania watakavyoweza kufurahi. Vilevile tunataka Ofisi hii itupeleke mahali pa kutuambia namna tutakavyoweza kupambana na umaskini mkubwa katika maeneo mbalimbali. Umaskini tulionao huu ndiyo unaoifanya nchi yetu ambayo ni tajiri sana ionekane kama bado haina maendeleo, kwa hiyo, lazima itupeleke hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa tuko katika kipato cha kati cha chini, lazima twende kwenye kipato cha kati cha juu na hatimaye ndoto yetu itupeleke kuwa kwenye nchi za kipato cha kwanza au cha juu kabisa, kwa hiyo, lazima twende hivyo. Mipango yetu lazima pia ituambie tunaendaje kulinda amani na utulivu na umoja wa nchi yetu, lazima mipango itupeleke hapo na mipango hii itupeleke katika namna tutakavyoimarisha utawala bora kwa Watanzania, tutakavyojenga jamii iliyoelimika na tutakavyojenga uchumi wa ushindani. Haya yote kwa kweli nina imani kwa heshima kubwa, Profesa ataitendea kazi nchi hii na atayazingatia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kazi kubwa iliyofanyika kuna mambo tulipendekeza kama Bunge yamefanyiwa kazi na kuna mambo bado hayajafanyiwa kazi sawasawa. Tunaamini tunaendelea kupendekeza, kwa mfano, sasa hivi tija ni ndogo sana katika maeneo mengi, tija kwenye biashara, viwanda, kilimo na uzalishaji iko chini. Hii inatokana na kwamba hatuna taasisi inayosimamia tija katika nchi hii. Mheshimiwa Waziri, ifike mahali sasa waangalie uwezekano wa kuanzisha Shirika la Kuongeza Tija, Shirika la Tija lilikuwepo kule nyuma, lakini tulilifuta. Naamini tulikosea kulifuta kwa sababu tija ni muhimu sana ili nchi iweze kupiga hatua, kwa hiyo, nashauri kwamba hili ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, yapo mambo ambayo yanachukua fedha nyingi sana za nchi yetu, kwa mfano, ununuzi wa magari, magari yote tunayoyaona Tanzania yanatoka nje na yote tunatumia fedha za kigeni kutoka nje. Siamini kabisa kwamba toka tumepata uhuru mpaka leo Watanzania hatuwezi kutengeneza gari au hatuwezi kuunda magari au tukawa na viwanda vya kuunganisha magari. Kwa hiyo, mipango hii lazima itusababishie sasa ufike wakati kama tumeweza kuunda meli ya

kisasa kule Mwanza, tumeweza kuunda vivuko vya kisasa, basi tuna uwezo wa kutengeneza magari hata madogo, magari ni muhimu. Kwa hiyo, nashauri Serikali waangalie uwezekano wa kuanzisha Kiwanda cha Kutengeneza Magari hapa Tanzania. Tumechoka sasa kuendesha magari ya mitumba, tunataka tuendeshe mapya yaliyotengenezwa hapa nchini na naamini tukiwa na dhamira ya kweli tutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tulipendekeza kule Tunduma mizigo karibu 70% inapita pale, tukaomba kwamba paanzishwe Bandari Kavu ili mizigo isafirishwe na treni ya *TAZARA* kutoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka pale, ikifika pale tukiwa na Bandari Kavu, wananchi wa kutoka Zimbabwe, kutoka Malawi, kutoka Kongo, kutoka Zambia waje wachukue mizigo pale. Tutakuwa tumerahisisha shughuli za biashara na tutaweza kupata mapato makubwa, lakini pia hata nchi itaweza kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, Songwe ni Mkoa wa mwisho, tunaita ni mkoa kitinda mimba kwa kuanzishwa hapa nchini. Sasa Mheshimiwa Waziri ifike mahali kwa sababu, tunataka kujenga jamii iliyoelimika, basi mipango hii itupeleke kuanzisha vyuo, matawi ya vyuo iwe vyuo vya kati au vyuo vikuu, tunahitaji vijengwe Songwe ili wananchi wa Mkoa wa Songwe waweze kupata elimu katika maeneo hayo, lakini si wananchi wa Songwe tu, tunataka na nchi jirani watuletee dola kwa kuja kusoma hapa. Vyuo vyote vilivyoko hapa tukivijenga vizuri, tukatoa elimu iliyo bora, wale watakuja kusoma hapa, tutapata dola. Tunaona Uingereza wanapata hela nyingi sana, Malaysia…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, Malaysia na maeneo mengine wanapata hela nyingi sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumwongezea Taarifa Mheshimiwa Hasunga kwamba, kwa Mkoa wa Songwe, tunaomba waanze na kupandisha Chuo cha *DIT* kukifanya kiwe Chuo Kikuu ili kiwe chuo cha kwanza kwenye Mkoa wa Songwe.

**SPIKA:** Hebu nikuelewe kwanza mimi kabla sijamwuliza unayempa Taarifa?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, kule Mkoa wa Songwe kuna Chuo cha *Dar es Salaam Institute of Technology* ambacho kinatoa masomo kuanzia *Certificate* mpaka *Diploma*. Kwa kuwa, tunatamani Mkoa wa Songwe upate vyuo vikuu na hakuna chuo hata kimoja, tunaomba tuanze na hicho kipandishwe hadhi kiweze kutoa *degree* ili tuweze kupata hizo dola nyingi ambazo Mheshimiwa Hasunga anasema.

**SPIKA:** Naona huyu alipaswa apewe nafasi yake achangie kwa sababu, nadhani kitu anachoongea ni kitu tofauti. Kama kinaitwa *Dar es Salaam Institute of Technology* maana yake ndiyo tawi la *Dar es Salaam Institute of Technology*, sasa kama inabidi kiwe chuo kikuu maana yake kianzie kule ambapo ni chuo mama.

Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa mchango wake, Mheshimiwa Mbunge wa Momba, ni mzuri na kweli tunahitaji tuwe na matawi ya vyuo vikuu katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kupendekeza, kama muda utaruhusu, ni lazima katika mipango yetu twende tukaangalie namna taasisi zetu na mashirika ya umma yanavyofanya kazi. Sasa hivi zipo taasisi ambazo hazina faida, zimekuwa ni mzigo kwenye Serikali Kuu. Tufike mahali wafanye uchambuzi wa kina kuangalia kila shirika na umuhimu wake, faida zake na kwa nini liendelee kupata fedha kutoka

Serikali Kuu. Hilo ni muhimu na litaipunguzia Serikali matumizi ambayo sio ya lazima. Sasa hivi kila mtu anapata hela kutoka Hazina, hafanyi kazi sawasawa, kwa hiyo, baadhi ya taasisi zirekebishwe, naamini hilo litatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwa nusu dakika, naomba mipango yetu ituoneshe namna tunavyoenda kuimarisha sekta binafsi. Bila kuimarisha sekta binafsi, bila kuiwezesha, bila kuchochea uwekezaji kwenye sekta binafsi, bado mzigo utakuwa kwenye Serikali Kuu katika kubeba majukumu mbalimbali. Haya majukumu yanaweza kufanywa na sekta binafsi vizuri iwapo Serikali itahamasisha na itailinda na kuchochea sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Exaud Kigahe. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa. Kipekee kabisa naipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya katika Taifa hili, hususan katika Ofisi hii inayoongozwa na mtu bingwa kabisa, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa mimi binafsi nayaona matumaini makubwa ya Tanzania kuwa nchi ya asali na maziwa kwa uwepo wa Ofisi hii ya Rais, Uwekezaji. Hakika Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anapaswa kupewa maua yake kwa uwepo wa Ofisi hii ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *specifically* naiona dhamira pana na akili kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hasa pale ambapo ameona ni muhimu vipaumbele vya Taifa hili kuwa *fixed*, kuwa *pin pointed,* sio kila anayekuja katika Taifa hili anakuja anatengeneza vipaumbele vyake. Hili ni jambo la busara, hekima

na akili kubwa kufanywa na mwanamke shupavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Jambo hili nakumbuka limesemwa kwa miaka mingi kwamba, tunahitaji vipaumbele vya Taifa letu viwe *fixed*, lakini leo tukiwa tunatimiza miaka 60 ya uhuru mwanamama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja kulitekeleza jambo hili, Mheshimiwa Mama Samia anastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiukweli kabisa natamani kuwashawishi Watanzania kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nikitambua pia michango mingine ya viongozi watangulizi wa Taifa letu, lakini natamani miaka 60 mingine ya uhuru inayokuja Taifa hili liendelee kuongozwa na wanawake ili tuweze kupima maendeleo ya miaka 60 ya uhuru na maendeleo, miaka 120 ya uhuru wa Taifa hili, Taifa hili litakuwa limefika wapi.

Mheshimiwa Spika, naona kabisa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inanipa mwangaza kwamba, kuna wanawake wengi wazuri kwenye Taifa hili wanaweza wakalisogeza mbele kabisa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha njia na ameonesha maono makubwa ya kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 41 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji ameeleza vizuri kabisa kwamba, Serikali ilichukua vile viwanda nane ambavyo vilibinafsishwa na kuhangaika kutafuta wawekezaji. Viwanda vinne kati ya vile vimepata wawekezaji, viwanda vingine kikiwemo cha *Mkata Saw Mills* bado hakijapata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kuikumbusha Serikali kwamba, jumla ya viwanda vilivyofungwa Mkoani Tanga ni 15, wakati Serikali inatafuta namna nzuri ya kuboresha uwekezaji nchini, pamoja na kutengeneza sera, pamoja na kupitia Sheria, naona ipo haja ya Serikali kuhakikisha inakaa chini na wawekezaji ambao wamevifunga viwanda vyao kule Tanga na wapo tayari kuvifungua, ili kuja na *solution* ya pamoja kuhakikisha viwanda vile vinafunguliwa. Viwanda vingine ni vipya kabisa, sitaki kuamini, sijawa *convinced* na *logically it does not imply* kwamba, watu wamefanya *investment* kubwa bila kufanya tafiti ya kutosha. Sisi

Tanga tunazalisha ngano, kule Lushoto tuna mashamba ya ngano, haiwezekani kiwanda cha kuzalisha unga wa ngano *Pembe Flour Mills* kiwe kimefungwa *within very short period of time,* inaonesha ni *failure* ya Serikali katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna viwanda vingi, sisi Tanga tunazalisha mkonge, inakuwaje kiwanda cha mabusati Tanga kifungwe? Vilevile tunazalisha nyanya, inakuwaje kiwanda cha kuzalisha nyanya kule Bumbuli kifungwe? Naiomba Serikali na natamani sana kusikia tamko la Serikali wakati wanakuja ku-*wind up,* watuambie mpango wao katika kuhakikisha wanakaa chini na wawekezaji walio tayari ili kuhakikisha viwanda vile vilivyofungwa Mkoani Tanga vifunguliwe na viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali, lakini vilevile kuna haja ya kuona umuhimu wa kufanya tafiti za kina ili kujua ni kwa nini viwanda hivi vilifungwa. *Imagine* katika mkoa ambao tumefanya *investment* kubwa ya bandari, ili meli kubwa zije ina maana ni lazima *production* iwepo, ni lazima viwanda vifanye kazi. Nina hakika miaka ile ya 80 kwa Mkoa wa Tanga kuwa na viwanda hivi vingi, kivutio kimojawapo kilikuwa ni bandari. Mtu anazalisha kiwandani, anapeleka mzigo bandarini unaondoka.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa huu tumefanya *investment* nzuri, Serikali ni lazima ione namna, ili *return of that investment* iende *simultaneously,* ni lazima tuchochee na vilevile kuhakikisha viwanda vinafufuka na *raw materials* ambazo zipo Tanga ziweze kuwa *processed* kwenda kwenye *products* badala ya kuviacha viwanda hivi vife. Viwanda 13 kufa, ni vingi sana, Tanga Jiji peke yake kuna viwanda sita; *Tip Soap Industries* kimekufa, *Gofu Mats* kimekufa, *Sandali Wood* kimekufa, *Play and Panel* kimekufa, *Bajader Packaging* kimekufa, *Usambara Drinking* kimekufa, *Usambara Factory* kimekufa na *Mkata Saw Mills* ndicho ambacho wanasema wanakitafutia uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingine ni *Kilindi Industrial Cooperative* kimekufa, *Derema Division* ya chai, *Namunga Division* ya Muheza, *Sange Salt* cha Pangani vyote hivi vimekufa. Wakati tunaweka mipango ya kusema tutatumia uchumi wa *blue* vizuri tunaruhusu Kiwanda cha Kutengeneza Chumvi Pangani

kinakufa. Kwa kweli, inaleta *contradiction* namna ambavyo tunaunganisha mawazo pamoja ili tupate yale matokeo tunayoyahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo naona kabisa wanataka kuwekeza katika *human capital,* hili ni jambo la kupongezwa. Tunapozungumzia *investment* ni lazima tuone namna *human capital* nayo inakuwa na ubora gani. Ndugu yangu pale alivyoitaja *DIT* akanikumbusha usemi au tunaita *University Motto or Institute Motto* ya *DIT* inasema hivi *"In Every Skilled Hand there is an Innovative Mind"*. Kama hatuwezeshi vyuo vyetu kufanya fanya, *there is no innovation that can happen in our country*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inaamua kuondoa mafunzo ya katikati, yale tunayaita *study tours,* ili kuweza kuboresha *productions,* ili kuboresha uhamishaji, tunaita mafunzo ya kisayansi katika uzalishaji, kuhamishia mafunzo ya kisanyansi katika uzalishaji. Ni lazima tuweze kuzalisha na tuweze kuhakikisha watu wanawezeshwa kufanya fanya zaidi, lakini wanafunzi wetu hawawezeshwi kufanya fanya. *We must help our kids from the very early age* kuweza kufanya fanya na hili linahitaji *investment* ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuainisha *tips* hizi ambazo zinatumika kuanzisha shule 100 za amali, *its good initiatives,* hususan kwa huu mtaala mpya wa elimu ambao unataka vitendo zaidi. *So, it is also a good initiative,* lakini ndani yake kama itakuwa *more theoretical* na hakuna kufanya fanya, *frankly speaking* hatuwezi kuhamishia maarifa ya kisayansi katika uzalishaji, lazima wanafunzi wawezeshwe kufanya fanya. Serikali ipange kurudisha zile *study tours* kwa walimu na wanafunzi wao, ili waweze kwenda kwenye maeneo ambayo mambo yanafanyika kwa vitendo na wanafunzi waweze kujifunza siyo kusubiria tu *industrial practical training* mpaka akitimiza mwaka mmoja wa chuo haitoshi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakuona unacheka Rais wa Dunia. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge nilikuwa najiuliza ni sentensi inakuwa ndefu ama, hiyo kufanya fanya ni nini? Kufanya fanya ni nini, ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawasawa? Maana umelirudia sana hilo neno, kufanya fanya nini?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namaanisha mikono yetu iwe imetengenezwa kuweza kufanya *hands on practices like that.* Yaani ile, sijui kama nimeeleweka? *I am sorry,* ile mazoezi kwa vitendo.

**SPIKA:** Haya. Kwa hiyo wajifunze kwa vitendo ama?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, wajifunze kwa vitendo lakini ni ili...

**SPIKA:** Kujifunza kwa vitendo ama kujifunza huku wakifanya kazi, wakifanya jambo fulani?

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, *what can I say.* Ni ile hali ya, yaani natamani mtoto kuanzia akiwa mdogo, anapokuwa nyumbani mpaka akiwa kwenye *level* za vyuo aweze kuwa *trained* katika hali ya kupenda ku-*practice* kufanya fanya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige naona unataka kuzungumza, lakini usituangushe kama mara ya mwisho nilikupa kazi ya kutupa neno kwa Kiswahili ukatupa ambalo halipo kabisa kwenye kamusi. Haya tusaidie, kufanya fanya ni nini?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi nimefanya fanya pia, maana yake ni kazi za mikono. Ni kazi za mikono, ndiyo kufanya fanya, anamaanisha hiyo.

**SPIKA:** Kwa maelezo aliyoyatoa hapa mwisho nadhani tumemwelewa. Hakukusudia tu kusema kazi za mikono kwa

sababu hata kuosha kikombe nyumbani ni kazi za mikono. Nadhani kile alichotaka kusema tumemwelewa. Kwa hiyo, Taarifa zetu Rasmi za Bunge zimeshakaa kwa ufafanuzi mzuri.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo kwa hotuba nzuri ya bajeti. Pia niwapongeze wasaidizi wake Wizarani kwa jinsi ambavyo wanasukuma ajenda za uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naishauri Serikali isimamie vyema utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ili kuisaidia nchi yetu kuzalisha kwa kutumia rasilimali tulizonazo na kutuletea maendeleo makubwa na kuongeza pato la Taifa. Pa kuanzia ni vyema Serikali ikabiliane na vikwazo vinavyoikabili Sekta ya Uwekezaji ambavyo baadhi ni vikwazo vya kikodi, vikwazo visivyo vya kikodi, vikwazo vinavyohusiana na utaratibu wa masuala ya uwekezaji na vikwazo vya wezeshaji uwekezaji hasa wale wa ndani. Kama Serikali itaangalia kwa makini vikwazo hivi, itakuwa imeweka mazingira wezeshi ya uwekezaji ili kuwawezesha wadau kushiriki kwa mafanikio na kufurahia matunda ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, utahusu maeneo ya kimkakati ambayo Serikali inatakiwa kufungua fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo makubwa yanayoweza kutumika kuzalisha mazao mbalimbali ya kimkakati. Maeneo mengi ya Tanzania hupokea mvua za kutosha na pia yana maji yanayoweza kutumika kumwagilia na kuzalisha mazao, kwa mfano, maeneo ya Iringa, Mbeya, Njombe na *West Kilimanjaro* yana maeneo makubwa yanayofaa kuzalisha mazao ya kimkakati ya ngano na shayiri ambayo yana soko kubwa la ndani na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Mafuta ya Kupikia, nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kuwekeza kwenye kilimo cha

mazao ya mafuta ya kupikia kama vile alizeti, michikichi, karanga, ufuta na nazi. Uwekezaji huu kwenye kilimo ni vyema ukaenda sambamba na uanzishaji wa viwanda vya kuyaongezea thamani mazao hayo ili tuzalishe mafuta yetu na kuyauza ndani na nje. Kuna uwezekano mkubwa sana wa kuvutia wawekezaji wa sekta ya mafuta ya kula katika Mikoa ya Singida, Tabora, Dodoma, Simiyu, Kigoma, Manyara, Lindi, Mtwara, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo uwekezaji wake utakuwa na tija kubwa ni kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya mbolea na viuatilifu. Nchi yetu ni nchi ya kilimo na Serikali yetu inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mbolea na viuatilifu vya viwandani. Soko la bidhaa hizi ni kubwa hapa nchini na kwa majirani zetu. Naishauri Serikali ihamasishe na kuweka mazingira rafiki ya kuwekeza katika maeneo haya ili kulisaidia Taifa na wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa kuboresha huduma za afya kwani hospitali, vituo vya afya na zahanati zimetapakaa nchi nzima. Kutokana na hili, ni wakati muafaka sasa Serikali ikahamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya dawa kwani soko la ndani lipo na ziada itapelekwa nje. Kwa kufanya hivi, nchi yetu itakuwa imejinasua kwenye tabia ya kuwa mwagizaji wa dawa kutoka nchi ya India na nyinginezo za nje.

Mheshimiwa Spika, fursa nyingine ni kuwekeza katika utengenezaji wa pikipiki hapa nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kuna matumizi makubwa ya pikipiki hapa nchini. Vijana wengi wamejiajiri kwenye biashara ya pikipiki. Hivyo basi, kuna umuhimu wa kuwa na viwanda vya pikipiki na ni vyema Serikali ikaweka mazingira mazuri na kuvutia wawekezaji katika eneo hili. Tukiwa na mwekezaji wa kimkakati, bei za pikipiki zitakuwa chini na vijana wataweza kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itahamasisha uwekezaji kwenye maeneo haya machache niliyoainisha, hii italisaidia Taifa katika safari yake ya kukuza uchumi na kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia bajeti hii ya Uwekezaji, lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake kubwa za kutengeneza ustawi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaase wasaidizi wake kwenda na kasi yake, ni vyema wakajibidisha kumwelewa, kufahamu matamanio yake, maono yake na matokeo anayoyatarajia. Kwa jitihada zake binafsi amepandisha idadi ya watu/makampuni yenye nia ya kuwekeza na hivyo kufanya *TIC* kusajili wenye nia ya kuwekeza kufikia 1,282 kwa muda wa miaka mitatu pekee. Kama wenye nia hawa hawa wote wangefanikiwa kuwekeza wangeingiza kiasi cha mitaji cha Dola za Marekani bilioni 15, sawa na shilingi trilioni 36 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kwa miaka 23 toka mwaka 1996 hadi sasa *TIC* iliweza kusajili jumla ya wawekezaji 12,381 ambao wangeweza kuingizia mtaji wa dola bilioni 117 sawa na shilingi trilioni 281. Kama angalau nusu ya wawekezaji hao wangewekeza, wangeweza kuchangia mitaji ya dola bilioni 59, sawa na shilingi trilioni 140 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, hapa naeleweka ninakoelekea, maana yangu ni kwamba wawekezaji wanakuja na dola, hivyo tungekuwa na *dollar reserve* ya kutosha na haya malalamiko ya dola yasingekuwepo; shillingi yetu ingeimarika sana dhidi ya dola na pia *multiplier effects* ya mitaji hii mikubwa ingeonekana kila pahali (sekta) na kuwa na uchumi imara, kwa mfano kila shilingi moja inaongeza shilingi tano kwenye mzunguko wa matumizi *(one shilling creates five shillings spending)* hivyo uwekezaji wa mitaji ya shilingi trilioni 140 ingetengeneza shilingi trilioni 700 kwenye mzunguko wa matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa uoni wangu jitihada hizi kubwa za Mheshimiwa Rais zimekuwa zikikwamishwa na watendaji wasioelewa tafsiri sahihi ya maono ya Mheshimiwa Rais kisha kutafsiri maono hayo kwa vitendo na mara nyingi ni zao la uvivu, uzembe wa kutowajibika.

Mheshimiwa Spika, ubora wa mambo utaonekana kwenye matokeo, mipango yetu ya mwaka, miaka mitano, kumi na kadhalika haioneshi matokeo chanya na tafsiri yake ni kwamba watekelezaji hawaimbi wimbo mmoja na wapangaji.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba mipango imekuwepo muda wote, *either* ikisimamiwa na Wizara ama ikisimamiwa na Tume, hivyo Tume ya Mipango sio jambo jipya kwani kuwa na matarajio mazuri kwa kigezo tu cha kubadilisha utaratibu wa nani asimamie mipango bila kubadilisha *mindsets* zetu huko ni kujidanganya, yatubidi sote wapangaji na watekelezaji tubadilishe mitazamo yetu ya jinsi ya kuwajibika. Kama tabia yetu ya kutofuatilia mipango yetu itaendelea, basi hakuna kitakachobadilika.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa hotuba yake iliyojaa taarifa muhimu zinazotuwezesha kushauri mambo mbalimbali kuhusu Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika ya umma 16 kuunganishwa na manne kufutwa; taarifa kwa vyombo vya habari ya tarehe 15 Disemba, 2023 aliyoitoa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo akieleza kuwa Serikali imeridhia na kuelekeza kuunganishwa kwa mashirika na taasisi 16 na kufuta mashirika na taasisi za umma nne. Maamuzi haya yamerejewa na Waziri katika Hotuba yake ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, ibara ya 29 na 30. 2.1. Changamoto kufuatia uamuzi huu wa Serikali wa kuunganisha na kufuta mashirika na taasisi za umma ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mashirika na Taasisi za Umma yalianzishwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge na hivyo hayawezi kufutwa na tamko la Waziri bila ridhaa ya Bunge. Suala la kuunganisha na kufuta mashirika na taasisi za umma ni la kisera na kisheria na linahitaji mjadala mpana kwa kushirikisha wadau na Bunge. Nimefuatilia taarifa ya Kamati za Bajeti na *PIC* za mwezi

Februari, 2024, suala hili halikujadiliwa na Kamati husika na wala hoja hii haijaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali kuingilia kazi za mhimili wa Bunge na kuharibu mahusiano mema yaliyopo. Bunge linaweza kukataa kufuta au kufanyia marekebisho sheria zilizoanzisha mashirika hayo huku Serikali imeshatangaza hadharani uamuzi wa kuunganisha au kufuta mashirika hayo. Tangazo la Waziri la kufuta na kuunganisha mashirika na taasisi za umma halijaainisha sheria iliyompa mamlaka kutoa tamko hilo na hakuna *GN*. Tangazo la Waziri la kufuta na kuunganisha mashirika hayo liko kwenye mchakato wa awali kwa kuwa Serikali bado ina mchakato unaoendelea katika Wizara husika hivyo hatua hizi hazikuwa zimefikiwa kutangazwa kwenye umma kama ilivyooneshwa katika kipengele cha 5(ii) na (iii) ya tangazo la Waziri. Tangazo hilo la Serikali kwa sehemu kubwa limerudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa mikakati na programu ya mashirika husika, lakini pia imeshusha morali kwa watumishi wa mashirika hayo yaliyotangazwa kufutwa au kuunganishwa kutojua hatma yao.

Mheshimiwa Spika, tatu, tangazo la kufuta au kuunganisha mashirika na taasisi za umma halina maelezo na taarifa muhimu zinazothibitisha uhalali wa maamuzi hayo. Hivyo Waziri, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo alijielekeza vibaya kufikia maamuzi haya katika kipengele cha 4 cha tamko lake kwani badala ya kutangaza kufuta mashirika manne na kuunganisha mashirika ya umma 16 alipaswa kuwasilisha mapendekezo Bungeni kama sheria, kanuni na taratibu zinavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Bunge halifanyii kazi maamuzi ya Serikali bali linajadili na kupitisha mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali. Kwa urahisi wa rejea nanukuu kipengele cha 4 cha tamko la Waziri kama ifuatavyo; "Kufuatia taarifa na mapendekezo ya timu ya wataalam, katika awamu ya kwanza, Serikali imeridhia na kuelekeza kuunganishwa kwa mashirika na taasisi 16 na kufuta mashirika ya umma manne. Natangaza mashirika na taasisi za umma zinazounganishwa na kufutwa ni kama ifuatavyo..." mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika yanayounganishwa au kufutwa, kwa muda mrefu tumekuwa tukiishauri Serikali kuunganisha au kufuta baadhi ya mashirika na taasisi za umma ambazo zina majukumu yanayofanana na kuingiliana kiutendaji, yanayojiendesha kwa hasara na kutegemea ruzuku ya Serikali. Kiujumla sina tatizo na uelekeo huo isipokuwa naukosoa utaratibu uliotumika kufikia maamuzi. Taarifa ya uchambuzi wa timu ya wataalam kuhusu utendaji wa mashirika ya umma inapaswa iwasilishwe kwa Bunge ili kukaribisha majadiliano zaidi kuhusu uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tangazo la Waziri kuna baadhi ya mashirika na taasisi za umma ambazo binafsi naridhia kufutwa au kuunganishwa, lakini zipo baadhi ya taasisi na mashirika ya umma ambazo haziwezi kuunganishwa wala kufutwa kulingana na unyeti wake katika Taifa. Kwa mfano, sioni mbadala wa Taasisi ya Chakula na Lishe *(Tanzania Food and Nutrition Centre-TFNC)* katika kipengele cha 4B(ii) ambapo inapendekezwa kufutwa taasisi hiyo. Vilevile sio mantiki ya kuunganisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Mamlaka ya Uzalishaji wa Mauzo Nje *(EPZA)* kama ilivyooneshwa kwenye kipengele cha 4A(vi) ya Tangazo la Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuunganishwa *EPZA* na *TIC; EPZA* na *TIC* ni taasisi nyeti na zilianzishwa kwa malengo na majukumu tofauti na hivyo itakuwa vigumu kuunganisha mashirika hayo. Malengo mahususi ya *TIC* kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na. 26 ya mwaka 1997 iliyorejewa mwaka 2022, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kimepewa jukumu la kukuza, kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji nchini Tanzania. Kwa kifupi lengo kuu la *TIC* ni kuvutia uwekezaji Tanzania. Malengo mahususi ya *EPZA,* kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, Sura ya 373 malengo ya kisera yaliyotajwa, kazi za *EPZA* kwa mujibu wa Sheria ya *EPZ* na *SEZ* ni kuendeleza, kusimamia na kukuza kanda maalum za kiuchumi pamoja na kanda za uzalishaji kwa mauzo ya nje ya nchi kwa dhana pana ya kuchochea uzalishaji kupitia viwanda hususani vinavyoongeza thamani. Katika kutekeleza azma hiyo *EZPA* hutwaa ardhi na kuweka miundombinu na mahitaji mengine muhimu katika maeneo ya kiuchumi ili kuvutia wawekezaji na kutoa leseni ya

uendelezaji na uendeshaji wa maeneo maalum ya uwekezaji na kanda maalum za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, changamoto za kuunganisha *EPZA* na *TIC* ni pamoja na:-

(i) Kupoteza malengo na mikakati iliyopo ya kila taasisi; itakuwa vigumu kupatanisha na kulinganisha vipaumbele na mikakati ya kufikia malengo ya kisera;

(ii) Kupoteza au kufifisha dira na dhamira ya uwekezaji, maendeleo na ukuzaji wa viwanda nchini;

(iii) Kupoteza imani kwa wawekezaji, uzoefu duniani ni kuwa taasisi hizi ni tofauti na hivyo kuunganishwa kutapelekea kuoanisha na kuunganisha sera, sheria, kanuni na vivutio vya uwekezaji jambo ambalo litaonekana kwa wawekezaji kuwa nchi yetu ina sera zisizotabirika;

(iv) Mgongano wa kimaslahi, kuunganisha *EPZA* na *TIC* kuwa taasisi moja tutapelekea taasisi mpya kutekeleza majukumu yanayokinzana. Mgongano wa kimaslahi utatokea kwa sababu taasisi mpya itatekeleza kazi inayofanywa na *TIC* ya kukuza na kuwezesha na kutumika kama kituo cha kutatua malalamiko ya uwekezaji wakati huo huo ikitekeleza majukumu ya udhibiti *(authority)* wa utoaji wa leseni za *SEZ* na *EPZ* pamoja na kuhakikisha kuwa wawekezaji wanafuata sheria na kanuni za nchi na mamlaka yake; na

(v) Mchakato wa kuziunganisha taasisi hizi utapelekea kuchelewa kutekeleza mambo muhimu yanayozikabili taasisi hizi kwa sasa, hivyo badala ya kukimbilia kuziunganisha taasisi hizi, Serikali iziongezee uwezo hususan mtaji stahiki wa ujenzi wa maeneo maalum ya kiuchumi na mahitaji maalum ya kitaasisi yatakayoboresha taswira ya nchi kiuwekezaji. Nimeshindwa kupata ushahidi wa moja kwa moja kwamba kuunganishwa kwa taasisi hizi mbili kutapunguza gharama za uendeshaji ama kuongeza ufanisi wa utendaji wa mashirika haya na zaidi naona kwamba tunakwenda kubomoa badala ya kujenga.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea Serikali ingeweka nguvu kubwa kutafuta suluhisho la matatizo ya msingi yanayozikabili programu ya *EPZ* na *SEZ* ambalo ni hitaji la rasilimali za kifedha kuwezesha kutwaa ardhi na kuendeleza miundombinu ya *SEZ* kwa madhumuni ya kustawisha ukuaji wa viwanda. Hivi sasa *EPZA* imeshindwa kulipa fidia na kusababisha kuongezeka kwa deni kutokana na riba ya ucheleweshaji wa malipo ya fidia katika kanda maalum za kiuchumi zilizoainishwa na Serikali. Tatizo la mtaji haliwezi kutatuliwa kwa kuunganisha mashirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa muda mrefu pia imeshindwa kutatua changamoto za kisheria zinazokikabili Kituo cha Uwekezaji na Mamlaka ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje na hata baada ya kutolewa mapendekezo ya mpango wa kuboresha mazingira ya biashara nchini *(blueprint),* hivyo changamoto za kisheria zilizopo baina ya taasisi hizi haziwezi kutatuliwa kwa kuunganisha mashirika. Serikali irejee malengo na madhumuni ya kuanzisha taasisi hizi, pia huko nyuma Serikali baada ya kuona ufanisi mdogo kwa taasisi moja kusimamia sheria na programu zaidi ya moja iliamua kuhamisha majukumu ya programu za *EPZ* kutoka Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na *SEZ* kutoka Tume ya Taifa ya Mipango *(NPC)*.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa baadhi ya Nchi nyingine duniani kama China, Malaysia, Kenya, Rwanda, Ethiopia, Ghana, Mauritius, Afrika Kusini na Misri taasisi hizi hazijaunganishwa. Huu ni mfano tu wa mambo ambayo hayako sawa katika tamko la Waziri na ndiyo maana nashauri Serikali ifute tamko lake hili na badala yake ifuate utaratibu wa kuwasilisha Bungeni pendekezo la kuunganisha na kufuta baadhi ya mashirika ya umma ili kupata uwanda mpana wa kupata maoni ya wadau na maamuzi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nilishamtaja Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, halafu Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika mwaka huu wa fedha 2024/2025. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametujalia kukutana siku ya leo kujadili bajeti hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ndiye hasa analifanya Taifa hili kuwa kipaumbele katika uwekezaji na kwa mipango mizuri ambayo inaliletea Taifa uchumi unaokua kwa kasi zaidi. Pia, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa sababu, ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo yote haya yanafanyika kwa umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana vilevile Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais, Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko. Nachukua nafasi hii pia, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Kitila Mkumbo, ambaye kwa kweli anafanya kazi kubwa sana na ndiyo leo tunajadili bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe Spika wetu pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu kwa jinsi ambavyo ameendelea kutuongoza vizuri katika kujadili Bajeti za Serikali na leo hii katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Pia naipongeza Kamati kwa kazi kubwa iliyofanya pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika maeneo mengi kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Maheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapa pole Watanzania wenzangu katika maeneo mbalimbali ambako kumetokea changamoto ya mafuriko kutokana na mvua hii ya *El-Nino*, lakini pia najua kuna changamoto kubwa katika miundombinu. Nachukua nafasi hii pia, kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa vile ambavyo wanaendelea kuniunga mkono na kuhakikisha natimiza wajibu

wangu kama Naibu Waziri katika Wizara ya Viwanda na Biashara katika Serikali hii ya Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua changamoto zilizopo maeneo mengi Tanzania, pamoja na kule jimboni kwangu, zipo barabara nyingi zimeharibika katika kata zote 11. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niishukuru Serikali yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana na kule kwangu kuna fedha ambazo zimeenda kwa ajili ya kutengeneza maeneo haya ambayo yana changamoto ya dharura kwenye miundombinu ya barabara. Sisi kama Wanamufindi Kaskazini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo katika bajeti hii muhimu. Moja ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana ni namna ambavyo Serikali imejipanga kuhakikisha Sekta ya Biashara Ndogo na Viwanda Vidogo *(SMEs)* inapewa kipaumbele katika mipango ya Serikali kwenye uwekezaji na kuwapa vivutio maalum.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinasema kwamba zaidi ya 95% ya biashara zote hapa Tanzania ziko kwenye sekta hii ndogo na ndogo sana. Pia 35% ya *GDP* ya Tanzania inatokana na sekta hii ndogo na ndogo sana na ya kati. Zaidi, katika sekta hii kwa maana ya *SME* zaidi ya 54.3% imeajiri wanawake. Kwa hiyo, maana yake ndio wanaofanya kazi kubwa sana katika mchango huu kwenye pato la Taifa na shughuli nyingi ambazo wanawake wanafanya zinahusisha shughuli za kilimo na uongezaji thamani katika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimesema haya ili tuone umuhimu wake kwamba Serikali tunachukulia sana umuhimu wa *SMEs*, tukianza sisi Wizara ya Viwanda na Biashara tunayo sera mahususi inayoangalia *SMEs*. Kwa sababu ya umuhimu wa sera hii ya mwaka 2003, kwa hiyo tunaenda kuihuisha ili iweze kuchukua uhalisia wa sasa na mahitaji kamili ya *SMEs* kulingana na wakati huu. Pia ndiyo maana *SMEs* iko katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao nao wanaangalia wajasiriamali kwa namna ya pekee ili kuhakikisha

wanafaidika na vivutio vyote ambavyo vinatolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu pia wamechukua sera hii na wanaifanyia kazi na ndiyo maana huko kuna *peer startups* ambayo tunaangalia wale wajasiriamali wadogo (*SMEs* wadogo) wanaoanza biashara basi wanaweza kupewa mitaji na elimu. Katika eneo hili tumeangalia zaidi kwenye *value addition*, kuongeza thamani na hasa mazao yanayotokana na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji tumeona ni lazima tuhakikishe tunaendelea kuweka vipaumbele. Moja, kuendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia *NEDF,* Mfuko huu ambao unasimamiwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Tanzania *(SIDO)*, ambapo huko kuna wajasiriamali wadogo wanaatamiwa *(incubation)* ili waweze kukua katika kujenga viwanda vidogo vidogo lakini pia kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, kupitia Chuo chetu cha Elimu cha Biashara (*CBE),* nako pia kuna uatamizi wa uanzishaji biashara mbalimbali ili kuhakikisha tunawasaidia *SMEs*. Katika maeneo haya Wizara imeweka mpango mahsusi wa kuanza kujenga mitaa ya viwanda *(Industrial Parks)* katika halmashauri. Pia tutaenda mpaka ngazi za kata ili kuhakikisha kunakuwa na maeneo mahususi ya uzalishaji, kwa sababu changamoto mojawapo tuliyonayo kama ambavyo wachangiaji wengine (Wabunge) kwamba tunazalisha bidhaa ambazo sasa tunaenda kushindana katika Eneo Huru la Biashara la Africa *(AfCFTA)*. Maana yake ni lazima tuzalishe bidhaa zenye ubora ili tushindane katika soko hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi kama Wizara kwanza tunaandaa maeneo hayo, lakini pia kujenga majengo ambapo humo tutaweka mitambo mbalimbali. Moja ya mitambo ambayo tunaibuni sasa hivi ni *sugar min plant* kwa maana ya viwanda vidogo vya kuchakata miwa ili kuzalisha sukari kwa ajili ya

matumizi ya ndani, lakini kwa ajili ya kuuza katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na michango kwenye eneo la viwanda vilivyobinafsishwa. Serikali chini ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji imeendelea kuratibu; na sisi kama Wizara ya Viwanda tumeendelea kuhakikisha kwamba viwanda vyote ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa na wale waliouziwa wameshindwa kuviendeleza hatua mbalimbali tayari zinakwenda kuchukuliwa, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, wale ambao walishindwa katika viwanda ambavyo vimerudishwa Serikalini; moja, tumesema tunaendelea kujadiliana nao ili wale ambao wana uwezo au wanataka kuviendeleza na tayari kuna kampuni kama nne ambazo viwanda vyao vimerudishwa Serikali, lakini wamesema wako tayari kuviendeleza, tunajadiliana nao ili tukiingia mikataba waweze kutekeleza kama ambavyo tutakuwa tumekubaliana ili viwanda hivyo vifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaendelea kuwasaidia wale ambao hatujafikia muafaka wa kuvirudisha Serikalini tuwape elimu na ujuzi wa namna ya kuviendeleza viwanda hivyo. Mheshimiwa Ulenge ametoa mfano Kiwanda cha Unga wa Ngano cha Pembe pale Tanga, ni moja kati ya viwanda ambavyo tunashauriana na wawekezaji. Moja, kuwapa namna ya kuendeleza biashara zao, lakini pia kama kuna changamoto ya mitaji Serikali iweze kuona namna ya kuwasaidia ili waendelee kuzalisha ili viwanda hivi vyote viweze kufanya kazi kama ambavyo vilikuwa vimekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na maeneo mengi ya namna gani tunaendelea kusaidia wawekezaji wa ndani ili waweze kufanya vizuri na kusiwe na ile hisia kwamba tunapendelea au tunatoa vivutio kwa wawekezaji wa nje. Moja, katika Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha, imeangalia viwango ambavyo mwekezaji wa ndani akikidhi anapata vivutio na hii tulipunguza mtaji kutoka Dola za Kimarekani 100,000 mpaka 50,000. Hii ina maana sasa Mtanzania

anaweza kuwekeza kwa mtaji huo na akapata vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi ili aendelee kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, pili, pia tunaendelea kutekeleza mpango ule wa MKUMBI *(Blueprint)* ambao nao umetekeleza mambo mengi ikiwemo kuondoa tozo na kodi kero ambazo wafanyabiashara wengi na wawekezaji walikuwa wanakumbana nazo. Kwa hiyo, tunaendelea kuboresha hilo.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango Mkakati wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, tumeshaanza kuweka lile dirisha la pamoja la kuhudumia wawekezaji ili kurahisisha kupunguza ule ukiritimba au urasimu usio wa lazima kwa wawekezaji; kuhakikisha kwamba wanapata huduma kwa haraka katika sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, taarifa tu, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, jumla ya miradi 295 kati ya miradi hiyo 509 yote ilisajiliwa na Kituo chetu cha Uwekezaji na miradi hii inamilikiwa na Watanzania. Kwa hiyo, utaona kwamba Watanzania tayari wanafaidika na vivutio hivi ambavyo Serikali inavitoa kwa wawekezaji bila kuangalia kwamba ni wa ndani au wa nje ambao ni zaidi ya 58% ya Watanzania ambao wamesajiliwa katika miradi hii.

Mheshimiwa Spika, usajili wa miradi katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika Mamlaka yetu ya Uwekezaji kwa ajili ya kuzalisha kwa mauzo nje; *EPZA* imeweza kusajili jumla ya miradi ya viwanda 25. Aidha, jumla ya miradi 206 ambayo imesajiliwa kupitia *EPZA* tangu mwaka 2006 ilipoanzishwa miradi hii imelenga zaidi katika viwanda vya kuongeza thamani na hasa kwenye sekta ya pamba, nguo na mavazi, lakini pia kwenye kuchenjua madini.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi 509 iliyosajiliwa na *TIC* sekta zilizoongoza kwa usajili wa miradi hiyo ni uzalishaji wa miradi viwandani kwa maana ya miradi 221 ambayo ni sawa na 43% ambayo inatarajiwa kuzalisha zaidi ya ajira 28,445 na wameweza kuwekeza zaidi ya mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 1,501. Kwa hiyo, hii ni mikakati ambayo inatekelezwa kwa uratibu wa Ofisi ya

Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Wizara ya Viwanda na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuchangia katika maeneo machache ambayo pia yaliongelewa kuhusiana na miradi ya kimkakati, imeongelewa kuhusiana na Mradi wa Magadi Soda Engaruka pia Mradi wa ule wa Liganga na Mchuchuma. Serikali inafanya jitihada za makusudi na hasa Awamu hii ya Sita kuhakikisha miradi hii ya kimkakati na kihistoria inaenda kukwamuka na ndiyo maana tayari fidia imeshaanza kulipwa katika maeneo haya. Tukianza kule Liganga na Mchuchuma lakini baadaye sasa tunaenda kulipa fidia katika eneo la Magadi Soda ili miradi hii yote iweze kutekelezwa kadri ambavyo Watanzania wengi wangependa.

Mheshimiwa Spika, kuliongelewa kuhusiana na Sekta ya Madini hasa kwenye chumvi na Mheshimiwa Dkt. Chaya pale Manyoni Mashariki; tunalifanyia kazi na Serikali imeshasema makusudi, chumvi ni bidhaa muhimu. Kwa hiyo, tutaangalia maeneo yote ambayo yana uzalishaji wa chumvi ili tuhakikishe chumvi hiyo inazalishwa hapa Tanzania, tutumie sisi Watanzania pia tuweze kuuza nje ya nchi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tutahakikisha miradi ya kimkakati kwenye bidhaa muhimu ambazo kama Watanzania lakini pia soko linahitaji tutazalisha kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme naunga mkono hoja bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa jinsi ambavyo umeendesha mjadala huu vizuri kama kawaida yako. Nimshukuru sana Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe kwa kunipa *company* kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Kigahe tumefanya naye kazi kwa muda

mrefu, ni Naibu Waziri mahiri, ni Mbunge mahiri sana na nitumie nafasi hii kwa kweli kuwaambia wananchi wa Mufindi Kaskazini wanalo jembe walishikilie vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuendelea kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa uchambuzi wao na taarifa yao makini ambayo ilisomwa hapa na mwanamama mahiri sana, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum. Tunawashukuru sana kwa kuunga mkono hoja na wametoa hoja nyingi, naomba nijibu mbili tu kwa upande wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la Dira ya Maendeleo; walishauri kwamba izingatie mabadiliko yanayoendelea duniani, lakini pia mfumo wa kiutawala. Tumepokea ushauri huo na tutauzingatia. Sasa hivi zoezi ambalo linaendelea katika upande wa dira ni zoezi la kukusanya maoni, kwa hivyo haya maoni ambayo yanatolewa na Kamati na mengine yatazingatiwa na timu ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile ilishauri na kusisitiza kwamba Serikali ihimize matumizi ya Mfumo wa Miradi *(National Project Management Information System)*. Niseme tu kwamba kwa mujibu wa Waraka Na.5 wa Hazina umesisitiza kwamba miradi yote ya Kitaifa lazima ipitie katika mfumo huu na isipopitia katika mfumo huu Tume ya Mipango haiwezi kuifikiria. Kwa hiyo, niwakumbushe watekelezaji wa miradi yote wakumbuke kuingiza miradi yote kupitia mfumo huu kwa sababu ndiyo utaratibu ambao tumekubaliana na ni utaratibu wa kisheria ambao pia umeidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu nipitie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, tumepata michango ya Waheshimiwa Wabunge 17 ambao wamezungumza moja kwa moja na Mheshimiwa Mbunge mmoja amechangia kwa njia ya maandishi. Niseme tu kwamba sisi kama Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji tumewasikia Waheshimiwa Wabunge na tutazingatia maoni na ushauri wao ambao kimsingi ni ushauri wa Watanzania kupitia sauti zao.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yamechangiwa ni matatu makubwa. Tunalo eneo la jumla la mipango, tunalo eneo la uwekezaji na uendeshaji wa mashirika ya umma. Nitataka nigusie baadhi ya maeneo haya kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa upande wa mipango hoja zimetolewa nyingi, lakini ni hoja tano. Hoja ya kwanza; mkakati wa kuandaa rasilimali watu ni muhimu sana uzingatie mahitaji yetu na Mheshimiwa Rashid Shangazi alitoa mfano, kwamba vyuo vingi kwa sasa vinatoa mafunzo ya ualimu wakati walimu wamejaa mtaani bila kazi. Ni hoja ya msingi na ndio maana katika mpango niliowasilisha moja ya jukumu na kipaumbele cha Tume ya Mipango kwa mwaka huu unaokuja ni kufanya tathmini ya rasilimali watu ili kubaini mahitaji halisi ya rasilimali watu na ujuzi unaohitajika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, hilo ni jambo la msingi sana kwa sababu tunapoenda mbele suala la rasilimali watu ni suala ambalo lipo katikati ya mipango. Bila kuwa na rasilimali watu ambayo imepangwa vizuri na ujuzi unaoeleweka na unaohitajika mipango yetu haiwezi kufanikiwa. Kwa hiyo, ukisoma majukumu 20 ya Tume ya Mipango jukumu lao la kwanza ni kufanya tathmini ya rasilimali ikiwemo rasilimali watu na mwaka huu ujao wa fedha hilo jukumu watalifanya ili tupate picha halisi ya mahitaji yetu na hili litazingatiwa vizuri sana katika Dira yetu ya Maendeleo ambayo inakuja. Kwa hiyo, hilo tumelichukua hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni maendeleo vijijini, hili Waheshimiwa Wabunge wamelitolea maoni. Kwa mujibu wa taarifa ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 takwimu muhimu sana zipo nyingi, lakini takwimu mbili za kuzingatia; moja, 65% kama alivyosema Mheshimiwa Kamani, ya Watanzania wanaishi vijijini. Kwa hivyo, huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi hii bila kuwa na *focus* katika maendeleo vijijini kwa sababu ndiko Watanzania walio wengi wako huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu ya pili ni ile aliyoisema Mheshimiwa Ngw'asi kwamba 76% ya Watanzania wapo chini ya umri wa miaka 35 na kuna mtu mmoja hapa amesema, mimi ni

kijana. Nilishapita siku nyingi huko, mimi kwa sasa sipo kwenye ujana, sisi ni wazee wa nchi hii. Kwa hivyo, 76% wapo chini ya miaka 35 na ukienda zaidi 42.8% wapo chini ya miaka 15. Tunasema nini? Tunasema kwamba kimsingi idadi kubwa ya watu wa nchi hii ni watoto na vijana. Kwa hiyo, huwezi kuzungumzia maendeleo yoyote ya maana bila kugusa makundi hayo mawili. Moja, vijijini na pili, vijana na watoto. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mipango yetu iliyopo na mipango ijayo ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Taifa tutazingatia sana makundi haya ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu unapokua uwe ni uchumi jumuishi, ulenge maeneo ambayo watu wengi wapo. Ndiyo maana kwa kuzingatia hilo, Mheshimiwa Rais ameipa kipaumbele sekta ya kilimo kwa sababu ndiyo ambayo inaajiri watu wengi zaidi ya 65%. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kusisitiza na kuwekeza sana katika maeneo ambayo yanagusa watu wetu wengi ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na kadhalika. Pia tuendelee kusisitiza kwamba lazima tu-*pay attention* ya kipekee kwa watoto na vijana kwa sababu ndiyo usalama wa Taifa kwa sasa na miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri kwamba kuna haja ya kuanzisha taasisi maalum inayoshughulikia maendeleo vijijini. Ni wazo zuri, lakini niseme tu kwamba tayari tuna taasisi ambazo zipo *dedicated* kwa maendeleo vijijini. Kwa mfano *REA*, *REA* ni taasisi maalum kwa ajili ya maendeleo ya nishati kwa maana ya umeme vijijini na inafanya kazi nzuri na ndiyo maana tangu ianzishwe tunazungumzia hapa karibu 90% ya vijiji vinaunganishwa kwenye umeme.

Mheshimiwa Spika, tunayo *TARURA* ambayo imekabidhiwa jukumu la kushughulikia barabara za vijijini, tunayo *RUWASA* ambayo Bunge hili mwaka 2018 ilitunga Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Maji Vijijini *(RUWASA)*, tangu ianzishwe Sekta ya Maji Vijijini inakwenda kwa kasi, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tayari tuna mfumo wa kitaasisi kwa lengo la kushughulikia baadhi ya maeneo kwa maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ina-*pay attention* kubwa sana kwenye maendeleo vijijini kupitia sekta mbalimbali, ndiyo maana tunatoa ruzuku ya mbolea vijijini ili wakulima wetu waweze kulima bila vikwazo vikubwa. Kwa hiyo, hili ni eneo kubwa ambalo tumeliangalia.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia umuhimu wa kufungamanisha sekta za maendeleo, wametoa mfano wa matumizi ya rasilimali za maji kwamba mradi wa *Lake Victoria* kwa mfano, haiwezekani mradi mkubwa kama ule ukaishia kuwa tu mradi wa maji ya kunywa, haiwezekani! Sisi kama Serikali Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo na tumekubaliana kuwa Mradi wa Maji unaotoka *Lake Victoria* kuja Dodoma, lazima ndani yake uwe na *dedicated lines* kwa ajili ya umwagiliaji ili Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma, ambako mradi huu utapita wananchi wasipate maji ya kunywa tu, bali lakini watumie maji hayo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais na mradi umeshapitishwa, tayari watalaam wanaendelea na upembuzi yakinifu na naamini Mheshimiwa Waziri wa Maji wakati wa bajeti yake ataueleza kwa kina.

Mheshimiwa Spika, tumeshakubaliana tulipoanzisha *National Water Grid* (Gridi ya Maji ya Taifa), lengo ni kutumia rasilimali za maji kubwa kwa maana ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, maji haya ambayo Mungu ametujalia, tuyatumie kwa lengo la uzalishaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo kilimo. Kwa hiyo, hili ndilo lengo kubwa ambalo tunakwenda nalo, Waheshimiwa Wabunge maoni yenu yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, mawazo yake mazuri yamezingatiwa, kama alivyosema *mate* wangu, haya mawazo yake mazuri yamezingatiwa na litafanyiwa kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, suala la nne lilikuwa ni suala la mipango ya Kitaifa *vis-a-vis* mipango ya kisekta. Mheshimiwa Kunambi aliongea vizuri kwamba ni lazima tuwe na dira moja, akaeleza kwamba tuna dira nyingi za kisekta, dira ya kitaifa. Kimsingi kwa jina lolote ambalo utaita na wala sihitaji kuwa na wivu unaogawanyika kwa sababu Serikali inafanya kazi kama kitu kimoja, Dira ya Taifa ni moja na mipango yote ya Taifa, sera zote za kisekta lazima ziakisi Dira ya Taifa ya Maendeleo na ndivyo itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, hii dira ambayo tunaiandaa hatimaye sera zote na hivyo ambavyo Mheshimiwa Kunambi ameviita vi-*vision* vidogo vidogo itabidi lazima viakisi Dira ya Taifa ya Maendeleo, hili halina shaka kwa sababu hatimaye Dira ya Taifa ya Maendeleo inasimamiwa na Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango kwa muundo wake Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndivyo sheria inavyosema na anao wajumbe wengine wanne pia Mawaziri wanaohusika na Mipango na Fedha ni wajumbe. Kwa hivyo, hii ni Tume kubwa na jambo likitoka pale huwa limepikwa vya kutosha, kwa hiyo msiwe na wasiwasi kwamba kutakuwa na mkanganyiko wa mipango ya kitaifa na mipango ya kisekta. Haiwezekani kwa sababu mipango ya kitaifa inaanzia kwenye mipango ya kisekta ndiyo inafika juu. Ndiyo maana hapa sekta zitawasilisha mipango yake yote na nitakuja kusoma Mpango wa Taifa tarehe 13 Juni, ambao utaunganisha mipango yote hiyo ili kupata mpango wa Kitaifa. Kwa hiyo, hapawezi kuwa na mgongano wa mipango ya kisekta na mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano nimeshalisema, Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza na Mheshimiwa Charles Kimei ameongea vizuri kwamba mfumo wa ufuatiliaji wa miradi ya kitaifa, ni muhimu sana tuwe na mfumo. Mheshimiwa Mbunge mfumo upo, tunao na unafanya kazi unaitwa *National Project Management Information System (NPMIS)* na kwamba sekta zote ambazo zinatekeleza miradi ni lazima zizingatie mfumo huu. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni eneo la kwanza la mipango.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni uwekezaji. Hapa Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni mengi katika maeneo matano. Kwanza, ni juu ya Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma. Waheshimiwa Wabunge, waliochangia akiwemo Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya *PIC* wamesema, Muswada huu uje na ameainisha maeneo pale.

Mheshimiwa Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Muswada huu ulishasomwa kwa mara ya kwanza, baada ya kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, Serikali iliona kuna maeneo ambayo inahitaji kuyafanyia kazi zaidi na tumeshayafanyia kazi, taratibu zinaendelea kukamilika ili tuweze kumwomba Spika aruhusu ule Muswada usomwe kwa mara ya pili. Niwahakikishie kwamba, Muswada huu bado upo na Serikali haijauondoa.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili lilikuwa ni suala la fursa za uwekezaji hususani uwekezaji kwa wazawa na hasa wawekezaji wadogo. Nitoe tu taarifa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, mwaka huu tuliwaagiza *TIC* na hata nilipoteuliwa mwaka jana, moja ya swali langu kubwa kwa Kituo cha Uwekezaji Nchini *(TIC)* ilikuwa ni kwamba, huko nje *TIC* inaonekana ni chombo cha wawekezaji kutoka nje, lazima mbadilishe *mindset* ili hiki chombo kionekane kwamba ni chombo cha wawekezaji wa Tanzania *primarily* na watu wa nje *secondarily*.

Mheshimiwa Spika, wamefanya hivyo tukaanzisha kampeni kubwa ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani, vijana hawa wa *TIC* wamefanya kazi nzuri wamezunguka nchi nzima kuhamasisha jambo hili, kwa kweli niseme Watanzania wengi ambao wamefikiwa wamefurahi sana.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna mwekezaji mmoja pale Geita ana hoteli kadhaa, alikuwa hajui faida za kujiunga na *TIC* kusajili mradi wake, tangu asajili anafurahia sana na amekuwa ni *ambassador* mkubwa sana wa *TIC*. Kwa hivyo, tutaendelea kuwasukuma vijana hawa wa *TIC* ili kuhakikisha kwamba wanawafikia Watanzania popote walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika hilo, *TIC* wameanzisha utaratibu mzuri kwamba, kama una eneo, una ardhi yako wanakuunganisha na wawekezaji, kwa sababu kuna Watanzania wengi ambao wana ardhi wamekaa nazo, wangeweza kutengeneza pesa. Kwa hivyo *TIC* wameanzisha utaratibu mzuri sana kama una ardhi yako unawataarifu *TIC* na wanakuunganisha na wawekezaji, kisha unaingia ubia na wawekezaji wa nje, wewe una ardhi unapata mtaji na unaanza kutengeneza fedha.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania wenye ardhi tafadhali wawasilishe ardhi zao kwa *TIC*, watawaunganisha na wawekezaji mbalimbali ili hiyo ardhi ibadilike kuwa mali waanze kutengeneza fedha na kujenga uchumi wao na uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni suala la miundombinu. Tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na tutayazingatia. Katika kuzunguka kwangu kote na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria walijionea tulipozunguka pamoja, changamoto kubwa sana kwa upande wa uwekezaji hasa kwenye viwanda ilikuwa ni suala la nishati, umeme ulikuwa hautoshi, tunashukuru kwa usimamizi mzuri na uongozi wa Mheshimiwa Rais na Waziri wetu wa Nishati ambaye ni Naibu Waziri Mkuu, hatimaye Mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere umekamilika na umeanza kuzalisha umeme. Kwa hivyo, hii changamoto ya umeme kwa viwanda inaenda kuwa historia na kwa miradi ya umeme ambayo ipo kama ambavyo Waziri wa Nishati ataeleza kwenye hotuba yake, changamoto ya nishati kwa viwanda inaenda kuisha na wawekezaji wengi watakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la maji viwanda vingi kwa kweli wanashukuru kwamba wanapata maji na kuna mfumo mzuri sana wa kuunganisha kwenye maji na suala la miundombinu linaendelea kufanyiwa kazi, hayo yote tumeyapokea.

Mheshimiwa Spika, suala la nne, ilikuwa ni vivutio. Ni kweli tulikuwa na changamoto ya vivutio kwa wawekezaji wanaoitwa wawekezaji wa kimkakati. Wapo wawekezaji 16 ambao walikuwa

wameomba vivutio 60 tangu mwaka 2018. Walikuwa wamekwama kwa sababu kulikuwa na mgongano kati ya Sheria yetu ya Uwekezaji na Sheria mbalimbali za Kodi. Sheria ya Uwekezaji inatoa unafuu wa hivyo vivutio, lakini Sheria za Kodi zilikuwa zimekwama.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako, Bunge limefanya marekebisho kadhaa kwenye Sheria yenyewe ya Uwekezaji na kwenye Sheria Mbalimbali za Kodi, tangu mwaka 2022 sasa kupitia *NISC (National Investment Steering Committee)* ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, vivutio vimeshaanza kutoka. Kati ya vivutio 64 ambavyo vilikuwa vimekwama vivutio 58 vimeshatoka vimebaki sita peke yake na hivi vipo katika taratibu mbalimbali za kupewa *GN* ili vitoke. Kwa hiyo, hii changamoto nayo inashughulikiwa na tunaamini kwamba inaenda kuisha.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho katika hili ilikuwa ni Mradi wa Bagamoyo. Mheshimiwa Muharami Mkenge ameongea kwa uchungu katika eneo hili anafahamu tulishafika, nawataarifu wananchi wa Jimbo la Bagamoyo kwamba, kwanza Mbunge wenu katika jambo ambalo halali nalo ni suala hili la Mradi wa Bagamoyo, anawapigania wananchi wake wapate fidia na pili, wapate maeneo yao ili waweze kuwekeza. Kwa hivyo wananchi wa Bagamoyo wana Mbunge imara sana ambaye kwa kweli analipigania sana suala hili na hoja zake zote tutazizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwishakamilisha mpango kabambe wa mradi huu na utaidhinishwa. Mradi huu una maeneo mawili ambayo ni ujenzi wa bandari kubwa na ujenzi wa viwanda. Mradi mzima utagharimu takribani shilingi trilioni 11, ni mradi mkubwa wa kitaifa, ni moja ya miradi 17 ya kielelezo na haki zote za wananchi wa Bagamoyo zitazingatiwa kikamilifu ikiwemo kulipwa fidia zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge suala hili asiwe na shaka nalo, mimi nimeshafika pale, anafahamu tulikuwa pamoja na wananchi wake, niwahakikishie kwamba, anawapigania vizuri na Serikali yao sikivu ya Chama Cha Mapinduzi imesikia kilio chako na itakizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu na la mwisho ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelitolea maoni ni eneo la mashirika ya umma. Hoja kubwa hapa ni mbili. Hoja ya kwanza inahusu kufutwa na kuunganishwa kwa mashirika ya umma. Tumepokea maoni ya Mheshimiwa Luhaga Mpina, ameandika vizuri na ametoa hoja za msingi ambazo Serikali tutazifanyia kazi na nyingine nitazijibu hapa.

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa ni mbili, kwanza, vigezo ambavyo vinazingatiwa katika kuunganisha ama kufuta mashirika haya ya umma. Msingi mkubwa wa uamuzi huu ambao Mheshimiwa Rais aliueleza hapa Bungeni na katika hotuba zake mbalimbali na hatimaye akatupatia maelekezo wasaidizi wake, moja ni kuipunguzia Serikali mzigo.

Mheshimiwa Spika, mashirika haya ya umma yanakusanya takribani shilingi trilioni 1.07, lakini mashirikika haya ya umma ukifanya hesabu yanakula fedha za Serikali ikiwemo mishahara na matumizi mengine takribani trilioni tatu. Kwa hiyo, katika hali ya kawaida na kwa kiongozi yeyote makini ni lazima hili eneo aliangalie. Ni lazima alifanyiwe *reform* ili hatimaye mashirika haya mosi, yaendeshwe kwa ufanisi na pili yachangie kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima tufanye tathmini na mapitio ya mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Wataalamu ya Kitaifa ikihusisha sekta mbalimbali walifanya utafiti na uchambuzi mpana na hatimaye wakabainisha kuwa mashirika 16 ambayo ilikuwa ni muhimu yaunganishwe na mashirika manne yafutwe. Mchakato huu unaendelea, tutafanya uchambuzi wa mashirika yaliyobaki na tutaendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunazingatia mambo gani? Moja, tunaangalia yale mashirika ambayo majukumu yao yanaingiliana, yanaunganishwa. Yale mashirika ambayo majukumu yao yamepitwa na wakati, kwa sababu tusisahau kwamba mashirika mengi haya yalianzishwa kipindi ambacho tulikuwa na *state-based economy* na sasa baadhi ya majukumu hayo

yamechukuliwa na *private sector*. Katika mazingira hayo, majukumu hayo yamepitwa na wakati, yatafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia yako mashirika ambayo majukumu yao yanashabihiana sana na yenyewe yataunganishwa. Kwa hiyo, huo ndiyo msingi ambao tunazingatia.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge amehoji ni kwamba, ilipaswa mchakato huu uje Bungeni na Bunge ndilo litoe uamuzi huu. Hata hivyo, kwanza tumezingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ukisoma Ibara ya 37 ile Sehemu ya Nane, tumezingatia Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370, Sheria ya Msajili wa Hazina, pia tumezingatia Sheria iliyounda makampuni ya umma. Yote hii inaeleza mamlaka ya kufuta na kuanzisha shirika la umma yako wapi. Mamlaka haya yako wazi na yametajwa katika sheria mbalimbali. Kwa hiyo nimhakikishie Mbunge kwamba, mchakato huu umezingatia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na umezingatia kikamilifu sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo limezungumziwa hapa ni kwamba mchakato huu unaua *morale* ya wafanyakazi, sasa wafanyakazi wako *demoralized*. Kwanza, *of course* hoja yenyewe haina ushahidi wa kisayansi, hakuna utafiti ambao umeshafanyika ukaonesha kwamba, kuna wafanyakazi ambao *morale* imekufa, lakini nimhakikishie Mbunge kwamba, wafanyakazi wote wa mashirika ambayo yameunganishwa na kufutwa wameshirikishwa kikamilifu, lakini wamepewa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, mosi, hakuna mfanyakazi ambaye atapoteza kazi, kwa sababu mashirika haya hayafutwi au kuunganishwa kwa sababu ya ubovu wa wafanyakazi, hapana! Ni majukumu tu, hivyo wafanyakazi wote katika mashirika ambayo yanaunganishwa na yanayofutwa wapo salama kikazi na watafanya kazi katika taasisi za umma. Usisahau kwamba tayari kuna maeneo mengi ya utumishi wa umma ambayo yana upungufu wa watumishi, hivyo, zoezi hili litatupatia nafasi ya kupata watumishi wengine ambao watapelekwa katika maeneo

mengine ya kazi. Kwa hiyo, suala la *morale* kwa watumishi wa umma halipo.

Mwisho, mchakato ambao tumeanza nao ni mchakato wa ndani ya Serikali hatimaye sheria husika zitabadilishwa au kuandikwa upya na Bunge hili litahusika. Pale ambapo mabadiliko ya kisheria yatahitajika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litahusika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema mambo makubwa matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, katika utekelezaji wa mambo yetu tunazo nyenzo nne kubwa ambazo ni lazima tuendelee kuzishikilia:-

(i) Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo imetafsiriwa katika mipango yetu ya maendeleo na kwa sasa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

(ii) Chombo chetu cha utekelezaji ni Serikali. Serikali imara inahitaji chama imara cha siasa. Chama Cha Mapinduzi ambacho ndicho kimeunda Serikali hii, kipo imara sana kuliko wakati mwingine wowote. *(Makofi)*

(iii) Tunahitaji nahodha imara. Hakuna shaka juu ya unyenyekevu, ushupavu, uzalendo, weledi na uchapakazi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

(iv) Tunahitaji Bunge imara ambalo linaakisi sauti na hisia za wananchi. Sina shaka na uimara wa Bunge lako, sina shaka na umahiri wa Wabunge wako. Chini ya uongozi wako makini sana, tuna imani kubwa kuwa kwa ushirikiano wa Bunge lako Tukufu, mipango yetu itaendelea kuwa thabiti, endelevu na kwamba fursa za uwekezaji zitaendelea kupanuka na kuimarika kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia juu ya umuhimu wa nahodha na kwamba tunaye nahodha imara sana na amethibitisha hivyo. Uhodari wa nahodha wa meli haupimwi katika maji yaliyotulia, uhodari wa nahodha wa meli hupimwa wakati wa mawimbi makali baharini. Tangu aingie madarakani Mheshimiwa Rais wetu ameshavuka vikwazo vingi na kumudu kuivusha meli katikati ya mawimbi makali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimtie moyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba yupo katika mstari sahihi na sisi wasaidizi wake na naamini Bunge lote hili tupo naye pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna wajibu kama Bunge na kama Watanzania katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza wajibu wetu katika kuhakikisha kuwa nahodha wetu anatuvusha salama. Nahodha wetu akitikiswa sote tutatikisika. Katika kijitabu chake cha Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania, Baba wa Baifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliandika, "Huwezi kumtikisa Rais na nchi ikawa salama." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusikubali Taasisi ya Urais kutikiswa kwa sababu tukiruhusu hilo tutakuwa tumeruhusu kutikiswa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kutoa hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Baada ya kusema hayo na hoja yetu kuungwa mkono sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Division*.................................................Sh. 3,428,529,700

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Nina jina hapa mbele la Mbunge ambaye angetaka ufafanuzi juu ya jambo ambalo kanuni zetu zinaruhusu kwenye Mshahara wa Waziri jambo ambalo linaweza kuombewa ufafanuzi, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Katika mchango wangu niliochangia kwa maandishi ambao na Mheshimiwa Waziri ameurejea hapa ni kweli nilihoji kwamba taasisi 16 ambazo zinaunganishwa na nne zinafutwa. Maamuzi haya ameyarejea pia kwenye Hotuba yake Ibara ya 29 na ya 30 lakini na Kamati nayo pia katika Ibara ya 2(4)(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya hapa ni moja; Waziri amefuta na ameunganisha Mashirika wakati mchakato bado unaendelea. Kwa hiyo hawezi akafuta mashirika halafu tena akasema kuna mchakato bado unaendelea. Pili, mashirika haya ya umma yalianzishwa na Bunge hili kwa sababu zilizokuwepo ambazo ni muhimu. Hayawezi kufutwa nje ya Bunge hili bila kuelezwa sababu hizo muhimu zilizopelekea kufutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ukifanya maamuzi ya kuyafuta Mashirika haya halafu baadaye ndiyo ukaleta sheria hapa Bungeni, Bunge hili liridhie kufutwa kwa Mashirika hayo kupitia Sheria zilizoanzisha Mashirika hayo; kama Bunge likikataa maamuzi yako hayo ya kubadilisha Sheria na wewe tayari umeshautangazia umma kwamba mashirika hayo umeyafuta au umeyaunganisha halafu Bunge likaja kukataa? Kwa hiyo naona kabisa kwamba ni Serikali kuingilia mamlaka ya Mhimili wa Bunge kwa sababu haikupaswa kufanywa hivyo. Ilipaswa ianze mchakato mwanzo halafu sasa ije ihitimishie na kufuta au kuunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ninayoiona hapa ndiyo hiyo ambayo nimemaliza kuitaja kwamba huku Waziri anatueleza kwamba Wizara zile bado zina mchakato sasa wa kuanza kufuta hayo Mashirika na kuyaunganisha kwa mujibu wa sheria. Sasa kama ilikuwa ni *mature* kiasi hicho yeye hilo tangazo alilolileta kwa umma lilikuwa linahusu nini huku akijua kwamba Mawaziri wa Kisekta wanaohusika na hayo mashirika bado hata hawajahitimisha na pengine yawezekana hata wao wakampinga maamuzi yake? Kwa mfano huwezi ukafuta Shirika la *EPZA* ukaunganisha na *TIC*. Sasa haya yote lazima tuambiwe kwa kina kama Bunge tufikie maamuzi ya kufuta kwa pamoja yasifanywe na Waziri.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu sahihi nitaondoka na mshahara wa Waziri na sitaurudisha. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 122 haitakuruhusu kuondoka na Mshahara wa Waziri, lakini utaweza kuondoka na shilingi moja. Waheshimiwa Wabunge hili tuliweke sawa isije ikaonekana kwamba ametoa hoja nyingi kwenye jambo ambalo kanuni inataka jambo moja mahususi. Sasa yeye aliita mambo lakini ukimsikiliza unagundua ni mifano ya hoja moja tu ya kufuta mashirika ya umma. Kwa hiyo nimeona nilifafanue hilo,

Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika hoja yake Mheshimiwa Luhaga Mpina amekubaliana na uamuzi wa Serikali kimsingi. Naomba nimnukuu, anasema hivi ukurasa wa tatu wa hoja yake, "kwa muda mrefu tumekuwa tukishauri Serikali kuunganisha au kufuta baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma ambazo zina majukumu yanayofanana na kuingiliana kiutendaji, yanayojiendesha kwa hasara na kutegemea ruzuku ya Serikali, kiujumla sina tatizo na uelekeo huo wa Serikali." Kwa hiyo *basically* kwenye hoja yake ameunga mkono uamuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja yake ya pili…

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja, kwa nafasi hii humjibu mchango aliochangia, kwenye ngazi hii unajibu hoja yake aliyoileta wakati wa kushika mshahara hapa. Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hiyo hoja yake kwamba tumefuta nje ya utaratibu, kama nilivyosema tumezingatia sheria. Pili, kufuta haya mashirika na kuunganisha ni mchakato. Kwa hiyo tangazo ambalo nililitoa kwa niaba ya Serikali tulizielekeza mamlaka husika zianze mchakato wa kuunganisha na kufuta Mashirika haya kwa kuzingatia Sheria ambazo zimeanzisha Mashirika haya. Kwa hiyo ni mchakato ambao unaendelea ndiyo maana kama ni *TIC* ipo na ndiyo maana tumetambulisha watu wa *TIC* na *EPZA*. Moja ya Mashirika ambayo yanaunganishwa ni *TIC* na *EPZA,* bado zinaendelea kufanya kazi mpaka pale mchakato wa kisheria utakapokamilika. Kwa hiyo ni tangazo la kufuta kwa kuzingatia mchakato wa kisheria kwa kuzingatia sheria ambazo mashirika haya yameundwa nazo.

**MWENYEKITI:** Kwa hivyo mashirika hayajafutwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika hayajafutwa ila Serikali imetangaza mchakato wa kuyafuta kwa kuzingatia sheria ambazo zimeundwa. Yatafutwa pale ambapo sheria husika zitakuwa zimebadilishwa ama kuwekwa vinginevyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aeleze ukweli. Ukisoma Ibara ya 2(4)(1) ya Kamati inayomsimamia inasema wazi kwamba Wizara hii imefanikiwa kufuta Mashirika matatu na kuunganisha mashirika 16. Kwa hiyo aseme ukweli kama anarekebisha tangazo lake na mantiki ya tangazo lake kwenye umma lilikuwa ni nini kama Serikali bado ina mchakato alitangaza kufanikisha nini? Kama nilivyosema kwamba leo hii watumishi umewaambia kwamba Shirika lao linafutwa halafu unasema *morale* ya kazi itakuwepo? Shirika kufutwa inategemea aidha utahama au utapelekwa Wizara gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, kwenye ngazi hii hutoi tena maelezo mengi ya kiasi hicho. Wewe kama umeridhika na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri unasema umeridhika unakaa, hukuridhika tunasonga kikanuni kabisa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mwongozo wako na sasa niwaombe sana Wabunge wenzangu waniunge mkono hili jambo tulijadili ili mwisho wa siku mimi niondoke na huu mshahara wa Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ili niweze kuondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya hoja yako haijaungwa mkono. *(Makofi)*

Haya Waheshimiwa Wabunge, wewe umesimama baadaye, hata hivyo uko peke yako, kwa hivyo hoja haijaungwa mkono.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Mpina, mimi mwenyewe nataka kushika shilingi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana, sasa ngoja hilo la kwako la baadaye kidogo. Mheshimiwa Mpina hoja yako imeshafungwa

hakuna Mbunge amekuunga mkono, kwa hivyo tunaishia hapo tunasonga mbele.

*(Hapa Mhe. Luhaga Mpina alisimama kutaka kupata nafasi ya kuendelea kutoa ufafanuzi wa hoja yake)*

**MWENYEKITI:** Umeshatoa si ulipewa nafasi ukakaa? Sasa hatuendi namna hivyo wewe umepewa nafasi ya kutoa hoja na ukasema Wabunge wenzangu waniunge mkono, ukakaa, hakuna Mbunge aliyesimama ndiyo hujaungwa mkono. Ndiyo utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Mpina hiyo lakini Mheshimiwa Waziri katika ule uhalisia maelezo ya Kamati namna yalivyoandikwa hapa na ufafanuzi ambao wewe umeutoa hapa labda niseme hata mimi nilipoliona tangazo niliamini kwamba mko katika kupima shirika lipi litafutwa, shirika lipi litaungana na lipi. Kwa sababu hoja ya kufuta kama shirika lilianzishwa na sheria haliwezi kufutwa kwa mchakato nje ya hapa na ndiyo maana hata Tume ya Mipango tulikuja hapa tulifuta na tukairejesha wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo utaratibu ni huohuo mtakapokuwa mmejiridhisha huko basi sheria itakuja hapa sisi ndiyo tunafuta kwa sababu mtakazotuambia ili isilete mkanganyiko. Nadhani ufafanuzi ulioutoa ndiyo ambao unasimama kwamba Wizara na Taasisi zenu zimepewa taarifa kwamba kuna hiyo nia ya kufuta. Kwa hivyo watu wajieleze kama wanaona kwamba bado wana umuhimu au wengine waungane na mambo kama hayo ili isije ikaonekana kwamba kuna utaratibu nje ya ule utaratibu uliowekwa kisheria ambao tumetunga sisi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge alisimama hapa Mheshimiwa Dkt. Kimei akisema na yeye anataka kutoa shilingi sasa utaratibu wetu wa Mbunge anayekuwa ana hoja kwenye kifungu cha kutoa shilingi lazima taarifa niwe nayo hapa mbele kutoka kwenye pande mbili kwa maana ya chama chenye Wabunge wengi humu ndani na wale walio wachache. Sasa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge hapa mbele, lakini utaruhusiwa kwenye

mafungu mengine huko mbele. Kwa maana ya mshahara, kikanuni ndiyo utaratibu ambao tumejiwekea.

Mheshimiwa Kimei hebu ngoja, washa kisemeo sikusikii.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni rahisi sana siyo gumu kama la Mheshimiwa Mpina, ni dogo tu. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, kwa sababu inabidi niendeshe kikanuni atasimama siku nyingine mtu mwingine nitakuwa nimemwonea nikimnyima. Unasema jina lako ulipeleka kwa Katibu? Basi hapa mbele hajaleta na kwa sababu hajaleta, utaratibu wetu ule wa kawaida ndiyo inabidi utumike, nikibadili utaratibu maana yake nitakuwa nimebadili utaratibu kila tutakapokaa hapa mtu mwingine akisimama itabidi nimruhusu. Kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, hoja ya Mshahara wa Waziri ilikuwa ni jina moja na ndiyo hilo ambalo tumeshalikamilisha hapa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Account Unit*...................Sh. 607,040,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*.....Sh. 1,502,032,000
Kifungu 1004 - *Legal Unit*.................................................Sh. 476,980,000
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*.....Sh. 749,792,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 588,444,000
Kifungu 1007 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 554,072,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*...................................Sh. 714,516,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 845,084,000
Kifungu 2001 - *Public Sector Investment Division*......Sh.1,686,336,000
Kifungu 2002 - *Private Sector Investment Division*....Sh. 6,714,150,000
Kifungu 2004 - *Business Environment Unit*.....................Sh. 785,556,300

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management Division*.......................Sh. 6,508,583,008
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Division*........Sh. 1,051,211,020
Kifungu 1003 - *Planning, Research and Development Division*...............................................Sh. 2,637,914,864
Kifungu 1004 - *Legal Services Division*.......................Sh. 1,141,602,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 375,110,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Division*..........................Sh. 1,844,677,584
Kifungu 1007 - *Public Relations and Communication Unit*.......................................................Sh. 509,974,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*..................................Sh. 716,332,020
Kifungu 1009 - *Risk Management Unit*..........................Sh. 642,520,000
Kifungu 1010 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 613,765,000
Kifungu 2001 - *Public Investment Management Division*.............Sh. 0
Kifungu 2002 - *Funds Management and Investment Division*............................Sh. 1,452,595,012
Kifungu 3001 – *Privatization and Monitoring* ...............................Sh. 0
Kifungu 4001 - *Management Service Division*..........Sh. 1,900,100,000
Kifungu 4002 - *Performance Management - Commercial Entities Division*............Sh. 22,296,884,492
Kifungu 4003 - *Performance Management - Non-Commercial Entities Division*.....Sh. 2,096,140,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*...................Sh. 5,891,647,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,138,296,000
Kifungu 1003 - *Planning and Budgeting Division*......Sh. 2,225,920,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh. 934,000,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 792,280,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 834,520,000
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*................................Sh. 808,000,000

Kifungu1008 - *Information and Communication Technology unit*......................................*Sh.* 932,000,000
Kifungu1009 - *Risk Management and Quality Assurance Unit*.......................................Sh. 754,000,000
Kifungu 1010 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 813,280,000
Kifungu 2001 - *National Planning Division*.................Sh. 9,869,297,000
Kifungu2002 - *Trade and Private Sector Engagement Division*.................................................Sh. 2,969,080,000
Kifungu 2003 - *National Key Results Areas Division*..Sh. 2,640,140,000
Kifungu 2004 - *Performance Monitoring and Evaluation Division*...............................Sh.4,390,602,000
Kifungu 2005 - *Innovation, Research and Development Division*........................Sh. 2,813,188,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE – MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 11 – Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Department*........Sh. 197,174,619
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*.........Sh. 1,138,081,385
Kifungu 2001 - *Public Sector Investment Division*........Sh. 657,248,729
Kifungu 2002 - *Private Sector Investment Division*....Sh. 5,978,739,267
Kifungu 2004 - *Business Environment Unit*................Sh. 11,377,970,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Division*.............Sh. 64,550,000
Kifungu 1003 - *Planning, Research and Development Division*...................................................Sh. 263,552,000
Kifungu 1006 - *Information and Communication Technology Division*..............................Sh. 182,358,000
Kifungu 1009 - *Risk Management Unit*...........................Sh. 81,250,000
Kifungu 2001 - *Public Investment Management Division*.............Sh. 0

Kifungu 2002 - *Funds Management and Investment Division*.................................................. Sh. 167,800,000
Kifungu 3001 - *Privatization and Monitoring*.................................Sh. 0
Kifungu 4001 - *Management Service Division*.............Sh. 113,038,000
Kifungu 4002 - *Performance Management - Commercial Entities Division*......................................Sh. 147,510,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4003 - *Performance Management Non-Commercial Entities Division*.............Sh. 1,289,658,000

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja, Waheshimiwa Wabunge Kifungu 4003 kinasomwa upya.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 4003 – *Performance Management - Non-Commercial Entities Division*................Sh. 269,600,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**

Kifungu 1003 - *Planning and Budgeting Division*......Sh. 8,415,380,000
Kifungu 2001 - *National Planning Division*....................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi, mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Hivyo, naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono na kama ilivyo ada, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa* Mwaka wa Fedha *2024/2025 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na wengi kusema ndiyo hoja hii imepitishwa rasmi na Bunge. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa hoja yake aliyoileta ambayo Waheshimiwa Wabunge pamoja na maoni na mapendekezo mbalimbali walioyatoa wameafiki Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii. Kwa hiyo tunawatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri pamoja na watumishi wenzako katika ofisi hii katika kutekeleza yale ambayo umewaahidi Wabunge kupitia hotuba yako.

Baada ya kusema hayo naishukuru Kamati yetu imefanya kazi nzuri sana ya kushirikiana na Ofisi hii mpaka wamefikia hapo. Tumesikia mambo mengi mazuri ambayo Kamati imeshauri. Kama mlivyomsikia Waziri aliposema hapa inaonesha wana ushirikiano mzuri sana. Kwa hiyo tunakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa Kamati hii na Wabunge wote mlioshiriki, tunawashukuru kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, mmetoa maoni mengi sana kwa sababu Ofisi hii ni mpya na kwa kweli sote tunamtakia kila heri Mheshimiwa Waziri na tuna matarajio makubwa sana na tumefurahi kwamba na wewe wakati ukitoa ufafanuzi umeonesha kwamba umezielewa hoja za Wabunge na Watanzania sehemu mbalimbali mambo wanayoyazungumza kuhusu matarajio ya Ofisi hii ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kutuweka sote tuwe na mwelekeo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri umesema vizuri kwamba Serikali ni moja, ni kweli lakini kwa sababu walioko kwenye hizi ofisi ni binadamu kila mtu anaweza kuwa na mawazo yake. Sasa tunatamani mawazo hayo yote yawe na mwelekeo mmoja ili tusiwe tunaenda mbele na kurudi nyuma. Kwenye Kamati hizi tutaendelea kupata taarifa, lakini yako maeneo mbalimbali ambayo hawa wanapendekeza hizi baadaye wakienda kufanya ukaguzi wanagundua jambo lilitekelezwa mahali ambapo halikupaswa kutekelezwa.

Mheshimiwa Waziri, mifano midogo ambayo tunakuhitaji uifanyie kazi, kwa mfano, katika eneo hili la huduma za jamii tunazungumza kuhusu maji, elimu na afya kama mifano. Kituo cha afya kinapoenda kujengwa mahali kwa kuwa tu Mbunge ameomba, hapana. Ofisi sasa ipo kwa ajili ya mipango. Lazima mtazame wingi wa watu na mwendo wa huduma ili kila Mtanzania apate haki ileile. Siyo mwenye Mbunge msemaji na mwenye Mbunge mpole, watofautiane, hapana.

Ziko taarifa za Kamati hapa ambazo nimezipitia kituo cha afya kimejengwa mahali mpaka leo kina majani tu; kwa nini? Hakuna watu wa kuwahudumia. Hata watumishi wangeenda

hakuna watu wa kupata huduma. Ukiuliza kimejengwa kwa mipango ipi, ndiyo hivyo sasa hakukuwa na ofisi ya mipango. Kwa hiyo hawawezi kulaumiwa sana maadam walipewa maelekezo kijengwe pale. Tunaamini kwa kuwepo kwa ofisi hii tutakapokuwa tunazungumza maji kwenda mahali Fulani, kuna mpango kabisa. Yaani nchi imejipanga kwamba maji tutapeleka hapa na hapa, umeme hapa na hapa na sababu zetu ni hizi na hizi. Hakuna sababu ya Mbunge kusema hapa kiwanda cha ngano kimefungwa wakati huko ndiko ambako ngano inalimwa.

Sasa lazima kuwe na kuoanisha na kuoanisha huko kwa kweli tunaitegemea ofisi yako; kwa sababu haya ya kisera kwa kweli kila mtu anaweza kuwa na mawazo yake, lakini tunatamani yote yawe yanajielekeza kwenye utekelezaji wa Mpango wa Taifa ambao kwa kweli utakuwa unatokana na ofisi yako. Ile dira sawa lakini tafsiri yake lazima itafsiriwe na ofisi yako.

Tunalalamika kuhusu ajira na tunazungumza kuhusu sayansi, kila mtu umekuwa ni wimbo, lakini je ni kweli nchi yetu hii tunahitaji watu wote wakasome sayansi mpaka leo, ama tumeshafika mahali ambapo tunapaswa kuwatia moyo wasome masomo yote, au bado tuna shida kwenye sayansi tuendelee kusoma sayansi? Tusipoweka mipango hata vyuo vyetu vinaendelea kufundisha yale masomo ambayo huku nje hayahitajiki. Kwa hiyo watoto wanazunguka na bahasha. Sasa hayo yote kwa kweli tunakutegemea wewe na tutakutwisha mzigo. *(Makofi)*

Umejitoa kwenye ujana lakini nadhani kuna miaka mipya imetajwa ya vijana, kwa hiyo usijitoe. Sisi tumekuita kijana kwa kuona unazo nguvu za kubeba haya yote tunayokwambia. Tunaamini kwa sababu hii ni ofisi mpya, tunakoelekea ofisi itakuwa imeshakomaa na kwa kweli tutakuwa tunashangaa kama huku tutakuwa tunasema watoto wasome sayansi na huku tunaona watoto wanahitajika kusoma historia, halafu watu wa kufundisha pengine hawapo ama tunashangaa kila mtu anaenda kusoma ualimu wakati sasa ofisi ipo. Hakuna sababu ya watoto wote kwenda kusoma ualimu wengine walipaswa wakasome huko ambako pengine ndiyo *Dar es Salaam Institute of Technology*.

Nilimsikia Mbunge mmoja amesema *IDM* Mzumbe irejee na mimi kwa kweli namuunga mkono. Naamini nanyi mtalitazama kwenye Serikali; kwa sababu haiwezekani tukawa ni nchi ambayo tunafikiri kila mtu lazima awe na *degree,* hapana. Wako wengine siyo lazima wawe na *degree* na bado watakuwa wasomi. Humu ndani pia wamo ambao ni wazuri kabisa na wengine ni Mawaziri hawana *degree* na wako vizuri kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama Taifa tunakutegemea sana Mheshimiwa Waziri utupangie mambo haya vizuri ili twende vizuri. Siyo kila mtu anajiendea vile anavyoona hapa panawezekana, pale panawezekana na huku inapatikana mikopo, basi nikasome tu hicho hicho ambacho mkopo unapatikana. Kama nchi lazima tujipange.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.36 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 23 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*